# Nipashe

Jumamosi Septemba 7, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580017

www.ippmedia.com


MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

## Bunge latahadharisha usajili wa simu kwa alama za vidole

UKURASA 3




UKURASA 13

# JPM awachongea watendaji Museveni

UKURASA 2



Rais John Magufuli na Rais wa Uganda, Yoweri Museveni, wakipunga mikono kabla ya kufungua Kongamano la Biashara kati ya nchi hizo mbili katika ukumbi wa Mkutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Masharti ununuzi korosho yapozwa

UKURASA 3

## Ubaguzi waziibua NGO

• **Zataka** SADC kutoa kauli, kuchukua hatua... *Ukurasa 2*


TAIFA STARS vs BURUNDI

SEPTEMBA 8, 2019 • UWANJA WA TAIFA




215393302

HAIUZWI KWA WALIO NA UMRI CHINI YA MIAKA 18. TAFADHALI KUNYWA KISTAARABU.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akizungumza na Mbunge wa Iramba Magharibi, Mwigulu Nchemba (kushoto), na Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (katikati), bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: OWM**

# JPM amtaka Museveni atumbue watendaji

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli ameeleza kukerwa na ucheleweshwaji wa mradi wa bomba la mafuta kutoka Tanga nchini Tanzania hadi Uganda, unaofanywa na baadhi ya watendaji wa serikali ya nchi yake.

Kutokana na kero hiyo, amemshauri Rais Yoweri Museveni wa nchi hiyo kuwachukulia hatua baadhi ya watendaji wa Mamlaka ya Mapato Uganda (URA) huku akimtolea mfano wa mabadiliko aliyoyafanya kwa muda wa miaka mitatu na nusu kwa kubadilisha makamishna wakuu watano wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Mei 21, 2017, Rais Magufuli na Rais Museveni walitia saini mkataba wa ujenzi wa bomba hilo ambalo linatoka Ohima, Uganda hadi mkoani Tanga.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam kwenye kongamano la biashara kati ya Tanzania na Uganda lililohudhuriwa pia na Rais huyo wa Uganda, Rais Magufuli alisema: "Suala hili la bomba la mafuta linaniuma, tulibidi tupeleke mabadiliko ya sheria ya kodi bungeni kwa ajili ya kufanikisha bomba hili lijengwe," alisema.

"Leo (jana) ninataka niwape siri moja, nilikuwa ninamwuliza Rais Museveni, mbona unachelewesha bomba la mafuta kwa sababu ya kodi ambayo umekataa kuikubali, kodi yenyewe ni dola 600 wakati utakuwa unatengeneza dola bilioni 80.

"Rais Museveni jitoe muhanga kwenye hii kodi ndogo ili utengeneze ajira na kupata fedha kwa kipindi cha muda mrefu. Watu wako wa URA wasikucheleweshe, mzee sisi tulitaka hiyo pipeline (bomba la mafuta) iitwe 'Kabuta Pipeline' siku tutakayoifungua,' aliongeza. Rais Magufuli alisema wanatakiwa kwenda mbele katika biashara, hivyo ili kupata faida kubwa lazima kupoteza kidogo ili wapate kikubwa.

"Watu wameanza kupata ajira na kuonyesha bomba linapita wapi. Hapa Tanzania mikoa minane itafaidika na bomba hili la mafuta likianza, takwimu za ukusanyaji mapato Uganda zitaongoza katika uchumi Afrika. Kwa nini ucheleweshwe na watendaji? Mzee yawezekana umekuwa mpole wakati ukipigana, sasa uongeze ukali kidogo kwenye hili," alisema.

Rais Magufuli alisema ameamua kueleza hayo kwa sababu wafanyabiashara ni watu wa kupoteza katika biashara zao ndio maana wanafanikiwa.

"Sisi watendaji serikali hatujali kwa sababu muda wote tunapata mishahara, mfanyabiashara asipo pata faida anakufa, lakini sisi mshahara upo hata kama hatukusanyi kodi, hata kama maendeleo hayasongi mbele hatujali, watendaji wote Uganda na Tanzania lazima tuwezeshe miradi ili tusonge mbele na kutoa ajira," alisema.

Pia Rais Magufuli aliwaeleza wawekezaji wa Uganda kuwa milango ya uwekezaji ipo wazi kwa sababu mazingira ya uwekezaji yanachangiwa na amani, utulivu na sheria zinazowalinda.

Hata hivyo, aliwataka wafuate bei elekezi zilizowekwa, wasiwanyonye wazalishaji.

"Kondamano hili limekuja muda muafaka nitashangaa leo tumekuja na Rais Museveni tena kwa kuwapenda Rais Museveni akamleta mke wake, alafu tumalize kongamano hakuna biashara yoyote ya iliyoongezeka.

"Nitawashangaa wafanyabiashara wa maeneo yote. Ila punguzeni maneno pawe na vitendo kwenye biashara, wakati mwingine maneno ni mengi mno, unajua wafanyabiashara mmekuwa na maneno mengi, visingizio vingi hakuna matendo, tufanye biashara, kama kuna changamoto za msingi tumekubaliana na Rais, zileteni tutazimaliza haraka.

"Nina uhakika mkiamua, mawaziri wakaamua, makatibu wakuu wakaamua, watendaji wakaamua, wakuu wa mikoa wakaamua hakuna kinachoshindikana."

Rais Magufuli mwezi uliopita akiwa mkoani Kagera alikuta taarifa kuwa wanataka kuuza kahawa nchini Uganda kwa sababu bei ni nzuri kwa kilo ni 1600.

"Rais Museveni kama wapo wanataka kuja kununua kahawa waje kuinunua kwa kilo waondoke, wasitafute visingizio, sisi wote ni waafrika na ni ndugu, ninawaomba yaliyoshindikana miaka 50 iliyopita sasa yafanikiwe," alisema.

Rais Magufuli alisema biashara na uwekezaji kati ya nchi hizo mbili bado kiwango ni kidogo hasa ikilinganishwa na fursa zinazopatikana Tanzania na Uganda.

"Mwaka 2018 thamani ya biashara ilikuwa bilioni 388. 5 sawa na ongezeko la asilimia 207 ikilinganishwa mwaka 2017 ilikuwa bilioni 116.7. Nchi ya Uganda inayo miradi 22 tu Tanzania yenye thamani ya dola za Marekani 143.25 iliyotoa ajira 2230 tu," alisema.

Aliongeza kuwa, "Kiwango cha mizigo ya Uganda inayoingizwa kupitia Bandari ya Dar es Salaam kwa mwaka 2017/18, tani 167 kati ya tani milioni 7.1 ya bidhaa zinazoingizwa Uganda, ndizo zilizopita, hiki ni kiwango kidogo."

Akilinganisha na nchi ya Kenya, Rais Magufuli wakati Uganda ikiwa na Kampuni 22 zilizowekeza Tanzania, Kenya ina kampuni 504.

Naye Rais Museveni alisema: "Watu wanajiuliza kwa nini watu wanaweka vikwazo kwenye shughuli za kibiashara hasa watumishi wa serikali ni kwa sababu hawaelewi umuhimu wa biashara."

"Kwenye vichwa vyao wanafikiri kuna njia nyingine ya kuinua ustawi wa jamii wa watu bila biashara, wanafikiri ipo njia nyingine nchi itakua kimaendeleo bila biashara, hawajui jinsi nchi inavyokua, hawajui" alisema.

"Hawajasoma kitabu cha mzungu mmoja, Adam Smith ambacho aliandika mwaka 1776, 'The Wealth of Nations' (utajiri wa mataifa), wanafikiri wanasaidia wafanyabiashara."

Alisema binadamu wamekuwa hapa miaka milioni nne na nusu na katika kipindi hicho chote, wamekuwa wakikandamizwa kwa shinda za aina mbili, zinazotokana na asili na binadamu mwingine kumkandamiza mwingine.

"Lazima Afrika wajiulize nchi kama China ina watu bilioni 1.3 na India hivyo hivyo, ndani wana soko kubwa kama nchi. Lakini hayo masoko ya China na India hayawatoshi wanatafuta masoko kwingine. Lakini Mganda akiona watu milioni 41 wanafikiri wengi sana, haitaji masoko mengine, wanafikiri wamefika, hii ni hatari," alisema.

## NGO zataka SADC kuchukua hatua ubaguzi

**Na Beatrice Moses**

TAASISI tatu zisizo za kiserikali zimemshauri Mwenyekiti Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Rais John Magufuli, kuitisha mkutano wa dharura wa wakuu wa nchi wanachama kujadili vitendo vya ubaguzi dhidi ya wageni wa kiafrika nchini Afrika Kusini.

Wakitoa tamko la kulaani kinachoendelea nchini Afrika Kusini, taasisi hizo, Action for Change (ACHA), The Right Way (TRW) na Mtandao wa Mashirika ya Kutetea Haki za Binadamu Kusini mwa Afrika (Sahringon), zilizema kauli ya kiongozi huyo na wengine italeta mabadiliko.

"Tuna imani kuwa Rais wetu Magufuli akidhamiria jambo analifanikisha. Tunaamini kwamba anaweza kujadiliana na viongozi wenzake wa nchi hizi ili kupata suluhisho la kudumu," alisema Mratibu wa Kitaifa wa Sahringon, Martina Kabisama.

Alisema kwa historia ya Tanzania kusimamia harakati za ukombozi kwenye nchi nyingine, suala la kusaidia Afrika Kusini kuachana na mashambulizi dhidi ya waafrika wenzao linahitaji msaada.

Kabisama alisema ubaguzi unaotokea nchini humo pia unaonekana kujitokeza kwenye nchi nyingine, na kwamba kauli ya pamoja ya viongozi hao katika kukemea itasaidia kuwakumbusha wajibu na umuhimu wa mshikamano.

"Mfano mzuri ni ule wa hivi karibuni nchini Kenya wakati mbunge mmoja alidiriki kutoa kauli inayoumiza kwa wale aliowaita wageni," alisema Kanisama.

Alisema wanasikitika uzalendo ambao uliasisiwa na waasisi wa mataifa ya Afrika umevamiwa na sasa unasinyaa, jambo ambalo halipaswi kuachwa hivyo.

"Ni suala la kupiga kengele kwamba Waafrika kwa pamoja waungane na kuainisha zaidi chanzo cha ubaguzi huu mpya unaobagua Waafrika wenzao," alisema.

Mwenyekiti wa ACHA, Justina Shauri, alisema kuwa wanatarajia kutakuwa na mikakati ya kuvunja minyororo ya utengano wa namna hii na unyanyasaji ambavyo vyote ni dalili ya kutengana na si kuungana Muungano wa Afrika.

"Viongozi wa Afrika hawana budi kurejea uongozi uliotukuka kujiamini na weledi, kutengeneza mitandao na viongozi wenzao wa Afrika ili kupambanua vikwazo kwa pamoja na kupambana kwa pamoja dhidi ya ubaguzi wa watu wa mataifa unaoota mizizi katika ukanda huu wa dunia," alisema.

Mwenyekiti wa TRW, Sebastian Masaki, alisema vitendo vya ukatili vinavyofanywa nchini humo vinavunja haki za kibinadamu na fursa ya maendeleo ya nchi hiyo ikiwa ni pamoja na kuwa fedheha kwa wanaotekeleza vitendo hivyo.

"Kinachotokea Afrika Kusini na sehemu zingine za bara letu ni cha kihistoria. Machafuko ya ukatili dhidi ya wageni yameachwa bila kushughulikiwa kikamilifu na viongozi husika," alisema Masaki.

Kutokana na mashambulizi yanayoendelea nchini humo, baadhi ya nchi kama Nigeria na Zambia zimetangaza kuondoa raia wake, huku viongozi mbalimbali duniani wakilaani yanayoendelea nchini humo na kuitaka serikali kuchukua hatua katika kukomesha vitendo hivyo.

Tanzania kwa upande wake imesitisha safari za Ndege ya Shirika la Ndege Tanzania (ATCL), kwenda nchini humo kutokana na vurugu zinazoendelea.

# Masharti ununuzi wa korosho yalegezwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema mfumo wa ununuzi wa korosho kwa msimu ujao utabadilika na sasa wafanyabiashara watanunua bidhaa hiyo na serikali itakuwa inaangalia utaratibu unaotumika ili kuepusha athari kwa wakulima.

Sambamba na hilo, wiki ijayo Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, anatarajiwa kutangaza utaratibu na namna gani ya mfumo wa ununuzi wa korosho utakavyokuwa kwa msimu huo.

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema hayo jana bungeni jijini hapa alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Newala Vijijini (CCM), Rashid Ajali, aliyetaka kujua serikali ina mpango gani juu ya bei ya korosho kwa msimu ujao ambao imebaki miezi mitatu ili kuepuka mgogoro kama uliojitokeza mwaka jana ili bei ya korosho ibaki kati ya mkulima na mfanyabiashara.

Akijibu swali hilo, Bashe alisema mbali na serikali kuangalia utaratibu huo wa wafanyabiashara usiathiri wakulima, pia serikali itatangaza utaratibu wa kuomba zabuni kwa uwazi.

"Hatutatumia utaratibu wa viboksi na usiku wa manane watu kwenda kutengeneza 'cartel' ambayo siku ya mwisho inaenda kutuletea matatizo. Transparency (uwazi) itakuwa msingi wa ununuzi wa korosho na matatizo yale yalijojitokeza hayatajitokeza," alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge huyo alihoji serikali imejiandaaje ili kuwapatia wakulima wa korosho pembejeo za uhakika na kwa wakati.

Akijibu swali hilo, Bashe alisema kuanzia mwaka 2012/13 serikali kupitia Bodi ya Korosho ilianzisha utaratibu wa ununuzi wa pamoja wa pembejeo za zao hilo kwa lengo la kuhakikisha wakulima wa korosho wanapata pembejeo bora za uhakika kwa wakati.

"Aidha, utaratibu huo unatoa unafuu wa bei kwa bei kwa mkulima, udhibiti wa ubora na upatikanaji wa pembejeo hizo kwa wakati," alisema.

Bashe alisema mahitaji ya viatilifu vya zao la korosho katika msimu wa mwaka 2019/20 ni tani 30,000 za salfa ya unga na lita 500,000 za viuatilifu vya maji.

"Kiasi cha viuatilifu kilichopo nchini tangu mwanzo wa msimu wa 2019/20 ni tani 19,000 za salfa ya unga na lita 270,000 viuatilifu vya maji, kiasi hicho kipo katika Bodi ya Korosho Tanzania," alisema.



Sehemu ya malori 300, yakiwa yamekwama kwenye foleni ya kuingia katika Bandari ya Dar es Salaam jana, kwaajili kupakia mizigo kwa karibu siku nne sasa, ambapo madereva wake, wamelalamikia mizani na mtandao wa kutoa vibali unaofanyakazi taratibu. **PICHA: JOHN BADI**

## Viongozi Afrika wamlilia Mugabe

**Na Waandishi Wetu**

VIONGOZI mbalimbali wametuma salamu za rambirambi kutokana na kifo cha Rais wa zamani wa Zimbabwe, Robert Mugabe.

Mugabe ambaye alipelekwa nchini Singapore tangu Aprili, mwaka huu, kwa ajili ya matibabu ya maradhi yaliyokuwa yakimkabili, alifariki dunia usiku wa kuamkia jana akiwa na umri wa miaka 95.

Taarifa za kifo chake zilitangazwa na Rais wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa, kupitia mtandao wa Twitter jana.

Baada ya taarifa za kifo hicho, baadhi ya wakuu wa nchi za Afrika kwa nyakati tofauti walituma salamu za rambirambi kwa taifa hilo kupitia kurasa zao za Twitter.

Rais John Magufuli aliandika: "Nimepokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kifo cha Rais mstaafu na Baba wa Taifa la Zimbabwe, mzee Robert Mugabe.

"Afrika imepoteza mmoja wa viongozi jasiri, shupavu, mwanamajumui wa Afrika na aliyekataa ukoloni kwa vitendo. Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. Amina," aliandika Rais Magufuli kupitia ukurasa wake wa Twitter.

INAENDELEA UK.7

# Bunge latoa angalizo usajili alama za vidole

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

BUNGE limeitaka serikali kuweka katazo kwa kampuni za simu na mawakala wao kutouza wala kuunganisha kadi za simu ambazo hazijasajiliwa kwa mfumo wa alama za vidole.

Limesema hatua hiyo itawaondolea wananchi mzigo wa adhabu watakaoupata pindi watakapotumia kadi za simu ambazo hazijasajiliwa kwenye mfumo huo licha ya kununua kadi hizo kihalali.

Akiwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mjumbe wa Kamati hiyo, Asha Abdallah Juma, alisema serikali inapaswa kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu madhara ya kutumia laini za simu zisizosajiliwa kwa mfumo wa alama za vidole.

"Serikali ijikite zaidi kwenye teknolojia ya kuzima simu zote ambazo zitakuwa hazijasajiliwa kwa Mfumo wa Biometria (alama za vidole) baada ya muda utakaokuwa umetolewa," alisema.

Asha alieleza hatua hiyo ni muhimu badala ya kujikita kwenye adhabu kali ambazo zinaweza kukosa uhalisia kwa wananchi wa kawaida ambao ndiyo watumiaji wa simu.

Mbunge huyo wa Viti Maalum (CCM), alibainisha kuwa kihalisia makosa hayo ni ya kampuni za simu za mikononi na mawakala wao ambazo wanauza kadi za simu bila kuhakikisha zimesajiliwa kwenye mfumo wa alama za vidole.

Vilevile, alisema serikali inapaswa kuhakikisha mfumo wa utoaji vitambulisho vya taifa unarahisishwa kwa kuwafikia wananchi wote. Awali, akiwasilisha mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Mawasiliano ya Kieletroniki na Posta, Sura ya 309, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Prof. Aderaldus Kilangi, alisema marekebisho hayo ni muhimu kwa maslahi ya umma.

Alisema yana lengo la kuimarisha udhibiti wa matumizi ya huduma za mawasiliano ya kieletroniki na kudhibiti watumiaji wenye lengo la kurubuni wananchi kwa kutumia kadi za simu zisizosajiliwa kwa majina tofauti.

"Pia yanalenga kuimarisha usalama wa watumiaji wa huduma za kimtandao ili kupunguza wimbi la uhalifu na kuhuisha sheria kuendana na hali ya sasa ya usajili wa laini za simu kwa alama za vidole," alisema.

Akiwasilisha maoni ya kambi rasmi ya upinzani bungeni kuhusu marekebisho hayo, Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Latifah Chande, alisema kambi hiyo inaona ni jukumu la kampuni za simu kuhakikisha laini za simu ambayo haijasajiliwa haifanyi kazi.

"Endapo kutakuwa na laini ambazo hazijasajiliwa zinafanya kazi basi kosa hilo litakuwa la kampuni ya simu na siyo kosa la mtumiaji wa huduma hizo," alisema.


**NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kampuni ya ***WAUNGWANA AUCTION MART, MELVA INTERNATIONAL LIMITED, JAGRO ENTERPRISES LIMITED and KOTI BROTHERS AUCTION COMAPANY*** kwa niaba ya **AccessBank Tanzania Limited** tunatoa Notisi na tangazo la mnada kwa mali zilizowekwa kama dhamana ya mikopo ambapo wateja husika wameshindwa kulipa mikopo yao kwa mujibu wa mikataba husika. Hivyo basi ifahamike kuwa utakapopita muda wa siku kumi na nne tangu kutoka kwa gazeti hili,Dhamana husika zitauzwa kwa njia ya mnada . Mnada utafanyika sehemu dhamana husika zilipo siku na tarehe kama vilivyotajwa kwenye jedwali hapo chini.

| S/N | TAWI HISIKA | JINA LA MTEJA | KAMPUNI HUSIKA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | SEHEMU DHAMANA ILIPO | TEREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MKUNGUNI | SHIRIMA/MATEI,PETER | WAUNGWANA AUCTION MART | SHIRIMA/MATEI,PETER | NYUMBA | KIMARA | 23/9/2019 SAA 10:00AM |
| 2 | MBEYA | FURAHA BAKERY | JAGRO ENTREPRESES CO. LTD | FURAHA BAKERY | NYUMBA | MWAKIBETE | 23/9/2019 SAA 10:00AM |
| 3 | MBEYA | MWALWEGA/A,JANKEN | KOTI BROTHERS AUCTION CO. | MWALWEGA/A,JANKEN | NYUMBA | VETA | 23/9/2019 SAA 10:00AM |
| 4 | HEAD OFFICE | ESTHER E. KISAMO | MELVA INTERNATIONAL LIMITED | ESTHER E. KISAMO | KIWANJA | TEMEKE - MWAPEMBA | 23/09/2019 |
| 5 | HEAD OFFICE | SHAMILA ALLY MDACHI | MELVA INTERNATIONAL LIMITED | SHAMILA ALLY MDACHI | KIWANJA | LUGURUNI - KIBAMBA | 24/09/2019 |
| 6 | HEAD OFFICE | ZENA SAID MOHAMED | MELVA INTERNATIONAL LIMITED | ZENA SAID MOHAMED | KIWANJA | MBONDOLE - ILALA | 23/09/2019 |

**MASHARTI YA MNAD**

1. UKAGUZI UNARUHUSIWA MARA USOMAPO TANGAZO HILI.
2. MNUNUZI ATALAZIMIKA KULIPA MALIPO YA 25% YA FEDHA TASLIMU PAPO HAPO NA 75% BAADA YA SIKU 14 TOKA SIKU YA MNADA KUFANYIKA NA UKISHINDWA KULIPA MALIPO YALIYOBAKI MNADA UTARUDIWA NA FEDHA ULIZO LIPA HAZITARUDISHWA
3. GHARAMA ZA KUBADILISHA UMILIKI NI ZA MNUNUZI MWENYEWE, KUMBUKA VIGEZO NA MASHARTI KUZINGATIWA.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI**
**PIGA SIMU NO. 0713077474-Waungwana auction mart**
**0757 785 247 Koti Brothers Auction Coampany**
**0719 974 916 Melva International Limited**

**WOTE MNAKARIBISHWA.**

215409202

# Sakata madeni maiti laibua zogo bungeni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SUALA la maiti kulipishwa fedha, jana liliibua zogo bungeni baada ya wabunge kudai kuwa maiti zimekuwa zikilipishwa fedha pindi mgonjwa anapofariki dunia na kuomba serikali kubadili mfumo huo.

Hata hivyo, serikali imesema kinacholipwa ni gharama za matibabu na si maiti na kwamba imekuwa ikitoa msamaha wa gharama kwa wanaoshindwa kulipia na kutolea mfano kuwa Hospitali ya Temeke ambayo ndani ya miezi mitatu, imesamehe Sh. Milioni 500 kwa wagonjwa 14,574.

Hali hiyo ilijitokeza bungeni katika kipindi cha 'Maswali na Majibu' kutokana na swali la msingi lililoulizwa na Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Susan Lyimo.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema serikali ina utaratibu wa kutoza fedha miili iliyohifadhiwa katika vyumba vya kuhifadhia maiti hospitalini, hivyo kusababisha vikwazo na simanzi kwa familia zisizokuwa na uwezo wa kulipa gharama hizo.

"Je, lini serikali itaacha kutoza fedha miili ya watu wanaofia hospitalini na kuhifadhiwa katika vyumba vya kuhifadhiwa maiti ili kupunguza simanzi kwa wafiwa?" alihoji.

Katika swali lake la nyongeza, Lyimo alisema ni kweli kuwa sera ya afya inazungumzia suala la uchangiaji, lakini alihoji kama serikali itakubaliana naye kuwa Tanzania watu wengi bado ni masikini.

Alisema maiti inapaswa kupata heshima yake ndiyo maana inahifadhiwa lakini uhalisia unaonyesha wazi kwamba watu wengi wameshindwa kutoa maiti hizo.

"Matokeo yake tumeona juzi juzi pale Muhimbili, Rais John Magufuli akitoa takribani Sh. milioni tano kwa yule mama kwa ajili hiyo. Sasa najiuliza Rais atakwenda kila sehemu kutoa hizo fedha?" alihoji.

Alihoji serikali ina utaratibu gani wa muda mfupi na mrefu kuhakikisha wale wenye matatizo makubwa ambao wanashindwa kabisa wanakabidhiwa maiti zao kwa wakati.

Katika swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Faida Mohammed Bakari, alisema inasikitisha kuona maiti zinalipiwa wakati kila mwanadamu ni maiti.

Alisema kama mtu hajapata fedha ya kuilipia maiti hairuhusiwi na familia na kushauri serikali kubadili mfumo huo na kuliomba bunge kukubali suala hilo kuwasilishwa kwenye chombo hicho ili utozaji wa fedha hizo uondolewe kwa kuwa maiti ina heshima zake.

"Je, ikiwa mtu huyo maskini anatoka kijijini lakini maiti yake hakuweza kuilipia na siku zinaongezeka kukaa pale hivyo gharama kuongezeka, Je serikali inaupeleka wapi ule mwili anazikwa kwa heshima zote au la," alihoji.

Akitoa majibu kwa wabunge hao, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alisema maiti hailipishwi bali kinacholipwa ni gharama za matibabu alizopewa marehemu alipokuwa anapatiwa huduma za matibabu.

"Kinachofanyika ni kulipia gharama ambazo mgonjwa amepewa na kutolea mfano kuwa kama mgonjwa amelazwa chumba cha uangalizi maalum (ICU) kwa siku ni Sh. 500,000 kwa huduma za dawa muhimu na hiyo ni kwa Hospitali ya Muhimbili, lakini hospitali binafsi ni Sh. milioni 2.5 kwa siku,"balisema.

Pia alisema katika Hospitali ya Temeke katika kipindi kati ya Juni na Agosti, mwaka huu, wagonjwa wa msamaha walikuwa 14,574. Juni walikuwa 4,949, Julai 4,816 na Agosti 4,809 na kiasi kilichosamehewa ni zaidi ya Sh. milioni 500.

Wakati akiendelea kutoa ufafanuzi huo, wabunge walionyesha kupingana na majibu yake hali iliyomlazimu Mwenyekiti wa Bunge, Najma Murtaza Giga, kuwatuliza na kuwataka kama kuna tatizo baadaye wamwone Waziri huyo.

Baada ya kuwatuliza wabunge, Mwenyekiti huyo alimruhusu Waziri kuendelea kutoa ufafanuzi na kusisitiza kuwa wagonjwa wengi wamesamehewa kutokana na kushindwa kulipa gharama kwa hiyo badala ya wabunge kulalamika wahimize wananchi wakate bima za afya.

"Mfano tukio la mama aliyefanya sherehe kisa mumewe kurudi nyumbani baada ya kutekwa na mchepuko (nyumba ndogo) muda mrefu sasa ametumia gharama kiasi gani lakini bima ya afya hawana, wanalalamika tu," alisema.

Awali, akijibu maswali ya wabunge hao, Naibu Waziri wa Afya, Dk. Faustine Ndugulile alisema ili miili ya marehemu wanaofia hospitalini au nje ya hospitali ihifadhiwe na kusitiriwa kwa heshima, inahitaji kutunzwa kwenye majokofu yenye ubaridi mkali na wakati mwingine kuwekewa dawa za kusaidia isiharibike.

Aliongeza kuwa ili kuondokana na changamoto hizo, wananchi wanahimizwa kujiunga na Bima ya Afya kwa lengo la kupunguza gharama za matibabu toka mfukoni.

"Mtu anapokwenda kupata matibabu kuna matokeo mawili anaweza akapona au akapoteza maisha, na mimi naomba niseme kwamba hakuna maiti ambayo imezuiliwa moja kwa moja kutokana na kwamba mtu ameshindwa kutoa gharama za matibabu,"alisema.



Mkurugenzi wa mradi wa VectorWorks, Waziri Nyoni (kulia), akimkabidhi cheti maalum Msimamizi wa Kitengo cha Kudhibiti Malaria nchini, Winfred Mwafongo (kushoto), wakati wa hafla wa kumalizika mradi huo, mjini Bagamoyo mkoani Pwani jana, ambao umedumu kwa miaka mitano. VectorWorks imekuwa ikiendesha mradi wa kugawa vyandarua vyenye dawa ya muda mrefu hapa nchini chini ya ufadhili wa Shirika la Misaada la Marekani (USAID) kupitia Mfuko wa Rais wa Marekani wa kudhibiti malaria. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Bil.20/- zaleta mageuzi tiba Bugando

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

UBORESHAJI wa miradi ya huduma za afya katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando jijini Mwanza ulioanza mwaka 2015 hadi mwaka huu, umegharimu Sh. bilioni 20.

Taarifa hiyo ilitolewa juzi na Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali hiyo, Profesa Abelly Makubi, katika ziara ya maofisa habari kutoka sekta ya afya waliotembelea miradi hiyo kujionea mafanikio ya Bugando mpya yaliyotekelezwa hadi mwaka huu.

"Uboreshaji wa huduma ya afya Bugando tuliyotekeleza kwa mafanikio makubwa ni pamoja na uanzishwaji wa huduma za tiba ya saratani uliogharimu Sh. bilioni 5.5, mashine za mionzi Sh. bilioni 3.5, upanuzi wa vyumba vya upasuaji kutoka vitano hadi 13 na kununua vifaa vyake ni Sh. bilioni 2.5, kununua vifaa vya uchunguzi wa kibingwa na ununuzi wa CT Scan uliogharimu Sh. bilioni 1.7," alisema Prof. Makubi.

Aliitaja miradi mingine iliyotekelezwa ndani ya kipindi hicho ni ununuzi wa mashine za maabara ya kawaida uliogharimu Sh. milioni 500, ujenzi wa jengo la huduma za wagonjwa wa bima ya afya kwa gharama ya Sh. milioni 800.

Pia alisema gharama za mfumo mpya wa kielektroniki wa hospitali na kompyuta mpakato (laptop) vimegharimu Sh. milioni 300 na upanuzi na ujenzi wa idara ya wagonjwa mahututi na dharura umegharimu Sh. milioni 600 na huduma za mashine 20 za kusafisha figo.

Aidha mafanikio mengine ya miradi hiyo ni pamoja na ukarabati wa jengo kuu la hospitali Bugando uliogharimu Sh. milioni 169 na ukarabati na uboreshaji wa wodi za wagonjwa wa kawaida, wodi za wajawazito kwa Sh. milioni 75.

Pamoja na ukarabati huo mkubwa, alisema huduma za bima ya afya katika hospitali hiyo zimeongezeka wagonjwa 120 hadi 250 kwa siku.

Vile vile alisema wagonjwa wameongezeka kutoka 600 kwa siku mwaka 2017 hadi 1,500 kwa sasa huku mapato yakiongezeka kutoka Sh. milioni 800 kwa mwezi hadi Sh. bilioni 3.9 kwa sasa. Prof. Makubi alisema kutokana na kuboreshwa kwa ukarabati na huduma, Bugando imeokoa Sh. bilioni mbili kwa mwaka kwa wagonjwa ambao wangekwenda kutibiwa nje ya nchi.

Aidha, alisema hivi sasa hospitali imeajiri madaktari bingwa 13 kutoka Cuba ambao ni wabobezi katika maeneo ya upasuaji wa ubongo, njia ya mkojo na wagonjwa mahututi.

# Kairuki akaribisha wawekezaji wa China

**Na Enock Charles**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, amewakaribisha wafanyabiashara na wawekezaji kutoka China kuwekeza kwenye sekta za kilimo, mifugo ma uvuvi.

Pamoja na kuwakaribisha kuwekeza, Kairuki amewahakikishia kuwapatiwa mazingira mazuri na rafiki ya uwekezaji nchini.

Kairuki alisema hayo jana alipokuwa akizungumza jijini Dar es Salaam katika kongamano la uwekezaji na biashara lililojumuisha viongozi na zaidi ya kampuni 180 kutoka jimbo la Shandong nchini humo.

Waziri Kairuki alisema lengo la kuwaleta wawekezaji hao nchini ni kujionea fursa za kuwekeza kwenye sekta za kilimo, mifugo na uvuvi.

"Kilimo, mifugo na uvuvi ni sekta ambazo kwanza zinaajiri watu wengi sana, lakini pili tija yake inaonekana kirahisi na ni kubwa tuki ukiangalia katika mnyororo mzima wa thamani ni sekta ambazo zina mnyororo mkubwa na zinaajiri watu wengi," alisema Kairuki.

Alisema uwekezaji katika sekta hizo unahitaji mtaji mkubwa, hivyo kuifanya serikali kuhamasisha uwekezaji kutoka ndani na nje ya nchi ili kuunga mkono juhudi za Rais John Magufuli kuelekea Tanzania ya viwanda.

Naye Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Biashara katika jimbo la Shandong, Lyu Wei, alisema wawakilishi wa wakazi wa jimbo hilo lenye zaidi wakazi milioni 99 wamekuja Tanzania kuangalia fursa za uwekezaji kutoka na urafiki wa muda mrefu uliopo kati ya China na Tanzania.

"Tumekuja Tanzania kutokana na urafiki wa muda mrefu ulioasisiwa na waasisi wa mataifa yetu Mwalimu Julius Nyerere na Mwenyekiti Mao Tse Dong. Serikali na kampuni za kibiashara tumekuja hapa kwa ajili ya uwekezaji," alisema Wei.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, SACP Jonathan Shana (aliyevaa gloves nyeupe), akiwaonyesha vijana 13 kwa waandishi wa habari, jana, wanaotuhumiwa kuwa ni vinara wa uporaji maarufu kwa jina la 'Tatu Mzuka', waliokamatwa Septemba 4 mwaka huu, katika eneo la Sanawari, jijini humo wakati wa oparesheni maalum ya Jeshi hilo. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# Kiwango cha malaria chapungua nchini

**Na Mwandishi Wetu**

KIWANGO cha malaria nchini kimeshuka kwa asilimia 50 ikiwa ni kupungua kwa maambukizi ya vimelea vya ugonjwa huo kutoka asilimia 15 mwaka 2015 hadi asilimia 7.3 mwaka jana.

Hayo yalibainishwa jana na Mratibu wa Malaria kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Stella Kajange, wakati wa mkutano wa wadau wa malaria uliofanyika Bagamoyo mkoani Pwani.

Alisema kupungua kwa ugonjwa huo kumetokana na jitihada za serikali, wadau na wahisani na kwamba Tanzania inaendelea vizuri katika mapambano dhidi ya malaria, ugonjwa ambao umekuwa tishio kwa jamii.

"Licha ya kupungua kwa ugonjwa huu nchini lakini ugonjwa huu bado ni tishio kwa jamii, hivyo serikali inaendelea na utekelezaji wa afua mbalimbali ili kuhakikisha tatizo hilo linapungua," alisema Kajange.

Alisema sera ya mwaka 2007 inaelezea mwelekeo wa nchi katika kuhakikisha wananchi wanakuwa na afya njema ili waendelee na shughuli zao mbalimbali za uzalishaji na kujipatia kipato.

"Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo tunatekeleza sera mbalimbali kwa faida ya wananchi wetu kuhakikisha wanakuwa na afya njema. Tunalishukuru Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (Usaid) na wahisani wengine kwa misaada yao,"alisema.

Naye Msimamizi wa Mradi wa Taifa wa kudhibiti Malaria (NMCP), Winfred Mwafongo, alisema malaria inaathiri zaidi kundi la wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka mitano.

Alisema katika mikakati yao waliyojiwekea ni kuhakikisha wanadhibiti Malaria nchini ambapo tayari wameweka utaratibu wa afua ambazo zinahusika na udhibiti wa Malaria.

Alisema miongoni mwa afua hizo ni kuhakikisha kuna kuwapo na matumizi ya vyandarua vyenye dawa kuangamiza vijidudu na upuliziwaji wa viuadilifu kudhibiti mbu.

Kwa Upande wake, Mkurugenzi wa Mradi wa VectorWorks, Waziri Nyoni, alisema mradi huo umedumu nchini takribani miaka mitano ambao ulijikita usambazaji wa vyandarua vyenye dawa katika mikoa mbalimbali.

"Mradi umedumu nchini ndani ya miaka mitano na mwezi huu ndiyo mwisho wa mradi huu, tunaamini kwa ushirikiano tulioupata umeweza kuleta tija kwa jamii katika kuhakikisha wananchi wanatumia vyandarua vilivyowekwa dawa,"alisema.

Akizungumzia shughuli zilizotekelezwa na VectorWorks, alisema ni kujenga mifumo ya kuhakikisha utaratibu wa ugawaji wa vyandarua kwa walengwa kupitia vituo vya kutolea huduma nchi nzima kupitia shule za msingi katika mikoa 14.

"Uwajibikaji unaendelea bila changamoto yoyote, tumejenga uwezo wa bohari kuu ya dawa (MSD) kuendelea na utaratibu huu na pia watendaji ngazi za halmashauri wataendelea kusimamia utoaji wa huduma hizi hata bila uwapo wa VectorWorks ambayo ni mafanikio makubwa ya mradi,"alisema.

Aidha alisema mradi huo ulijikita katika maeneo matatu ikiwamo kushauri serikali juu ya sera zinazohusu masuala ya malaria, utekelezaji wa afua ya ugawaji wa vyandarua vyenye dawa, kufanya tafiti juu ya ugonjwa wa malaria na upimaji wa matokeo ya program za malaria.

Mradi wa VectorWorks umekuwa ukifadhiliwa na USAID kupitia mfuko wa Rais wa Marekani wa kudhibiti Malaria (PMI).

# Mbunge ashangaa mgawo wa kondomu mikesha ya Mwenge

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Mtambile (CUF), Masoud Abdallah Salim, ameelezea kushangazwa na kitendo cha serikali kugawa kondomu maboksi kwa maboksi katika mikesha ya Mwenge.

Kutokana na hali hiyo, ameshauri serikali iuweke Mwenge wa Uhuru kwenye jumba la makumbusho kama inaona kukimbizwa kwake kunachangia maambukizo ya virusi vya ukimwi (VVU) nchini.

Akiuliza swali la nyongeza jana bungeni, Mbunge huyo alisema serikali imezuia mikesha zikiwamo ngoma na mambo mengine ili kuondokana na maambukizo hayo.

"Kazi ambazo zinafanywa na mbio za mwenge zinaweza kufanywa na baadhi ya watendaji serikalini na tumeshuhudia uzinduzi mbalimbali wa miradi, kondomu zimekuwa zikigawiwa maboksi kwa maboksi katika mikesha ya mwenge.

"Je, hamuoni haja sasa ya Mwenge wa Uhuru ukawekwa kwenye makumbusho baada ya kutembea katika maeneo mengine?" alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia watu Wenye Ulemavu, Stella Ikupa, alisema si kweli kwamba mwenge unasababisha maambukizo hayo kupitia mikesha na kuwataka Watanzania kubadili tabia zao ili kuondokana na maambukizi hayo.

Alisema Mwenge wa Uhuru una mambo mengi na ni tochi ambayo inaangaza na yako mambo mengi yanayofanywa na mwenge wa uhuru katika maeneo mbalimbali.

"Utaendelea kuwa alama na utaendelea kukimbizwa kila mahali kwa sababu mwenge huo wa uhuru ambao faida zake ni kukagua miradi mbalimbali ambayo kama usingepita wasingekuwa wanaona wakandarasi wengi wana hofu,"alisema.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalum (CUF), Mgeni Jadi Kadika, alisema mwenge unaleta maendeleo lakini kuna changamoto kuwa mkesha mwenge unapolala unafanya kishawishi kikubwa na maambikizi makubwa mapya ya Ukimwi hivyo kusababisha vijana wengi kuathirika.

Alihoji ni kwa nini serikali haifanyi mfumo mwingine wa kulaza mwenge huu kwenye vituo vya polisi au ofisi za halmashauri ili kupunguza maambukizi kwa vijana.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kila na kheri Taifa Stars, tuwachape Burundi

**KWA** mara nyingine kikosi cha Timu ya Soka ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), kinatarajia kushuka dimbani kuwakabili wapinzani wao Burundi katika mechi ya kuwania tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Dunia zinazotarajiwa kufanyika Qatar mwaka 2022.

Mechi hiyo kati ya Stars dhidi ya Burundi, itachezwa kesho kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam baada ya Jumatano kutoka sare ya bao 1-1 mjini Bujumbura.

Ili kuwa kwenye nafasi nzuri ya kutinga hatua ya makundi ya mashindano hayo, Taifa Stars inayofundishwa na Etienne Ndayiragije, raia wa Burundi, inahitaji ushindi wa aina yoyote kwa sababu sare ya kuanzia magoli 2-2 itakuwa imewaondoka kwenye michuano hiyo.

Ni mechi ambazo zinachezwa ndani ya muda mfupi, lakini ni kalenda ambayo imetolewa na Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), ambayo inazihusu timu za mataifa yote.

Stars inatakiwa kujiandaa vema kuhakikisha inashinda mechi hiyo na kuondoa akilini mwao kwamba ina faida ya bao moja la ugenini ambalo walilipata katika mchezo wa kwanza.

Kama wao waliweza kupata goli hilo, wapinzani wao Burundi pia wanaweza kupata bao, kikubwa ni kujilinda na kutumia vizuri nafasi za kufunga watakazozitengeneza katika mchezo huo na hatimaye kuwapa furaha Watanzania.

Nipashe inaamini kuwa endapo wachezaji watakapopata nafasi ya kucheza mechi hiyo watajituma na kupeperusha vema bendera ya Tanzania, hakuna kitakachoshindikana.

Ni wazi kuwa dunia ya leo, mgeni anaweza kupata ushindi, kamwe jambo hili Watanzania tusilikubali, tushikamane, tutapambane kuona Stars inatinga hatua ya makundi na baadaye kutimiza ndoto za kucheza fainali za Kombe la Dunia kwa mara ya kwanza. Pamoja na Tanzania kutuchukua miaka 39 kurejea katika fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), hicho si kigezo cha kuchukua tena muda mrefu ili kukata tiketi ya kushiriki mashindano hayo makubwa, tunawaamini wachezaji wetu wanaweza kupambana na hatimaye kupata matokeo chanya katika mchezo huo ambao utachezwa kuanzia saa 10:00 jioni.

Kufanya vema kwa Stars, mbali na kutangaza jina la nchi katika ngazi ya kimataifa, pia kutatoa nafasi kwa wachezaji wa Tanzania kunadi vipaji vyao na hatimaye kupata idadi kubwa ya wachezaji wanaocheza soka la kulipwa.

Gazeti hili lina imani na kikosi cha Stars pamoja na benchi lake la ufundi, lakini ili waweze kukamilisha kazi yao, mchezaji namba 12 (shabiki) ambaye ni muhimu zaidi, naye anatakiwa kutimiza wajibu wake katika kuhakikisha taifa linaibuka na ushindi kwenye vita hii.

Hata hivyo, Nipashe linawakumbusha wachezaji wa Stars kucheza kwa tahadhari katika mechi hiyo ya marudiano, huku ikikumbuka Burundi ni moja ya timu zilizoonekana kuonyesha soka la kueleweka kwenye fainali za AFCON, licha ya kutolewa kwenye hatua ya makundi.

Mashabiki watakapofika kwa wingi uwanjani kwa lengo la kuwashangilia wachezaji wao kwa dakika zote 90, naamini kila mmoja ataona kuwa ana deni la kupambana kwa lengo la kupata matokeo chanya na si kitu kingine.


Nipashe linapenda pia kuwakumbusha mashambiki wa soka wa hapa nchini, kuwa watulivu kabla ya baada ya mchezo huo kumalizika na kuendeleza sifa yetu kuwa Tanzania si sehemu tulivu na ya amani, licha ya kuwapo kwa taarifa za kiongozi mmoja wa Stars na mwandishi wa habari (majina tunayahifadhi) kufanyiwa vurugu za hapa na pale kule mjini Bujumbura.

Kwa nguvu ile ile iliyotumika kuwaondoka Kenya (Harambee Stars) katika safari ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), itumike pia kuwafunga Burundi na hatimaye kusonga mbele.

Kila na kheri Taifa Stars, Mungu ibariki Tanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Ya Simba na KMC yasijitokeze kesho

**TIMU** ya soka ya Tanzania (Taifa Stars), kesho itakuwa nyumbani kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam kucheza dhidi ya wenzao kutoka Burundi katika mechi ya marudiano ya kusaka tiketi ya kucheza fainali za Kombe la Dunia mwaka 2022 nchini Qatar.

Kwenye mechi ya kwanza iliyocheza mjini Bujumbura nchini Burundi, Stars ililazimisha sare ya bao 1-1.

Ili kutinga katika hatua ya makundi, Taifa Stars inatakiwa kutoka sare isiyo na magoli, au ushindi wa idadi yoyote ile ya magoli.

Sare ya kuanzia magoli 2-2 na kuendelea au kufungwa idadi yoyote ya magoli itaitoa Stars kwenye kinyang'anyiro cha mashindano hayo.

Kinachonifanya niandike hili, ni wasiwasi wangu ambao ulianza kuniingia tangu kwenye mechi ya marudiano ya Kombe la Shirikisho Afrika kati ya KMC dhidi ya AS Kigali na mechi nyingine ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa kati ya Simba dhidi ya UD Songo.

Baada ya kutoka sare ya bila kufungana ugenini, KMC ilionekana ina nafasi kubwa ya kushinda mechi kwani inacheza ugenini, lakini kilichotokea hakuna aliyeamini, kwani ilichapwa hapa hapa mabao 2-0 na kutolewa kwenye michuano hiyo.

Simba nayo, baada ya sare ya bila kufungana ugenini, ilishangazwa nyumbani ilipolazimishwa sare ya bao 1-1 na kwa matokeo hayo, ikawa nje ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa bao la ugenini.

Matokeo haya yawe ni somo kuelekea kwenye mechi ya kesho kwa viongozi, makocha na wachezaji wetu wa Taifa Stars.

Hawatakiwi kubweteka kabisa kuona kama kazi imeisha kwani Burundi wanaweza kupindua matokeo kama zilivyofanya timu nilizozitaja.

**Wao watafunguka, watacheza mpira, hivyo uwanja utakuwa mpana, hapo sisi ndipo tutatumia mwanya huo, lakini pia tutasaka bao la mapema ili kuwapa presha wapinzani wetu.**

Ukiangalia kwa makini utagundua kuwa Simba na KMC zilitolewa kwa sababu za kisaikolojia zaidi kwani viongozi, makocha na wachezaji wao waliona kama vile wamemaliza kazi na kujiingiza kwenye raundi inayofuata kabla mechi za marudiano hazijachezwa.

Wachezaji wa Taifa Stars inapaswa wakumbushwe kuwa pamoja na sare ya bao 1-1, huku mkononi wakiwa na goli la ugenini, waondokane kabisa na fikra za mechi ile, iwe kama vile haijachezwa na wanachohitaji ni kupambana na kutoka na ushindi tu ili waweze kusonga mbele na si vinginevyo.

Kama akili za wachezaji zikiwa ni kutafuta sare ya bila kufungana kwa bahati mbaya Burundi ikapata bao la mapema, linaweza kabisa kuwachanganya wachezaji na mechi ikaishia hapo.

Nilimsikia Kocha Mkuu wa Burundi akisema kuwa hana wasiwasi na mechi hiyo kwani Stars itacheza kwa kufunguka, tofauti na ilivyocheza Burundi ambapo ilikuwa inazuia zaidi.

"Wao watafunguka, watacheza mpira, hivyo uwanja utakuwa mpana, hapo sisi ndipo tutatumia mwanya huo, lakini pia tutasaka bao la mapema ili kuwapa presha wapinzani wetu." Alisema kocha huyo.

Hiyo ndiyo mbinu watakayoingia nayo, hivyo Stars itabidi ijipange vizuri ili yenyewe ndiyo ianze kushambulia tangu mwanzo ili kupata bao la mapema na kutoruhusu Burundi kumiliki mpira dakika za mwanzo, kwani kitendo hicho kinaweza kusababisha kutimiza lengo lao na kuwatoa mchezoni wachezaji na mashabiki kwa ujumla.

Kila la kheri Taifa Stars, Mungu Ibariki Tanzania kuelekea Qatar mwaka 2022.

# Dawasa yatangaza neema ya maji

**Na Frank Monyo**

MWENYEKITI wa Bodi ya Dawasa, Jenerali (mstaafu) Davis Mwamunyange, amesema zaidi ya wakazi 120,000 wa Mlandizi, Chalinze na Mboga wanatarajiwa kuondokana na adha ya maji ifikapo Februari, mwakani, baada ya kukamilka kwa mradi mkubwa katika eneo hilo.

Akizungumza juzi wakati wa ziara ya kukagua maendeleo ya mradi huo wa maji Mlandizi-Chalinze Mboga, alisema kukamilika kwa mradi huo kutasaidia kuondoa kero ya muda mrefu kwa wakazi wa maeneo hayo waliokuwa wakihangaika kupata maji safi na salama.

"Mradi huu wa maji wa Mlandizi-Chalinze -Mboga wenye urefu wa kilomita 59 utakapokamilika, utahudumia wananchi 120,000 na maji yatakayosafirishwa ni kiasi cha lita milioni tisa kwa siku," alisema.

Alisema katika kufikia lengo la kukamilika mradi huo, pia kutasaidia kuondoa kero ya maji kwa wananchi wa maeneo yote yaliyo pembezoni mwa bomba katika maeneo yote bomba litakapopita kuanzia Chalinze, Mlandizi na mji mdogo wa Mboga pamoja na maeneo mengine ya karibu.

Mwamunyange alisema ili kufikisha maji katika maeneo husika, vituo vidogo viwili vya kusukuma maji vitajengwa katika vijiji vya Chamakweza na Msoga.

# Viongozi Afrika wamlilia Mugabe

INATOKA UK.3

Naye Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta, alituma salamu za rambirambi akisema hana maneno ya kutosha kuelezea uzito wa kuachwa na kiongozi shupavu, shujaa na mzalendo wa Afrika ambaye alitekeleza jukumu muhimu katika kutetea maslahi ya bara la Afrika

Rais Kenyatta, kutokana na kifo hicho, ameamuru bendera zote nchini humo kupepea nusu mlingoti kuanzia leo hadi Jumatatu kumpa heshima mwana mapinduzi huyo wa Zimbabwe.

Kwa upande wake, Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa alimtaja rais huyo wa zamani wa Zimbabwe kuwa "bingwa dhidi ya ukoloni."

**MUGABE NI NANI**

Alizaliwa Februari 21, 1924 katika Kijiji cha Shona Kutama Mission wilaya ya Zvimba Kusini mwa Rhodesia.

Baba yake, Gabriel Mitibiri, alikuwa seremala wakati mama yake, Bona, alifundisha Katekisimu kwa watoto wa kijiji.

Baada ya kumaliza miaka sita ya masomo ya msingi, mwaka 1941 Mugabe alipewa nafasi kwenye mafunzo ya ualimu katika Chuo cha Kutama.

# Waziri abainisha kikwazo dhidi udhibiti mazingira

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, George Simbachawene, amesema uharibifu wa mazingira nchini unachangiwa na utekelezaji wa sheria ya mazingira ya mwaka 2004 kuwa chini ya asilimia 30.

Kauli hiyo aliitoa jana jijini hapa alipokuwa akifungua mkutano wa wadau wa mabadiliko ya tabia nchi uliolenga kupokea taarifa ya utekelezaji wa miradi ya Eco Village Project inayofadhiliwa na Jumuiya ya Umoja wa Ulaya (EU) ambayo inalenga kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Alisema amejaribu kufanya tathmini isiyo rasmi na kubaini kuwa sheria imeachwa na ndio maana kuna uharibifu wa mazingira.

Alibainisha kuwa kutokana na hali hiyo, EU imeanzisha programu za kubadilisha jamii kuishi maisha ya tofauti kama anafanya kazi inayochangia kuharibu mazingira, anafundishwa njia ya kuishi tofauti na yale aliyokuwa akiyafanya.

Alisema Serikali imeandaa programu mbalimbali kwa ajili ya kusaidia utunzaji wa mazingira, unaosababishwa na upungufu mkubwa uliopo wa utekelezaji wa sheria hiyo.

"Haya maeneo ambayo mradi umetekelezwa yanatakiwa kuwa mfano ili elimu hiyo ifikishwe kwenye vijiji vingine," alisema.

Awali, Mkuu wa Kitengo cha Rasilimali Asili kutoka EU, Jenny Correia Nunes, alisema EU itaendelea kufanya kazi na Tanzania kuisaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi kama walivyokubaliana katika mkutano uliofanyika Paris.

Alisema mpango kazi wa kifedha wa miaka saba ijayo EU imejizatiti kuelekeza asilimia 28 ya bajeti yake kwenye suala la mabadiliko ya tabia nchi.

"Kiwango hiki ni kikubwa na tunatarajia wengine watafuata na tuhakikishe zinaleta matokeo chanya, leo tumekutana kujifunza jinsi ya kufanikisha haya chini ya programu ya GCCA+ ili kujua athari za mabadiliko ya tabia nchi Tanzania," alisema.

Simbachawene alifafanua kuwa programu hiyo imefadhiliwa na EU na imeanza miaka 10 iliyopita na imelenga hasa maeneo ya vijijini kuondokana na athari hizo na miradi 8 kupitia mradi wa Eco Village imefadhiliwa Sh. Bilioni 25.428.

Naye, Meneja Mradi anayehusika na miradi ya mabadiliko ya tabia nchi na utunzaji wa mazingira EU, Mathew Mpanda, alisema umoja huo unatekeleza miradi hiyo inatekelezwa katika Mikoa ya Dodoma, Tabora, Tanga, Arusha pamoja na Pemba.

Alisema wananchi wanafundishwa mbinu hizo katika sekta ya kilimo, ufugaji pamoja na kuboresha mazingira wanayoishi ili kutunza mazingira.



Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro (wa tatu kulia), kwa kushirikiana na Taasisi ya walemavu wa Uti wa Mgongo ya KASI, akikabidhi misaada ya vitu mbalimbali ikiwamo mtaji wa maji ya jumla, rangi za nyumba, hotpot na vyakula kwa walemavu wenye matatizo ya uti wa mgongo walioko katika Wilaya ya Arumeru, mkoani Arusha juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# TBS yaonya vifaa ubora hafifu

**Na Joseph Mwendapole**

WATAALAM wa ujenzi nchini wametakiwa kuhakikisha vifaa wanavyotumia kwenye shughuli vinakidhi viwango ili miradi wanayotekeleza ilingane na thamani za fedha wanazotumia na iwe imara.

Ofisa Udhibiti Ubora wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Isack James, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari katika maonyesho yaliyoandaliwa na mkutano wa pamoja wa mashauriano wa Bodi za Usajili Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB), Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) na Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB).

Alisema wataalamu wa ujenzi wana mchango mkubwa kwenye suala zima la kusimamia viwango, hivyo shirika hilo limeshiriki mkutano huo kwa ajili ya kuwakumbusha wajibu wao katika kutumia vifaa vilivyothibitishwa ubora.

James alisema ni muhimu wataalamu hao katika shughuli zao za ujenzi wakatumia bidhaa zenye viwango zikiwamo nondo, saruji, mabati vyuma, vigae na vinginevyo.

Aliongeza kwamba ni jukumu la TBS kuwakumbusha wadau hao kutumia vifaa vyenye viwango mara kwa mara bila kuhitaji kusimamiwa.

"Wasipotumia bidhaa ambazo hazina viwango miradi wanayotekeleza haitakuwa na ubora unaotakiwa," alionya James na kuongeza kwamba madhara mengine ya kutumia vifaa ambavyo havina viwango ni miradi wanayojenga kutokuwa na thamani inayolingana na fedha zinazotumika.

Alisema kwa kutambua umuhimu wa viwango ndiyo maana maofisa wa shirika hilo wamekuwa wakifanya ukaguzi wa kushtukiza kwenye masoko na kuchukua sampuli ili kuzipima kuthibitisha kama zina ubora unaotakiwa bila mzalishaji kuwa na taarifa.

Pia aliwataka wataalam hao wanapokuwa na mashaka na vifaa wanavyotaka kutumia kwenye shughuli zao za ujenzi kuwasiliana na shirika hilo ili wapatiwe ushauri wa kitaalamu.

Kwa upande wa wazalishaji na waagizaji wa vifaa vya ujenzi, James aliwahimiza kuzingatia matakwa ya viwango wakati wote ili kulinda mitaji yao, kwani vinginevyo watakutana na mkono wa sheria.

# Magari 300 yakwama bandarini Dar

**Juster Prudence,** TUDARCO

ZAIDI ya magari 300 ya kusafirisha mizigo kutoka nchini kwenda nchi mbalimbali yamekwama kwenye foleni kwa siku nne katika Bandari ya Dar es Salaam.

Sababu za kukwamba kwa foleni hiyo zimetajwa kuwa ni mizani na mtandao wa kutoa vibali unaofanyakazi taratibu.

Kutokana na foleni hiyo inayofika hadi Uwanja wa Taifa madereva wamelazimika kusubiri kwa zaidi ya saa 24.

Nipashe ilifika eneo la bandari na kushuhudia changamoto hiyo iliyoanza Septemba 3, mwaka huu, huku msongamano ukianzia geti namba tano .

Baadhi ya madereva walilieza gazeti hili kuwa tangu wabadilishiwe mzani, matatizo ya foleni yamekuwa makubwa kwa sababu wanalazimika kuhakiki magari yao kabla ya kuingia bandarini, hivyo kutumia muda mrefu zaidi ukilinganisha na ilivyokuwa siku za nyuma.

Mmoja wa dereva huyo, Haji Yunga, alisema moja ya sababu za kuwapo kwa msongamano huo ni mazingira ya rushwa ili kuruhusu madereva kupakia mizigo kutoka bandarini hapo.

Dereva Mohamed Kombo alisema amekuwa kwenye foleni kwa siku nzima na kuongeza kuwa tatizo hilo linasababishwa na mtandao mbovu unaotumika bandarini kwa ajili ya kutoa vibali kwa madereva.

"Nipo hapa tangu juzi saa 5:00 usiku mpaka leo (jana) sasa ni saa 6:00 mchana nipo hapa kwenye foleni. Nilikuwa na safari ya kwenda Congo, kwa ufupi mtandao wa kutolea vibali ni mbovu," Kombo alilalamika.

Kutokana na tatizo hilo, baadhi ya madereva waliiomba serikali kushughulikia kwa haraka jambo hilo ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa bandari.

Madereva hao walitoa mapendekezo ya kukaguliwa mara moja wakishauri kusiwe na ukaguzi mwingine wanapoendelea na safari kama inavyofanyika sasa.

Foleni hiyo imeonekana pia kuwa tatizo kwa wakazi wa maeneo hayo kwa sababu wengine wameshindwa kufika katika maeneo ya kazi kwa muda uliopangwa, huku wengine wakishindwa kufanya biashara zao kama ilivyokuwa mwanzo.

Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) kupitia Meneja Mawasiliano, Leonard Magomba, walipoulizwa kuhusu suala hilo, walisema waulizwe Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads) kwa kuwa ndio wahusika.

TRA ilitafutwa ambapo Mkurugenzi wa Mawasiliano kwa Umma na Elimu kwa Mlipakodi, Richard Kayobo, hakupokea simu yake ya mkononi.

Foleni kama hiyo iliwahi kutokea mapema Julai 3, mwaka huu na Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, alitaja sababu ni baadhi ya taasisi zinazofanya kazi na TPA ambazo hazijaanza kufanya kazi kwa saa 24 kama ilivyoelezwa.

Tangu Septemba 18, 2017 serikali ilipitisha sheria ya kuzitaka taasisi zote za umma, kufanya kazi kwa saa 24, lakini Waziri huyo alisema katika bandari hiyo, zipo ambazo hazijatii agizo hilo hali ambayo inasababisha kuchelewa kutoka kwa mizigo.

Kamwelwe akiwa katika mkutano wake na wachimbaji wakubwa wa madini duniani na wafanyabiashara waliokutana kwa lengo la kujadili changamoto zinazokwamisha kupitisha mizigo yao katika bandari hiyo, alisema sababu nyingine ni hujuma zilizokuwa zinafanywa na wamiliki wa malori.

Alizitaja baadhi ya mamlaka zinazotakiwa kufanya kazi kwa saa 24 katika bandari hiyo kuwa ni Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Wakala wa Barabara (Tanroads lakini hazifanyi hivyo jambo linalochochea foleni.



Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda Bugando, Prof. Abel Makubi (wa pili kulia), akizungumza na wakuu wa idara ya mawasiliano na maofisa mawasiliano kutoka taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, walipofanya ziara katika hospitali hiyo, jijini Mwanza jana. Kulia ni Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Bugando, Lucy Mogele. **PICHA: ELIZABETH FAUSTINE**

# Hali majeruhi wa moto zaimarika

**Na Mary Geofrey**

HALI za majeruhi saba kati ya 11 wa ajali ya moto waliolazwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MHN), zinaendelea kuimarika.

Wanne kati yao wako katika chumba cha uangalizi maalum (ICU), wakiendelea kupatiwa matibabu kwa ukaribu zaidi. Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Umma MNH, Sophia Mtakasimba, akizungumza na Nipashe jana kwa njia ya simu, alisema majeruhi hao saba wanaendelea kufanya mazoezi.

"Majeruhi mmoja aliyekuwa amelazwa ICU ametolewa leo (jana) na kupelekwa katika wodi za kawaida baada ya afya yake kuimarika kwa ajili ya kuendelea na mazoezi ya viungo," Mtakasimba alisema.

Alisema madaktari wanaendelea na jitihada za kuhakikisha majeruhi hao hasa wanne waliopo ICU wanapona na kurejea katika shughuli zao za kila siku.

Idadi ya watu waliopoteza maisha kutokana na ajali ya lori la mafuta iliyotokea mkoani Morogoro Agosti 10, mwaka huu, imefika 104.

Kati ya majeruhi 47 walifikishwa hospitalini hapo kuanzia Agosti 11 mwaka huu 36 wamefariki dunia na kubakia 11.

Idadi hiyo ya waliopoteza maisha inatokana na ajali ya lori lililokuwa limebeba tangi la mafuta ya petroli, kuanguka eneo la Msamvu mkoani Morogoro na baadaye kulipuka wakati baadhi ya wananchi wakichota mafuta yaliyokuwa yanamwagika.

# Mahakama yataifisha dhahabu kilo 35.34

**Na Rose Jacob,** MWANZA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mwanza imetaifisha kilo 35.34 za dhahabu yenye thamani ya Sh. bilioni mbili na kuwatia hatiani washitakiwa wawili kwa makosa matatu.

Makosa hayo ni kuongoza genge la uhalifu, kusafirisha madini kinyume cha sheria na utakatishaji fedha.

Hukumu hiyo imetolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi Rodha Ngimilanga, baada ya kusikiliza kesi hiyo ya uhujumu uchumi dhidi ya Charles Warioba na Warioba Marwa ambao ni mtu na mdogo wake wanaomiliki kampuni ya Nyamaswa Investment ya jijini Mwanza.

Watuhumiwa hao walihukumiwa kwa makosa hayo baada ya kukiri, hivyo kila mmoja kutakiwa kulipa Sh. milioni tano au kifungo cha miaka mitano kwa kosa la kwanza na kosa la pili Sh. milioni 10 au kifungo cha miaka 10. Kosa la tatu walihukumiwa kulipa Sh. milioni 100 kwa kila mmoja au kifungo cha miaka 15 kwa kila mmoja.

Pamoja na ndugu hao kuhukumiwa adhabu hiyo, washtakiwa wengine 10 waliachiwa huru baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Biswalo Mganga, kuwafutia mashtaka.

Wengine wawili aliwachia kipindi Rais John Magufuli alipofika katika Gereza la Butimba baada ya kujiridhisha kuwa hawakuhusika. Charles na Mwita walirudishwa Butimba hadi hapo watakapolipa fani au la.

Upande wa mashitaka katika kesi hiyo uliongozwa na mawakili wanne Shadrack Kimaro, Jacqueline Nyantori, Georgina Kinabo na Castus Ndamugoba huku wakili wa upande wa utetezi wakiwa Mwaya Mabela, akete Masato na Wilbart Kilomi. Mawakili wa pande zote hizo walidai kuwa wameridhishwa na hukumu hiyo.

Februari 15, mwaka jana, Baraka Chaulo alikamatwa na maofisa wa Mamlaka ya Mapato Kenya baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jomo Kenyata akiwa na kilo 35.34 za dhahabu akizisafirisha kwenda Dubai.

# Watakiwa kuachamapanga ili kutumia mashine

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

WAKULIMA na wafugaji mijini na vijijini wamekumbushwa kutumia mashine za kuchakata vyakula vya mifugo na kuachana na usumbufu wa kukatakata vyakula hivyo kwa mapanga.

Mtaalamu wa Mifugo katika Halmashauri ya Wilaya ya Babati mkoani Manyara, Lilian Lyimo, ndiye aliyetoa ushauri huo kwa wafugaji wa kuku na ng'ombe

Aliwashauri wakati akizungumza na wakulima na wafugaji wa Kijiji cha Endasaki kilichopo wilayani Hanan'g mkoani humo.

Aidha, aliwaonyesha mashine hiyo, ya kuchakata vyakula vya mifugo ili wafugaji hao waweze kufuga kwa kutumia njia za kisasa zaidi.

Alisema siku hiyo, iliandaliwa na shirika la Farm Afrika, kwa lengo la wadau wa kilimo na mifugo kuonyeshwa zana mbalimbali kilimo na namna zinavyotumika.

Lyimo, alisema mashine hizo, ni nzuri kwani zinarahisisha kazi kwa kukatakata mabua ya mahindi na vitu vingine kama majani kwa muda mfupi tofauti na wafugaji wanavyokata mabua kwa kutumia panga kwa muda mrefu.

Alisema mashine hizo, zikitumiwa ipasavyo zitawasaidia kuokoa muda na gharama za kununua chakula hasa cha kuku ambacho gharama yake ipo juu sana.

Aidha aliwataka wafugaji wa kuku kuichangamkia mashine hiyo, kwani itawasaidia sana kwa sababu mashine hiyo ina uwezo wa kusaga nafaka kwa ajili ya kulishia mifugo.

Mtaalamu huyo, alisema wapo wafugaji wa kuku ambao wakiona kuku wakila mayai au wakidonoana, lakini wafugaji wengi wamekuwa wakiona ni jambo la kawaida.

Aliwaambia kuwa kitendo cha kuku kula mayai au kudonoana kinasababishwa na upungufu wa madini fulani hivyo, njia ya kutibu tatizo hilo ni kununua damu ya mbuzi au ng'ombe kwenye machinjio iliyopimwa na daktari halafu ikaushwe na kuchanganywa katika vyakula vya mifugo hiyo na kuwapatia.

Aliwashauri kununua damu ya ng'ombe au mbuzi kutoka machinjioni ambayo mnyama aliyechinjwa amekaguliwa na daktari wa mifugo ili waende waikaushe na kuwapatia kuku wao wataacha kula mayai au kudonoana. Alisema wafugaji watakaohitaji washine hiyo, gharama yake haizidi kiasi cha Sh. mil.1.2 na wataepuka kununua chakula cha kuku kwa gharama kubwa.

Aidha aliwataka wafugaji na wakulima kuwatumia wataalamu kupata ushauri ili wafuge na kulima kilimo chenye tija na wakifanya hivyo watafaidi matunda ya kazi zao kwa haraka.

# Wawili wanaswa kwa tuhuma kupokea rushwa ya 20,000/-

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

MWENYEKITI wa Baraza la Ardhi Kata ya Bwawani wilayani Kiteto mkoani Manyara, Steven Tollya na Katibu wake Maiko Lemabi, wanashikiliwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), kwa madai ya kuomba na kupokea rushwa ya Sh.20,000.

Rushwa hiyo iliombwa kutoka kwa mwanakijiji wa Bwawani aliyekuwa na shida ya kufunguliwa shauri la madai ya ardhi. Mkuu wa Takukuru wa Mkoa wa Manyara, Fidelis Kalungura aliyasema hayo jana, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kukamatwa kwa viongozi hao wawili.

Kalungura alisema viongozi hao walikamatwa kwenye kijiji hicho kwa nyakati tofauti, baada ya kuomba rushwa kwa mwananchi mmoja ambaye jina lake limehifadhiwa.

**Watuhumiwa hao wanatarajiwa kufikishwa mahakamani wakati wowote taratibu za kisheria zitakapokamilika.**

Alisema watuhumiwa hao walimuagiza mwananchi huyo awape kiasi hicho fedha, Julai 22 mwaka huu baada ya kuwaeleza kuwa anataka kufungua shauri la ardhi, kwenye baraza la ardhi la Kata ya Bwawani.

Alisema watuhumiwa hao walimuomba mwananchi huyo Sh.10,000 ya ziada wakati gharama halisi ya kufungua shauri na Sh.20,000.

"Baada ya kuambiwa hivyo Julai 24 mwaka huu, mwananchi huyo alifika ofisi za Takukuru na kutoa taarifa ya kuombwa rushwa na watuhumiwa hao wawili ambao ni viongozi wa baraza la ardhi la kata hiyo," alisema Kalungura.

Alisema baada ya kutoa taarifa hiyo waliandaa mtego kwa kuwatumia fedha hizo kwa njia ya Airtel Money ndipo wakamfungulia mwananchi huyo shauri hilo.

Alisema baada ya kufungua shauri hilo waliwakamata kwa nyakati tofauti na kuhojiwa kwenye ofisi za Takukuru.

"Watuhumiwa hao wanatarajiwa kufikishwa mahakamani wakati wowote taratibu za kisheria zitakapokamilika," alisema.

Alitoa wito kwa viongozi wa umma na wananchi wote kujiepushe na vitendo vya rushwa na kufanya kazi kwa kuzingatia taratibu, kanuni na maadili ya kazi zao vinginevyo watakumbana na mkono wa sheria.



Mkuu wa Wilaya ya Mbulu mkoani Manyara, Chelestino Mofuga, akizungumza na wananchi wa Kata ya Imboru jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mtaala wa elimu ufundi wakosolewa

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

MDAU wa elimu mkoani Arusha ameuelezea mtaala wa elimu ya ufundi stadi kuwa ni wa zamani na unawapa changamoto kubwa walimu wanaofundisha shule hiyo.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi wa Shule ya Msingi ya Healsun, ambaye pia ni Mkurugenzi Mkuu Wa Taasisi ya Elimu ya Sinoni, Edward Laizer, wakati akisoma hutuba yake katika mahafali ya nne ya kidato cha saba ya shule hiyo.

Alisema mtaala wa elimu ya ufundi stadi haujaboreshwa tangu ulipotungwa mwaka 1984 hivyo, unawapa tabu ya kupata vitendea kazi ikiwamo vitabu vya kufundishia masomo mbalimbali .


"Tunapata taabu sana kupata vitabu pamoja na vitendea kazi vingine kwa sababu mtaala huu haujarekebishwa tangu mwaka 1984 hivyo, tunaiomba serikali kupitia mtaala huu na kuubadilisha ili tuweze kufundisha watoto kulingana na mtaala unaoenda na wakati huu ili tuweze kufikia sera hii ya viwanda, " alisema Laizer.

Alisema kama taaluma ya ufundi itapewa kipaumbele itasaidia kupunguza tatizo la ajira nchini, kwani wanafunzi wengi wanao maliza shule za ufundi watakuwa na ujuzi wa kutosha wa vitendo.

Hata hivyo, alisema ujuzi wanaoupata shule utawasaidia kujiajiri au kuajiriwa badala ya kutegemea kuajiriwa serikalini.

Mgeni rasmi katika mahafali hayo, Mwenyekiti wa Umoja wa Wazazi Mkoa wa Arusha, Daudi Hezron Mbise, aliwatala wanafunzi hao kuzingatia na kufuata mambo mazuri waliofundishwa na walimu wao , huku akiwasihi kuzingatia sana elimu kwa kuendelea kusoma kwani kwa dunia ya sasa elimu ndio kila kitu.

"Najua mmefundishwa vyema na walimu wenu sasa kazi kwenu kuzingatia yote mliofundishwa darasani na hata nje ya darasani, pia napenda kuwasisitiza wazazi kufuatilia maendeleo ya watoto wao mashuleni na sio kuwaachia walimu kwani ukifuatilia maendeleo ya mtoto kama yupo chini utajua jinsi ya kumkazania mtoto wako.



# Mwekezaji atamani kuweka Tanzania

**Na Godfrey Mushi,** SAME

RAIS wa Taasisi ya Kimataifa ya Foundazione Same ya nchini Italia ambayo inamiliki asilimia 100 ya hisa za uwekezaji wa kiwanda cha utengenezaji wa matrekta, Fransisco Carozza, amesema anatamani kuja kuwekeza nchini Tanzania akiombwa kufanya hivyo.

Pia ameeleza kuridhishwa kwake na sera nzuri ya uwekezaji akisema Tanzania ni sehemu nzuri ya uwekezaji kutokana na kuwa na soko la uhakika, nguvu kazi na bandari lakini kubwa zaidi ni sera mbalimbali zimefanyiwa kazi.

Carozza alikuwa akizungumza jana katika Wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro, alipokwenda kukabidhi kwa Mkuu wa Wilaya hiyo, Rosemary Senyamule, mabweni mawili, madarasa, baiskeli 40 na trekta moja kwa ajili ya Chuo cha Ufundi cha St. Joseph kinachomilikiwa na Kanisa Katoliki.

**Nimefurahi kuelezwa kwamba serikali imeshaondoa kodi na tozo mbalimbali zilizokuwa kero kwa wawekezaji, hivyo kuongeza mazingira bora kwa wawekezaji nchini Tanzania.**

"Nia yangu ni kuendelea kushirikiana na Kanisa Katoliki, Jimbo la Same na serikali ya Tanzania katika kufikia malengo ya kuelekea katika uchumi wa viwanda, lakini nitafanya hivyo kadiri nitakavyoshirikishwa.

"Nimefurahi kuelezwa kwamba serikali imeshaondoa kodi na tozo mbalimbali zilizokuwa kero kwa wawekezaji, hivyo kuongeza mazingira bora kwa wawekezaji nchini Tanzania," alisema.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Senyamule, akizungumza baada ya kupokea msaada huo, alimshukuru Rais wa taasisi hiyo 'Foundazione Same' kwa kushiriki dira ya serikali ya kufikia uchumi wa kati wa viwanda ifikapo mwaka 2025, kwa kuwa kuwekeza katika uzalishaji wa rasilimali watu wenye ujuzi mahiri wa viwanda na ufundi, ndio nguzo maalum ya kufikia ndoto hizo.

"Kwa dhati kabisa ya moyo wangu, nimependezwa na ujio wa Rais huyu wa taasisi ya Foundazione Same, kwani hawa ni marafiki wazuri walioitumia vizuri jina letu, nimemuomba aje awekeze katika wilaya hii na amesema yuko tayari," alisema Mkuu huyo wa Wilaya

Awali, Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Same, Rogarth Kimario, alisema mchango huo ni mkubwa kwa wilaya na kanisa hilo katika kukuza sekta ya elimu na kuandaa rasilimali watu wenye ujuzi wa viwandani.

Kwa miaka mingi sekta ya viwanda imekuwa haifanyi vizuri na Tanzania imeendelea kutegemea kilimo chenye tija ndogo na sekta ya kuzalisha malighafi na bidhaa zenye thamani ndogo.

Matokeo yake, mchango wa viwanda katika pato la taifa umebaki vilevile kwa muda mrefu. Pia, uchumi umekuwa ukikua kwa asilimia saba kwa miaka 15 iliyopita. Ukuaji huo ni chini ya kiwango kilichokadiriwa cha kati ya asilimia nane na 10, kinachohitajika kupunguza na hatimaye kuondoa umaskini.




Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kaskazini, Aikansia Muro (wa pili kushoto), akikabidhi cheti kwa Mkuu wa Shule ya Sekondari Usangi, Delfina Msoffe Kombe, kama hongera kwa kuibuka nafasi ya pili katika Mkoa wa Kilimanjaro kwenye mitihani ya kidato cha sita 2019, katika hafla fupi ya Siku ya Walimu, iliyoratibiwa na benki hiyo, mkoani humo juzi. Katikati ni Msaidizi wa Ofisa Elimu wa mkoa huo, Fulgence Mponzi na Meneja Mwandamizi Wateja binafsi wa benki hiyo, Ally Ngingite. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Wakili awapa mchongo vijana

**Na Paul William,** MOSHI

WAKILI Zacharia Katikilo ambaye ni Mkufunzi Msaidizi wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Kumbukumbu ya Askofu Stephano Moshi (SMMUCo), amewataka vijana wanaohaha kutafuta ajira serikalini, kuelekeza zaidi ndoto zao katika kutafuta mbinu za kujiajiri.

Ukosefu wa ajira unaoneka kuwa janga kubwa kwa vijana na changamoto hiyo inachukuliwa kama kitu kinachoweza kukwamisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya nchi hasa wakati huu ambao taifa linajielekeza kwenda katika uchumi wa kati wa viwanda.

Alitoa ushauri huo jana mjini Moshi, akitaka vijana wa Kitanzania kuachana na ndoto za kutafuta ajira serikalini tu, badala yake kubuni mbinu za kujiajiri zitakazowasaidia kujikwamua na tatizo la ajira.

"Sasa hivi Tanzania ndiyo injini inayoongoza Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC). Tumieni fursa hiyo kutafuta maeneo ya kufanyia kazi ikiwamo ujasiriamali. Vijana mkiwa tayari kuzitumia vyema fursa hizo, tatizo la ajira litaondoka nchini na litaiondolea serikali mzigo wa utegemezi," alisema Katikilo

Katikilo ambaye pia ni Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), alisema tatizo la ajira linazidi kuongezeka kutokana na kutokuwapo na uwiano kati ya ugavi na mahitaji kwenye soko la ajira, hivyo uongezekaji wa ajira mijini unaobakiza ajira kwa sekta isiyo ya kilimo.

Kutokana na hali hiyo, alishauri kuanzishwa kila mkoa programu ya 'ready to work' itakayotoa elimu ya ujuzi inayoweza kuwaandaa vijana kujiajiri kwa kuwa itatoa muongozo kwa vijana kwa upande wa mafunzo na maendeleo wanayohitaji kwa ajili ya kukuza malengo yao kwenye ajira za serikali au ajira binafsi.

Taarifa zinaonyesha kuwa vijana wenye umri wa kuanzia miaka 15 hadi 34 ambao hawana ajira ni asilimia 13.4 wasichana wakiwa asilimia 7.2 na wavulana asilimia 6.3.

Katikilo alisisitiza kuwa maendeleo ya taifa hayawezi kuletwa na mtu mmoja na badala yake akawataka wananchi kuungana na kushikamana kuhakikisha taifa linapiga hatua kimaendeleo.

# Ataka wakusanya taka warejeshwe

**Na Godfrey Mushi,** HAI

SERIKALI wilayani Hai, imeagiza kurejeshwa kazini kwa Kikundi cha Mbalamwezi kilichokuwa kikikusanya takataka katika mji mdogo wa Bomang'ombe na viunga vyake, baada ya baadhi ya wananchi kulalamikia tatizo la watu kutupa taka ovyo barabarani.

Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza na vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM).

"Nimeambiwa kwamba kuna kikundi cha Mbalamwezi kilikuwa kikifanya kazi ya kukusanya takataka katika mji wa Bomang'ombe kilisimamishwa na mji unaendelea kuwa mchafu. Namwagiza DED (Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya), kikundi hicho kirejeshewe kazi hiyo kwa sababu kipindi walichokuwa wanafanya kazi hiyo waliifanya kwa ufanisi mkubwa,"alisema Ole Sabaya

Maeneo yanayolalamikiwa kukithiri kwa uchafu ni pamoja na mtaa wa Gezaulole ambako baadhi ya wananchi wamekuwa wakieleza kutoridhishwa kwao na kadhia ya utupaji wa takataka barabarani inayoendelea nyakati za usiku.


Kutokana na hali hiyo, baadhi yao wamekuwa wakiiomba Halmashauri ya Wilaya ya Hai pamoja na maofisa afya, kuanza ukaguzi wa kushtukiza na watakaobainika kutokuwa na mashimo ya kuhifadhi taka wawajibishwe.

Aikael Lema, mkazi wa Gezaulole, alisema adha ya takataka kutupwa na watu wasiojulikana nyakati za usiku katika barabara za mtaa huo na karibu na makazi ya watu sio jambo jema linalotakiwa kufumbiwa macho, kwa kuwa linahatarisha afya na usalama wa watu.

Naye Boniface Lyatuu, mkazi wa Gezaulole alisema: "Halmashauri yetu ni vizuri ikaja na sheria ndogo za udhibiti wa usafi wa mazingira. Madiwani ndio wanaotaka halmashauri yao iweje, hivyo ndivyo ninavyofahamu. Mnaweza mkawa na mipango mizuri lakini madiwani wakisema hapana, inakuwa ndivyo, usafi kwa Bomang'ombe ni changamoto."

Sheria Namba 20 ya mwaka 2004 ya Usimamizi wa Mazingira, inaweka masharti ya muundo wa kisheria na kiasasi juu ya usimamizi endelevu wa mazingira, kuweka misingi ya usimamizi, tathmini na kuchukua hadhari kuhusu madhara kwa mazingira.

Pia inatoa kinga na udhibiti wa uchafuzi wa mazingira, usimamizi wa taka, ubora wa viwango vya mazingira, ushirikishwaji umma na utekelezaji sheria.





# Jafo aomba viongozi wa dini kuliombea taifa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amewataka viongozi wa dini nchini kuendelea kuliombea taifa hasa wakati huu ambao miradi mikubwa ya maendeleo inatekelezwa.

Waziri Jafo aliyasema hayo wakati akifunga mkutano wa 82 wa Chama cha Madaktari wa Kikristo Tanzania unaofanyika chini ya Taasisi ya Huduma ya Kijamii za Kikristo (CSSC), katika ukumbi wa St. Gasper, jijini Dodoma.

"Serikali ya awamu ya tano inatekeleza miradi mikubwa ambayo haijawahi kutokea tangu Uhuru, kila unapopita unaona ujenzi wa miundombinu ya barabara inaendelea, halikadhalika ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), huku mradi wa ufuaji umeme wa Mto Rufiji unatekelezwa hatuna budi kuendelea kumuombea rais wetu Dk. John Magufuli azidi kuwa na afya njema na aweze kusimamia miradi hii hadi ukamilifu wake," alisema Jafo.

"Tunashukuru Mungu Mahakamu Kuu ya Gauteng, Africa Kusini imetoa hukumu na kuamuru ndege yetu ya Air Tanzania iliyokuwa inashikiliwa nchini humo iachiwe na mlalamikaji alipe gharama za kesi hizi ni habari njema sana kwetu na haya ni matunda ya kufanya vitu kwa nia njema na dhamira ya dhati ya kuwainua Watanzania tusiache kuomba kwa ajili ya taifa hili," aliongeza Jafo.

**Hizi tabia za halmashauri kusema hawana hela za vikao sijui viburudisho zisikwamishe ufanyikaji wa vikao, kutaneni hata saa nane mchana mpaka 10 jioni cha msingi mjadiliane changamoto zinazokabili hospitali hizo na kuzitafutia njia ya kuzitatua kwa pamoja.**

Wakati huo huo, Waziri Jafo aliziagiza halmashauri zenye Hospitali Teule (DDH), kuhakikisha wanafanya vikao na Taasisi za kidini zenye makubaliano ya uendeshaji wa hospital hizo.

"Hizi tabia za halmashauri kusema hawana hela za vikao sijui viburudisho zisikwamishe ufanyikaji wa vikao, kutaneni hata saa nane mchana mpaka 10 jioni cha msingi mjadiliane changamoto zinazokabili hospitali hizo na kuzitafutia njia ya kuzitatua kwa pamoja," alisema Jafo.

Alisema kuna changamoto ndogondogo ambazo zinaweza kutatuliwa kwa ushauriano tu, lakini unapoziacha kwa muda mrefu zinakuwa tatizo kubwa, hivyo ni vizuri wakiwa wanakutana katika uboreshaji wa huduma za afya kwenye halmashauri husika.

"Taasisi za dini mnafanya kazi kubwa sana katika Sekta ya Afya na kwa muda mrefu mmekuwa mkimiliki hospitali takribani 105 na serikali tulikuwa na hospitali 77 pekee kabla hatujaanza ujenzi wa hospitali za wilaya 67," alisema Jafo.

"Mmekuwa msaada katika kuwafikia wananchi ambao serikali ilikua bado haijajenga hospitali, niwapongeze kwa kuhakikisha huduma za afya zinapatikana karibu na wananchi na kwa haraka, hakika mmewasaidia Watanzania wetu kupata huduma bora za afya na mmeboresha afya zao," alisema Jafo.

Pia Jafo alisema mpango wa serikali ni kukamilisha mchakato wa kuajiri watumishi wa afya takribani 400 ambao watasaidia kupunguza uhaba wa watumishi wa afya katika vituo vya kutolea huduma za afya.

"Ninafahamu fika tatizo la uhaba wa watumishi katika hospitali nyingi za serikali, tunalifahamu hilo na tumechukua hatua za makusudi za kutangaza ajira za afya na sasa tunakamilisha mchakato wa ajira hizo na muda si mrefu mtaanza kuwapokea kwenye baadhi ya hospitali ambao wataongeza nguvu katika utoaji wa huduma za afya nchini," alisema Jafo.

Akizungumza katika kikao hicho Rais wa Chama cha Madaktari wa Kikristo Tanzania, Dk. Bwire Chirangi, alitaja changamoto zinazowakabili kuwa ni pamoja na kukosa vikao vya ushauriano, uhaba wa watumishi wa afya pamoja na miundombinu duni ya kuzifikia huduma.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Seleman Jafo (kushoto), akipokea karatasi za malipo ya benki kutoka kwa Mkurugenzi wa Taasisi ya Dk. Msuya, Dk. Ombeni Msuya (kulia), jijini Dodoma jana, ikiwa ni malipo ya msaada wa ada kwa wanafunzi wanaotoka kwenye mazingira magumu nchini, taasisi hiyo imewalipia ada wanafunzi 23 yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 3.5. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Waziri Mahiga amwagia sifa Makonda

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WIZARA ya Katiba na Sheria imeitaka mikoa mbalimbali nchini kuiga mfano wa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, wa kuweka jitihada ya kufuatilia masuala ya kijamii yanayogusa maisha ya watu.

Kauli hiyo ilitolewa na Waziri mwenye dhamana Balozi Augastine Mahiga, wakati akipokea mapendekezo ya maboresho ya Sheria ya Mirathi na Ndoa inayowakandamiza wanawake.

Balozi Mahiga alisema, Mkoa wa Dar es Salaam unapaswa kuigwa na mikoa mingine kwa sababu umeisaidia wizara kujua nini kinatendeka katika mikoa kwa upande wa kinamama wajane.

"Ninaomba mikoa yote igeni Dar es Salaam kwa sababu amekusanya maoni ambayo ni mwongozo katika mapendekezo ya mabadiliko ya sheria ya mirathi na ndoa," alisema Mahiga.

Alisema kuna manyanyaso mengi vijijini na mijini, lakini waathirika wanakosa mwongozo wa kufikisha sehemu husika.

"Naomba mikoa mingine mikubwa igeni mfano wa Makonda, lengo ni kuboresha sheria hiyo ili isiwakandamize," alisema Balozi Mahiga.

Hata hivyo, alisema wanatarajia kuwasilisha hoja hiyo bungeni wiki hii kama taarifa ili ijadiliwe na baadaye kupitishwa kama itakubalika.

Aliwataka Watanzania kujua maana ya ulinzi jamii, jinsi ya kuongeza thamani katika maisha ya kila siku.

"Naomba wanahabari mtusaidie kutangaza kwa sababu social security (ulinzi jamii) wengi hawajui, lakini ipo duniani na inalinda maisha ya binadamu," alisema Balozi Mahiga.

Kwa upande wa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Makonda, alisema kinamama wengi wananyanyasika ndio maana katika mkoa wake kwa kushirikiana na watendaji wake walifanyia kazi suala la sheria ya maboresho ya mirathi na ndoa.

Alisema wana kila sababu ya kufanya hivyo kwa sababu sheria hiyo ni ya muda mrefu na imepitwa na wakati.

Alisema mapendekezo yao ambayo yamewasilishwa kwa Waziri Mahiga wanaimani yatafanyiwa kazi kwa sababu yamefikia sehemu husika.

# Dodoma kuboresha barabara kupunguza ajali

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WIZARA ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi imeeleza mkakati wake wa kuboresha miundombinu ya barabara kwa lengo la kuzifanya kukidhi viwango vya ubora na kukabiliana na ajali zinazoweza kusababishwa na ufinyu wa barabara.

Barabara zitakazohusika na mkakati huo ni barabara kuu ya kutoka Mji wa Makambako Mkoani Njombe hadi Songea yenye urefu zaidi ya kilometa 250.

Akizungumza katika kikao cha baraza la ushauri la usalama barabarani nchini, Naibu Waziri wa wizara hiyo, Elius Kwandika, alitaja barabara nyingine itakayohusika na maboresho hayo kuwa ni kipande kingine cha barabara cha kuanzia katika mji wa Igawa mkoani Mbeya hadi mji wa mpakani wa Tunduma, mkoani Songwe katika Barabara ya Tanzania na Zambia (Tanzam), yenye urefu wa kilometa 266.

"Katika kipande hiki cha barabara ya Igawa Tunduma pia kitahusisha ya mchepuko katika Jiji la Mbeya ili kukabiliana na msongamano wa magari," alisema Kwandika.

Alifafanua kuwa mchepuko wa kilomita 40, utaanzia katika mji wa Uyole jijini Mbeya hadi Songwe viwandani na itatumika kwa ajili ya malori yote yanayosafirisha mizigo toka Bandari ya Dar es Salaam kupeleka nchi za Kusini mwa Afrika kupitia mpaka wa Tunduma.

Alisema serikali inaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu tatizo la kung'oa alama za barabarani ambazo ni kielelezo cha madereva katika uendeshaji hususani nyakati za usiku.

Kwandika alisema asilimia chache za ajali zinazotokea husababishwa na uharibifu wa alama za barabarani, lakini nyingi zinatokana na uzembe wa madereva.

Pia alisema serikali itaendelea kutoa elimu kwa wananchi ikiwamo kushirikiana na viongozi wa ngazi ya vijiji hadi mkoa kuhakikisha wanatoa taarifa ya watu wanaochukua alama hizo na kuziuza kama vyuma chakavu.

Alisema watu hao wakibainika serikali itawachukulia hatua kali kutokana na uharibifu huo.

"Serikali inaendelea kuwasaka wahalifu wanaotumia alama za barabarani kama chuma chakavu muuzaji na mnunuzi, wote watakuwa hatiani," alisema.





# Jamii Forums yashinda Tuzo ya Daudi Mwangosi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BALOZI wa Sweden nchini , Anders Sjoberg, amesema kuwa demokrasia na uhuru wa vyombo vya habari ni muhimu katika kukuza taaluma ya uandishi wa habari.

Akizungumza katika hafla ya tunzo ya mwandishi wa habari, Daudi Mwangosi, iliyofanyika Mjini Zanzibar alisema kuwa kuwepo kwa demokrasia na uhuru wa vyombo vya habari, kutawawezesha waandishi kufanya kazi kwa weledi.

Hafla hiyo ya Tunzo ya Daudi Mwangosi ilitwaliwa na Mtandao wa Kijamii -Jamii Forums, hivyo kujinyakulia Sh. milioni 10 katika kumbukumbu hizo zilizoandaliwa na Umoja wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC).

**Inawezekana kabisa kuwa, waandishi wa habari wamekosea pahala fulani katika harakati zao kama ambavyo wadau wengine wa ujenzi wa taifa wanavyoweza kukosea.**

Balozi huyo aliwapongeza waandishi wa habari wa Tanzania kwa kuwa na umoja na mshikamano kwa kuadhimisha siku hiyo ambayo inalenga kulaani mauaji ya wanahabari nchini.

Aliwataka kuendelea kufanya kazi zao kwa kuzingatia maadili ili kuweza kuepukana na migogoro mbalimbali.

"Ni vyema kuzingatia maadili ya kazi zetu ili kuweza kuitumikia jamii bila ya kuwa na migogoro na migongano katika jamii"alisema.

Charles Kayoka, Mwenyekiti wa Jopo la Majaji wa Tunzo ya Daudi Mwangosi ambayo huadhimishwa kila ifikapo Setemba 2, ambapo kwa mwaka huu ilifanyika jana, alisema kuwa jukumu la kuadhimisha siku hiyo ikumbushe kazi ya wadau wa habari kuwa si kuendelea kulalamika na kulaumiana bali kuwa daraja la kusameheana na kujenga umoja wa kitaifa.

Alisema huenda wadau wa habari bado hawajatambua dhima ya sekta ya habari hivyo kupitia tukio hilo watoe maelekezo ili itambulike kuwa lengo la waandishi wa habari si kubomoa,ila ni kuwa sehemu ya msingi na muhimu kwenye ujenzi wa taifa.

"Inawezekana kabisa kuwa, waandishi wa habari wamekosea pahala fulani katika harakati zao kama ambavyo wadau wengine wa ujenzi wa taifa wanavyoweza kukosea. Dawa si kuvunja madaraja ya kuunganisha bali ni kuitana, kufahamishana, kuelimishana na kukemea..., alisema Kayoka.



Balozi wa Sweden hapa nchini, Anders Sjoberg, akizungumza na waandishi wa habari mjini Zanzibar jana, katika maadhimisho ya kumbukumbu ya mwandishi wa habari, Marehemu Daudi Mwangosi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Idara za umma zifanye utafiti

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema ni muhimu kwa idara na taasisi zote za serikali kufanya utafiti, badala ya jukumu hilo kuachiwa Idara ya Mipango, Sera na Utafiti pekee yake.

Dk. Shein aliyasema hayo Ikulu mjini Zanzibar, wakati akipokea taarifa ya utekelezaji wa mpango kazi kwa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka 2018/2019.

Alisema katika kufanikisha jambo hilo, idara zinaweza kuwatumia wataalamu wake na pale wanapokosekana, ni vyema ikatoa mafunzo kwa wafanyakazi ili watumike kwa kazi hiyo, na kubainisha kuwa baadhi ya utafiti hauhitaji fedha nyingi.

Aliwataka viongozi wa idara za umma kufanya utafiti, sambamba na kujenga uwezo wa kitaaluma ili waweze kutekeleza shughuli hizo kwa ufanisi.

Aidha, alizitaka wizara kupitia Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa kuwasilisha waraka serikalini, ili kuujua ukweli baada ya kubainika kuwapo kwa baadhi ya wizara zilizonunua vifaa mbali mbali vya sherehe kwa lengo la kuvikodisha , jambo ambalo linapaswa kufanywa na idara hiyo.

Akigusia mchakato wa serikali kuihamishia mjini Dodoma Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali iliyopo Dar es Salaam, Dk. Shein alisema eneo la ardhi la ekari 30 ililopatiwa SMZ na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kubwa, hivyo akasisitiza azma ya serikali ya kuihamishia ofisi hiyo Dodoma, mara baada ya hatua ya ujenzi kukamilika.

Katika hatua nyingine, Dk Shein aliwakumbusha watendaji wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kama ilivyo Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, zinahitaji wafanyakazi wanaoheshimika na kuchapa kazi kwa weledi.

Aidha, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Idd, aliwataka watendaji wa ofisi hiyo kujifunza na kutekeleza kwa ufanisi yale yote walioelekezwa, kuambatana na shabaha na malengo waliyojipangia.

Aliwataka watendaji hao kuendelea na mshikamano wao na kufanya kazi kwa pamoja, akibainisha kuwa ndio siri ya mafanikio waliyoyapata, mbali na baadhi nyakati za kukabiliana na matatizo mbali mbali.

Mapema, akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa mpango kazi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Waziri wa Wizara hiyo, Mohamed Aboud, alisema kuna mafanikio makubwa katika kipindi hicho, ikiwemo kuratibu ujenzi wa nyumba ya makazi ya Makamu wa Pili wa Rais, unaoendelea kufanyika Pagali, kisiwani Pemba,

Katika hatua nyingine, Waziri Aboud alisema Ofisi ilichukua hatua ya kuandaa ujenzi wa ukuta eneo la fukwe huko Msuka ili lisiendelee kumong'onyoka kutokana na maji ya bahari, kazi itakayogharamiwa na serikali.

# SMZ kuboresha ofisi za umma

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), imeahidi kuimarisha miundombinu na ujenzi wa ofisi za umma ili kuwawezesha watendaji wake kufanya kazi kulingana na maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Kufanya hivyo ni kuendeleza azma ya serikali ya kutoa huduma bora kwa wananchi sambamba na kuongeza ufanisi kwa watumishi wa umma.

Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Shaaban Seif Mohamed, alieleza hayo wakati alipofanya ziara ya kushtukiza katika Tume ya Usimamizi na Uratibu wa Dawa za Kulevya ikiwa ni mwendelezo wa ziara zake za kukagua taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, eneo la Kidonge Chekundu.

Mohamed alisema ziara yake kwenye taasisi hiyo imemwezesha kujionea hali halisi ya watendaji hao kufanya kazi katika mazingira magumu.

Uongozi wa wizara una wajibu wa kuangalia namna gani unaweza kuipatia ufumbuzi changamoto hiyo, alisema.

Aliwataka watendaji hao kuendelea kuvuta subra katika kutoa huduma kwa mujibu wa mazingira walionayo huku serikali ikiendelea kutafuta eneo jingine mbadala kwa ajili ya ujenzi wa ofisi mbali mbali kwa zile taasisi ambazo bado zinakabiliwa na changamoto hiyo.

"Ili Mfanyakazi afanye kazi kikamilifu anahitaji apate sehemu yenye mazingira mazuri ya kufanyia kazi," alieleza Katibu Mkuu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya, Heriyangu Khamis, alisema licha ya kwamba tume hiyo inakabiliwa na changamoto ya mazingira ya kufanyia kazi lakini watendaji wake wanaendelea kujituma kwa uadilifu bila ya kukata tamaa.

Alisema kutokana na changamoto inayowakabili wamelazimika kulisanifu jengo walilonalo ili likidhi haja kwa wafanyakazi.

"Urefu wa jengo letu haukidhi haja kwani hauruhusu hewa safi kuingia ndani kama inavyostahili". Alisema Mkurugenzi Khamis.

Akizunngumzia suala la utendaji kazi alisema tume inafanya kazi zake kwa umahiri na umakini katika kuisaidia jamii kuachana na vitendo viovu vya utumiaji wa dawa za kulevya sambamba na kuzuia dawa hizo kuingizwa nchini.


Alisema ofisi hiyo tayari imeandaa maandiko mbali mbali yenye mapendekezo na karibuni yatawasilishwa wizarani kwa ajili ya kujadiliwa ili kupata ufumbuzi wa kujengwa kwa majengo mapya ya ofisi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII



Soma UK. 14
RAYVANNY

JUMAMOSI SEPTEMBA 7, 2019



# WAMEAMUA

## KIBA, ASLAY WANA SIRI NZITO UK.16

BASI SAWA



## Fid Q akataa utumwa Afrika Kusini

RAPA mkali, Farid Kubanda maarufu Fid Q, amesema hakufanya kosa kukacha onyesho lake Afrika Kusini kwani yeye kama Mwafrika anaguswa na mauaji yanayotokea nchini humo.

Fid Q amesema ameamua kuahirisha shoo yake ya MTV BASE SHOW CASE, ili kuondokana na utumwa wa kuimba na kucheza katika nchi ambayo hawapendi watu wengine.

"Wakati nikiwa Afrika Kusini napenda kuburudisha mashabiki wangu Watanzania, lakini kwa hali iliyopo huwezi kufanya jambo hilo kutokana na usalama kuwa mdogo, mimi naona jambo hili ni baya na halipaswi kufanywa na watu weusi kama sisi," amesema.



## Rayvanny awafundisha Waafrika kupenda

MSANII wa muziki wa Bongo Fleva, Rayvanny, amekuwa msanii wa kwanza kutoka Afrika Mashariki kuachia wimbo maalum wa kukemea vurugu za ubaguzi zinazoendelea nchini Afrika Kusini.

Wimbo huo wa 'AFRICA', Rayvanny amesikika akisema "Kama hatutakemea machafuko yanayoendelea, Basi siku moja machafuko yatatumaliza wote".

Rayvanny pia ametumia nukuu za muasisi wa Taifa la Afrika Kusini, Hayati Nelson Mandela akisema "Watu wanajifunza kuchukia, na kama wanajifunza kuchukia basi wanaweza pia kujifunza kupenda,".



# JUX KUONGEZA NGUVU KWENYE MITINDO

MWANAMUZIKI wa RnB, Juma Jux, ameanza safari yake ya kusaka pesa nje ya muziki kwa kuboresha nembo yake ya kibiashara.

Wiki hii msanii huyo kupitia uongozi wake wametembelea maduka ya Kariakoo na kugundua kuna bidhaa nyingi zenye nembo feki ya 'African Boy'ambayo ni mali ya mwanamuziki huyo.

Jux ambaye bidhaa zake za nguo zinapendwa na vijana wengi, kwa siku za hivi karibuni ameonekana kujikita katika sekta ya mavazi.

## INSTA-TWITTER





**Dora** ni msichana wa aina yake.Msichana aliyetimia kila kipimo. Ana kila kitu alichotakiwa kuwa nacho, mwanamke wa kidunia. Dora ni msichana mwenye urefu wa kadiri usiochosha wala kuchusha kumtazama. Wembamba wake unachukuana na kuafikiana barabara na urefu wa kimo chake. Namuombea nafasi-**Gabo Zigamba**.



**Ukiendekeza** mapenzi utakwanguliwa uwe bwege mtozeni-**Rich Mavoko**.



## Finaly atambulisha 'Mukide' kibabe

MSANII wa bongoflava Abubakari Mrisho 'finally', ameachia wimbo wake mpya uitwao 'Mukide' na kutangaza ujio wa shoo yake hivi karibuni.

"Najisikia furaha sana kufikia mafanikio haya katika kipindi hiki kwani nimeanza kusambaza wimbo huu na baadaye kufanya shoo,"alisema Finally.

Shoo yake hiyo itakwenda sambamba na sherehe ya kutimiza miaka 10 kampuni ya Pilipili entertainment ambayo inamsimamia kikazi.




@burudanitele

**>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

UNASEMAAA...



# MADEE
## AZUIA NYIMBO ZAKE KUCHEZWA TV

MKONGWE wa muziki wa bongoflevani, Madee Ally, amepiga marufuku nyimbo zake ambazo picha zake alizichukua nchini Afrika Kusini, kuchezwa kwenye vituo vya televisheni kupinga kuwashambulia na kuuawa kwa wageni.

Madee amesema machafuko yanayoendelea nchini humo juu ya raia wa kigeni hasa wakiafrika yamemsikitisha na ameamua kuzuia zisipigwe pamoja na kumuenzi rais mstaafu wa Zimbabwe mzee Mubage aliyefariki dunia usiku wa kuamkia jana.

"Mambo vipi naitwa MadeeAlly, leo, Sept 06 2019 kwa hiari yangu nimeamua kuzuia kuchezwa kwa nyimbo zangu ambazo nimezifanya kwenye ardhi ya South Africa especially HYPERLINK "https://www.instagram.com/explore/tags/vuvula/" #VUVULA na zingine zisipigwe kwenye kituo chochote cha habari na zaidi ikiwa ni TV, Kwa sababu TV ndio kitu kinachoonyesha mandhari ya nchi tajwa ambayo ni SA. Binafsi nimechukua hatua kwanza kwa kuufuta hata kwenye channel yangu ya Youtube ambako ulikua unapatikana," amesema.

## INSTA-TWITTER


Tuffolow/ Tu-tag
@burudanitele



**Oyaa** mabaharia jitokezeni basi. Ile saa imekaribia sasa, muda wowote kinawaka-**Joh Makini**.



**Bora** kuchelewa kuliko kukausha kabisa-**Timbulo.**



**Siku** utakapopata tatizo ndiyo utajua rafiki na watu unaowafahamu tu-**Chuchu Hans.**

# Kuumbe!



# WAMEAMUA

## KIBA, ASLAY WANA SIRI NZITO

WIKI hii mashabiki wa Bongofleva wamepata kitu chenye ladha tofauti kutoka kwa wanamuziki wawili ambao haikutarajiwa kama siku moja watafanya kazi pamoja.

Wanamuziki hao nyota, Ali Kiba na Aslay wametoa ngoma yao ya kwanza 'Bembea'ambayo inawapeleka puta mashabiki .

Hata hivyo wadau wa muziki wanahoji muungano huo wa wasanii hao umekuja kama bahati mbaya? Ukweli ni kwamba hapana, wawili hao wanajua kwa nini wameamua kushirikiana lakini imebaki kuwa siri yao.

Wimbo huo umefunika siri hiyo licha ya wasanii hao kuonekana wenye jambo Fulani ambalo pengine tunaweza kulisikia siku za mbele.

Wachambuzi wa burudani wanaeleza kwamba Aslay alionekana ameanza kubanwa, akashindwa kupumua kwa kile kinachodaiwa kuwa kupigwa vita kutoka kwa wasanii wenzake hasa baadhi ya wale waliotoka nao Yamoto Band.

Kutokana na vita kuwa kubwa na yeye kukosa  uwezo wa kuhimili, ndipo alipotunga kibao cha 'Chuki' angalau atoe kinyongo chake ili wasiofahamu wajue.

Kubanwa huko kila kona kunakofanywa na mahasimu wake wa kisanii, aliona bora ajisalimishe kwa Ali Kiba, mfalme wa Bongo Fleva ili angalau kipaji chake kiendelee.

Akihojiwa na redioa moja Aslay alikiri kwamba yeye ni mshabiki mkubwa wa Kiba "tangu nikiwa mdogo namkubali sana Kiba, na nilipoanza kutunga mashairi ya 'Bembea' niliona mtu wa kwanza ni kaka yangu,".

Kiba naye amemwagia sifa Aslay akisema ni msanii mwenye kipaji na kushirikiana naye si jambo la bahati mbaya.

Kwa kusikiliza kwa makini maelezo yao, utagundua wasanii hao kuna kitu kinaendelea kati yao, na baadhi ya mashabiki wao wanabashiri umoja huo utaendelea.



# NGOMA MPYA 5 KALI MWEZI AGOSTI

**Na Adam Fungamwango**



TUMEINGIA mwezi Septemba, huku mwezi uliopita tukishuhudia tasnia ya muziki wa kizazi kipya nchini ikifanya kazi kubwa.

Ni mwezi ambao baadhi ya wasanii walifanya kazi ya 'kufa mtu' na kutoa ngoma kali ambazo zimetokea kupendwa na mashabiki wa muziki huo.

Lakini vile vile kumekuwa na mageuzi fulani, kwani mara nyingi tumeona wasanii wakitoa ngoma karibuni asilimia 99 ni za mapenzi.

Leo tutaangalia baadhi ya wasanii waliotoa ngoma mwezi Agosti ambazo zimekuwa zikitamba kwa sasa kwenye vyombo vya habari pamoja na mitandao ya kijamii.

**Harmonize-Magufuli**

Ni ngoma kali iliyotolewa mwanzoni mwa mwezi Agosti. Ilikuwa ni tarehe mbili, msanii maarufu kwa sasa nchini Harmonize, alipotoa ngoma iitwayo 'Magufuli'.

Katika ngoma hiyo, msanii huyo ameainisha kila kitu kilichofanywa, kuendelea kufanya na vile ambavyo vimeahidiwa kufanywa na Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Rais Dk. John Magufuli.

Ukiisikiliza ngoma hiyo, mtunzi amebainisha vitu vyote kama vile ununuzi wa ndege, ujenzi wa madaraja, reli, nyumba za serikali, pamoja na kuwabana watumishi wazembe.

Ni ngoma ambayo imetokea kupendwa mno, sehemu mbalimbali ya nchi na hata kwenye mikutano wa serikali.

**Lameck Ditto-SADC**

Ditto, ambaye zamani aliitwa Dogo Ditto ameandika mashairi, akaungana na baadhi ya wasanii nchini, wakaingia studio na kutoa ngoma iitwayo 'SADC'.

Hii ni Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ambayo ilikuwa na mkutano wake hivi karibuni nchini Tanzania, chini ya mwenyeji na Mwenyekiti Mpya wa Jumuiya hiyo, Dk. John Magufuli ambaye alikabidhiwa kijiti hicho kutoka kwa Rais wa Namibia Dk. Hage Geingob.

Kutokana na mkutano huo kuwa nchini Tanzania, Rais akipokea viongozi wa serikali kutoka nchi 16 za Jumuiya hiyo, wasanii wa Kibongo hawakuwa nyuma, kwani walitoa ngoma Agosti 14, chini ya Ditto, kundi wakaliita Tanzania All Stars,  ambayo inahimiza umoja, mshikamano wa Waafrika.

**Lavalava ft Susumila-Warembo**

Agosti 9, msanii Lavalava naye hakuwa nyuma, kwani alitoa ngoma yake akishirikiana na Susumila, walioiita 'Warembo'.

Hii ni ngoma ya mapenzi ambayo imeanza kubamba mashabiki wengi, wakikimbizana na kutoka kwenye mtandao wa kijamii kwa ajili ya kuisikiliza.

**Gnako ft Nikki wa Pilli-Kitonga**

Msanii wa hip hop, Gnako, akishirikiana na mwenzake Nikki wa Pilli, nao mwezi Agosti hawakuwa nyuma. Walikuja na ngoma yao walioiita 'Kitonga'. Imetoka Agosti 15, huku mashabiki wa muziki huo wakichamka kuingia kwenye mitandao ya kijamii kuiangalia video na kuisikiliza ngoma hiyo kali ambayo jamaa 'wamechana kirogo mbaya'.

**Darasa ft Mausa Sama-Shika**

Yule jamaa wa ' rudi ututoni, usipotembea utabebwa mgongoni' umekuja na ngoma yake kali inayotwa 'Shika'. Huyu si mwingine ila Darasa. Huyu ndiyo aliyotoa ngoma moja kali iliyotesa nchini iitwayo 'Muziki'. Sasa Agosti 22, ametoa ngoma hiyo ambayo bado ya moto na muda si mrefu inaweza kuwa gumzo nchini, kwani tayari mashabiki wameshaanza kuifuata kwenye mitandao ya kijamii na kuwa na waangaliaji wengi kwa muda mfupi tu.

# Vijimambo

1. Hii ndio inaitwa 'nikinywa maji, nakuona kwenye glasi' - Agatha Mbale, Moro Town.
2. Ai weeewe, naoomba - Ebby Mbwambo, Tanga.
3. Hahahaaa, endelea kuomba tu mzee baba, atakupa tu - Maunda Alawi,
4. Duuh, kweli utoto kazi! Kidume kinategemea kabisa kimegewe mkate! - Beneali Moussa, Zenji.
5. Naomba, ukinipa na mie nikinunuliwa soda nakupa - Mauwa Minde, Kibada Kigamboni DSM.
6. Lazima huyo dogo atakua wa Bush Stars, anaiomba picha mkate! - Sultani Ubwa, Kibada DSM.
7. Endelea tu kuomba, huyo siyo mchoyo atakumegea tu - Moussa Beneali, Migombani Zenji.
8. Kama ulikuwa hujui tafsiri halisi ya neno 'zwazwa', basi ndio hiyo - Beneali Moussa, Migombani Zenji.
9. Naenda kukusemea kwa mama yako umeomba mkate kwa watu ->Julius Anthony, Usagara Tanga.
10. Acha uchoyo wewe, mwenzio anakuomba ndio unaingiza wote mdomo! - Mama Nah, Manzese DSM.
11. Mwache na uchoyo wake, na wewe ukinunua vitu vyako usimpe - Rehema Bwahoja, Buguruni DSM.
12. Dogo utachubuka 'makongoro' kwa kupiga magoti, hiyo picha tuu - Subira Bwahoja, DSM.
13. Jamani, si mngemuambia kama hiyo ni picha tu sio mtu kweli. Ona sasa anavyotia huruma - Dule DSM.
14. Yes, hiyo ndio dawa ya ombaomba. Kesho leteni roli lenye picha ya hela - Kijusi, Magomeni Mapipa DSM.
15. Daaah, mjukuu wa 'Matonya' anadhalilika hivi hivi kwa picha tu - Kijusi, Magomeni Mapipa DSM.
16. Huyo naye kubwa zima hajajua tu picha na mtu wa ukweli? Muacha achune magoti - Kole, Msata Pwani.
17. Hapo atalifuata gari mpaka wapi kwa kupiga magoti hivyo Magdalena Kachenja, Mabwepande DSM.
18. Tatizo dogo hajafunguka, anataka mkate au anataka uchumba - Alli Shaaban Mpanjira, Mbagala Kuu DSM.
19. Kweli walimu wanakazi. Huyo mpaka aje kujua hiyo ni picha tu si atakua Chuo Kikuu! - Pili Mpanjira DSM.
20. Mmmh, mie mgeni hapa, acha nipite tu! - Abass Ngulunga, Msasani Macho, DSM.
21. We mtoto utagongwa na magari buree. Huyo sio mtu kweli ni picha tu - Bernad Isuja, Makore Dodoma.


**SMS Bomba ya Leo:**

**Tatizo dogo hajafunguka, anataka mkate au anataka uchumba -Alli Shaaban Mpanjira, Mbagala Kuu DSM.**

## PICHA MPYA




**TUMA MESEJI - 0773 477311**



# Watoto Watatu Yatima nyuma ya giza la haki

**Na Adam Fungamwango**

DUNIA hii ina mambo mengi sana mengine ya kusitikisha.

Unaweza kukuta hata watoto yatima wanadhulumiwa haki yao, lakini jamii iliyowazunguka iko kimya tu, inaangalia.

Wakati mwingine watoto hao wanakuwa wadogo na hawana uwezo au akili ya kutafuta haki zao kwa njia yoyote ile, iwe kwa nguvu au kisheria bila msaada wa watu wazima.

Watu wazima wenyewe nao utakuwa wanawaangalia tu kwa kile ambacho wakati mwingine utaambiwa, wanaogopa kuwasaidia kwa kuhofia kuharibu ujirani.

Mtunzi wa filamu ya 'Watoto Watatu' amefikiri mbali sana na kutujia na filamu hii, ambayo ushauri wake ni kuwataka watoto kwanza kupambana kwanza wenyewe kwa sababu siku hizi watu wanaogopa sana kutoa msaada.

Imechezwa na wasanii Mohamed Fungafunga, Ben Blanco, Sudi Muhogo, Geovina Innocent, Rehema Mohamed, Husna Sudi, Islam Kitwana, Godfrey Lucas, Malaika na wengineo.

Neira, binti wa miaka 10 amefiwa na wazazi wake. Shangazi yake ndiye sasa ameikalia nyumba kama ya kwake.

Ili aichukue moja kwa moja na aishi kwa amani, anamkodisha muuaji ili ammalize mtoto huyo, lakini anaamua kukimbia nyumbani kwao, kabla hajauawa.

Binti wa mama huyo, Yusta ambaye anampenda mno Neira, anajikuta kwenye wakati mgumu na kupigwa na mama yake, pia kutishiwa kuuawa kama ataendelea na tabia ya kulia na kumuulizia Neira.

Binti huyo anajikuta anakuwa chokoraa wa mitaani na huko anakutana na wenzake wawili Samira na Samili. Wanamuuliza kisa cha yeye kuwa pale. Baada ya kuwahadithia, wanamwambia kuwa kisa chake kinafanana na wao.

Wao wametimuliwa kwenye nyumba na babu yao baada ya baba yao kufariki dunia, hivyo na wao hawana pa kuishi.

Baada ya majadiliano ya muda mrefu nini wafanye kwani kumekuwa hakuna msaada wowote kutoka kwa jamii, wanaamua wenyewe waingie kazini.

Samira akaenda nyumbani kwa shangazi yake Neira kuomba kazi ya uhausigeli. Kwa bahati anaipata. Bahati kubwa kwake ni kwamba hata Yusta binti wa umri usiozidi miaka 12 alikuwa amechoshwa na tabia za mama yake, hivyo alimpa kampani kubwa Samira.

Neira naye alikwenda kuomba kazi kwa mzee Jengua, lakini kwa bahati mbaya alimkatalia.

Kitendo cha kusahau kufunga mlango na kuondoka, kilimpa nafasi Neira kuingia ndani na hata alipokumbuka, alirejea na kufunga, bila kujua kuwa kuna mtu ameingia.

Aliporudi na kufungua mlango, akamkuta binti huyo ambaye naye umri wake ni miaka 10, alishtuka na kuingiwa woga akidhani ni jini.

Hiyo ilimpa nafasi Neira kujifanya jini na kuanza kumpa masharti mzee Jengua, sivyo angenyonya damu yake.

Wakati watoto wote wawili wakiwa sehemu tofauti, mtoto wa kiume Samili asiyezidi miaka 13 yeye alibaki mitaani, lakini akiletewa taarifa na mabinti.

Akishirikiana na Yusta, Samira alifanikiwa kuchukua hati za nyumba ya shangazi wa Neira, huku Neira naye akifanikiwa kuchukua hati za nyumba inayokaliwa kimabavu na babu wa kina Samira na Samila.

Samira na Yusta wanamshirikisha mlinzi wa getini Ben kuwaonyesha walipo wanasheria kwa sababu awali wazazi wao waliwaandikisha wao, lakini baadaye wavamizi walizibadilisha.

Ben anafanikiwa kuwasaidia Samira, Samila na Neira na hati zote zinarudishwa kwa majina ya warithi halisi.

Mzee Jengua anaondolewa kwenye nyumba ya urithi ya kina Samira na Samili kwa kazi iliyofanywa na Neira, huku Neira naye akiipata nyumba ya wazazi wake kwa kazi iliyofanywa na Samira, mama Yusta akitimuliwa.



# ANUSURIKA

## KEVIN HART APASULIWA MGONGO MARA TATU

MWIGIZAJI mkongwe wa Hollywood,Kevin Hart (40), anaendelea kupigania maisha yake baada ya kufanyiwa upasuaji mara tatu mgongoni.

Hart amefanyiwa upasuaji baada ya kuumia katika ajali mbaya ya gari iliyotokea katika barabara kuu ya Mulholland huko Malibu, Marekani.

Kulingana na mtandao wa TMZ, vyanzo vya uhakika vilieleza kwamba mwigizaji huyo alifanyiwa upasuaji huo baada ya kugundulika mgandano wa damu katika sehemu ya uti wa mgongo.

Ilieleza kwamba upasuaji mwingine ulikuwa kurekebisha mifupa ya uti wa mgongo na alirekebishwa sehemu ya nyonga.

"Tunashukuru utaratibu huo ulikuwa wa mafanikio na anatarajiwa kufanyiwa mazoezi kwani upasuaji kama huo mara nyingi zinaweza kusababisha matatizo makubwa kutembea au kupooza sehemu ya viungo," amesema mmoja wa watu wa karibu.

Nyota huyo wa filamu ya 'Get Hard' anatarajiwa kutumia miezi kadhaa akifanya mazoezi ya ukarabati wa mwili kwa hivyo uwezekano wa ratiba yake ya kazi, ikiwa ni pamoja kucheza filamu tano kuathirika.

Mpenzi wa Kevin, Eniko, hivi karibuni aliwahakikishia mashabiki kuwa mumewe wake atakuwa na afya njema.

"Yeye ni mzima atakuwa sawa." Alisema.

Eniko ambaye ana mtoto wa miezi 22 Kenzo, alisema kwamba nyota ya msanii huyo iko macho, lakini aliweka tahadhari kwa kusema atahitaji kukaa hospitalini kwa muda kidogo ili kupona kutokana na upasuaji na kutulia akili baada ya ajali hiyo.

Ajali hiyo ilitokea Plymouth Barracuda baada ya gari hilo kupinduka mara kadhaa kwenye barabara kuu huko Malibu Hills, California, na kuishia karibu mita 10 kutoka barabarani.

Wote Kevin na dereva wake walipelekwa hospitalini baada ya kupata majeraha makubwa ya mgongo.

# Pettit ukitoka hapa bahati yako



Cameron James Pettit amefunguliwa kesi akihusishwa na kifo cha utatanishi cha mwanamuziki Mac Miller.

Kwa mujibu wa TMZ, rapa huyo alikufa baada ya kupatiwa na kijana huyo mwenye umri wa miaka 28 kifurushi cha dawa ya kulevya aina ya oxycodone.

Hii ni kesi mpya kwa Pettit ambaye alisomewa mashtaka ya kurasa 42 katika Mahakama ya Wilaya ya California.



## MI Abaga hukujua ubaguzi ni sumu?

MKALI wa muziki kutoka Nigeria, MI Abaga, amewaomba radhi wananchi wa nchi hiyo kutokana na Tweet yake aliyoiweka hivi karibuni.

MI Abaga amechukua hatua ya kuomba msamaha baada ya ujumbe wake huo aliozungumzia mapigano ya ubaguzi yanayoendelea nchini Afrika Kusini kueleweka vibaya.

Mwanamuziki huyo katika ujumbe wake alimtetea rapa wa Afrika Kusini, AKA, ambaye aliwalaumu baadhi ya Wanageria kusababisha madhara nchini mwake.

## Genevieve ataka umoja dhidi ya wauaji A Kusini

MWIGIZAJI mkongwe wa Nollywood, Genevieve Nnaji, amesema imefikia muda kila mmoja kuonesha anachukia kile kinachoendelea Afrika Kusini.

Genevieve amesema hayo akiungana na wasanii wengi wa nchi hiyo kupinga vitendo vya mauaji dhidi ya wageni yanayoendelea nchini humo na kusema watu wanaoendelea kuwaua Wanigeria lazima wafahamu wao ni nani kwa kusimama pamoja.

"Tuoneshe tumefika muda wa mwisho tusimame pamoja, wacha watufahamu ni muda wa kuwaambia sisi ni nani," ulisema sehemu wa ujumbe wake.





## Harusi ya Davido, Chioma pasua kichwa

WIKI hii mashabiki wa muziki walijikuta wakielekeza macho na masikio yao kwa mwanamuziki Davido na mchumba wake Chioma.

Davido Adeleke alimtambulisha Chioma Avril Rowland kwenye familia yake na hapo kuibua habari kubwa katika mitandao ya kijamii nchini humo na Afrika kwa ujumla.

Baada ya utambulisho huo, mashabiki wengi wanahoji harusi ya nyota huyo itakuwa ya aina gani na gharama yake ni kiasi gani kwani wanavyofahamu msanii huyo anapenda ufahari na kujigamba kuwa ana fedha.

## Ikechukwu shukuru Mungu wamekuachia

RAPA kutoka Nigeria, Ikechukwu, ametumia mtandao wa kijamii kulaumu kikosi cha polisi cha kupambana na ujambazi SARS kuwa utendaji kazi wake unatia hofu.

Katika ujumbe wake, msanii huyo amesema yeye amekuwa miongoni mwa watu walioathiriwa na polisi hao kiasi ambacho kimempa mashaka.

Amesema Septemba 4, mwaka huu SARS walimvamia akiwa barabarani jijini Lagos na kumtisha kama yeye alikuwa mhalifu.



**SAFU**



**MIONZI YA SHERIA**

Na John Juma
0716217615

# Huna sababu ya kuhofu kulipa kodi

VIJANA wengi wajasiriamali wadogo kwa wakubwa wamefungua kampuni na hakika, wote waliofanya hivi wamelenga jambo jema linaloendana na wakati. Ni zama za viwanda na uwekezaji ili kuwa na Tanzania ya uchumi wa kati.

Katika safu hii makala za nyuma tuliwahi kuandika namna nyepesi ya kuanzisha kampuni na kufafanua kuwa ni vigumu kwa leo kufanya biashara na ukawa na mafanikio nje ya kampuni na utaratibu rasmi unaoeleweka.

Makala zikaleza kuwa hata kama unauza maziwa, mama lishe, mayai , kibanda cha huduma ya fedha kupitia simu, unauza vitafunwa kama mihogo huzuiliwi kufungua kampuni.

Kuna kampuni hata za mtaji mdogo na pengine wapo wenye milioni moja na pesa hiyo si lazima uwe nazo mkononi ila ni katika maandishi pekee.

Nipashe ikasema kuwa anayetaka mafanikio kwa sasa ahakikishe biashara yake hata kama ni ndogo kabisa anaifungulia kampuni.

Kwakuwa wapo wengi ambao tayari wamefungua kampuni basi zipo changamoto nyingi wanazokumbana nazo na kubwa zaidi ni taarifa au ujuzi wa mambo mbalimbali ya namna ya kuendesha kampuni ili iwe na mafanikio.

Moja ya eneo lenye shida au ambalo wajasiriamali wadogo hawana taarifa bora kuhusu masuala ya kodi zinavyolipwa na kwa mujibu wa sheria.

Wengi hawajui ni kiasi gani, kwa muda gani na vipi ndiyo maana leo tunakujuza na kukueleza kwa uchache kuhusu kodi za kampuni.

Kampuni hulipa kodi ya mapato, na wengi ni vyema wakafahamu jibu la swali hili kodi ya mapato ninini?

### KODI YA MAPATO

Kodi ya mapato kwa Tanzania ni tozo kwa wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayotokana na vyanzo vitatu ambavyo ni ajira, biashara pamoja na uwekezaji.

Aina hii ya kodi inatozwa kwa Mamlaka ya Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004, kama ilivyorekebishwa. Kwa upande wa kampuni kodi inayolipwa kwa tafsiri hiyo hapo juu ni kwakuwa kampuni ni biashara na pia ni kwakuwa ndani ya kampuni unaweza kuwamo uwekezaji. Hii ndiyo sababu kampuni hulipa kodi ya mapato.

### NANI ANALIPA KODI

Si kila kampuni hutakiwa kulipa kodi ya mapato. Mjasiriamali anatakiwa kujua kuwa si kampuni zote hutakiwa kulipa kodi ya mapato.

Ambazo zinazotakiwa kulipa kodi ya mapato ni kampuni zenye dhima ya ukomo ambazo ni Limited. Kama kampuni yako ni Limited (Ltd) basi inatakiwa kulipa kodi ya mapato. Nyingine zinazotakiwa kulipa kodi ni kampuni za kudumu za ndani na matawi ya kampuni za wageni wasio wakazi. Kwa vile hizi hazihusiki na wajasiriamali tuziweke pembeni.

Aidha, kama kampuni umeiunda na umeingia ubia na kampuni nyingine basi hutakiwi kulipa kodi ya mapato.

Huna haja ya kuogopa kodi hutozwa katika faida tu na si kutoka kila fedha unayoingiza. Katika kodi ya mapato ya kampuni hutozwa kwenye faida tu iliyotokana na shughuli za biashara za kampuni au faida uliyoipata kutokana na uwekezaji. Ikiwa umeunda kampuni umempata mtu ana mtaji akawekeza mtaji, faida inayopatikana hapo ndiyo faida kutoka katika uwekezaji.

Ifahamike kuwa si kweli kuwa kila unachoingiza lazima kilipe kodi, faida tu ndiyo hutozwa kodi ya mapato lakini tujiulize swali, biashara unafanya wewe , akaunti za kampuni unazo wewe, kila kitu kuhusu kampuni yako ni wewe, je hawa watu wa mapato wanajuaje faida unayopata ili wakutoze kodi sahihi .Kuna mambo yafuatayo ;

Kuna kitu kinachoitwa utangazaji wa mapato na kodi ambacho ni tamko linalowasilishwa TRA kuonyesha mapato na kodi inayopaswa kulipwa kwa kila mwaka wa mapato.


Kwa mujibu wa sheria ya kodi, kampuni inalazimika kuwasilisha makisio hayo hata kama haina faida. Wewe mwenyewe unajitathmini umepata nini na unatakiwa kulipa nini na unapeleka mwenyewe makadirio hayo. Kinyume chake ni kosa na asiyefanya hivyo adhabu inamsubiri.

Suala jingine ni hesabu za makadirio hayo unayopeleka TRA, lazima yawe yamefanywa na mhasibu ambaye anatambuliwa na bodi ya uhasibu Tanzania na kukaguliwa na mkaguzi wa hesabu anayetambulika pia.

Hawa ndiyo wanaotegemewa na TRA kupeleka ukweli iwapo umepata faida kiasi gani na unatakiwa ulipe kiasi kama kodi ya mapato. Ndiyo maana wanaitwa wahasibu wanaotambulika na bodi

Ikumbukwe kuwa kodi ya kampuni ni asilimia 30 tu ya faida. Kiwango kinachotumika cha kodi ya mapato ya kampuni ni kukatwa asilimia 30 ya faida, na kwa kawaida hulipwa katika hatua mbili.

Kodi ya kwanza hulipwa kulingana na makadirio ya mlipa kodi mwenyewe mwanzo wa mwaka wa biashara na ya mwisho hulipwa baada ya utathmini rasmi wa mapato kamili mwisho wa mwaka wa mapato.



**KALAMU YA MWALIMU**

Na Reubeni Lumbagala

# Hongera Mo kuwainua vijana

SAFARI ya masomo ni ndefu na mlolongo unaanzia pale mwanafunzi anapohitimu darasa la saba na kuingia sekondari. Mara nyingi changamoto huibuka hatua zinapovisogelea vyuo vikuu baada ya kumaliza kidato cha sita.

Kwenye elimu ya juu tofauti na shule za msingi na sekondari, hakuna kuungaunga. Jambo kubwa ni majibu ya wapi pa kupata fedha za kugharamia masomo ya chuo kikuu. Unahitaji mkopo au uhisani. Na zama hizi si kila anayeomba fedha kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), atazipata.

Katika kusaidia kumaliza changamoto ya uhisani wa masomo ya elimu ya juu Taasisi ya Mo Dewji, kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), inatoa ufadhili wa masomo kwa vijana wanaotoka familia maskini na wenye ufaulu wa juu wa daraja la kwanza na pili au divisheni I & II ili kuweza kupata nafasi ya kutimiza ndoto zao za kupata elimu ya juu katika chuo hicho kupitia mpango wa 'Mo Scholarship Program.'

Mfanyabiashara Mo Dewji hufadhili ada na fedha za kujikimu ili kuwawezesha wanafunzi hao kusoma kwa kutumia teknolojia ya kielektroniki wawapo chuoni. Aidha, huwapatia kompyuta mpakato kwa wanafunzi wanaofanya vizuri katika masomo yao wawapo mwaka wa kwanza chuoni.

Kompyuta ni nyenzo muhimu kwa wanafunzi kujifunza hasa wanafunzi wa elimu ya juu. Baadhi ya vitabu vya marejeo ambavyo wanafunzi wanapaswa kuwa navyo ili kujiongezea maarifa na kuvitumia katika kujibu maswali ya makundi vinapatikana kwa njia ya mtandao.

Upo umuhimu wa wanafunzi wa vyuoni kuwa na kompyuta hasa kompyuta mpakato ambayo wana uwezo wa kutembea nayo sehemu mbalimbali katika kufanya shughuli za kimasomo.

Kwa kutambua gharama kubwa za mahitaji ya elimu ya juu, Taasisi ya Mo Dewji imejitolea kutoa ufadhili kwa baadhi ya wanafunzi wachache wa masomo ya sayansi kutoka familia duni ili waweze kupata haki yao ya msingi ya kupata elimu kwa ngazi za juu zaidi.

Kwa mwaka wa masomo 2016/2017, taasisi ilitoa ufadhili kwa wanafunzi saba na kwa mwaka wa masomo 2017/2018, wako 22 kwenye ufadhili huo.

Dewji akitangaza orodha ya wanafunzi 22 waliopata ufadhili kwa mwaka wa masomo 2017/2018, anasisitiza kwa wanufaika hao kujituma ili waweze kufikia malengo waliyojiwekea katika maisha yao. Dewji anasema "Mmepata ufadhili huu muutumie vizuri, wapo wengi ambao walituma maombi lakini nyie mmefanikiwa kupata msaada. Msome kwa bidii na baadae mpate kazi bora ambazo zitawasaidia kupata kipato na kusaidia ukuaji wa uchumi wa nchi".

Miongoni mwa wanufaika wa ufadhili wa Taasisi ya Mo Dewji ambaye hatasahau taasisi hii katika maisha yake ni Amos Ntandu. Msomi huyu anatoka katika familia yenye kipato kidogo, awali alikuwa amekata tamaa kabisa ya kupata elimu ya juu kutokana na gharama za elimu ya chuo kikuu.

Na alikuwa na shauku kubwa ya kupata elimu ya juu, ndipo alipoamua kuweka tangazo katika mitandao ya kijamii akisema anauza figo ili aweze kupata fedha za kumwezesha kusoma chuo kikuu. Taasisi ya Mo Dewji imesikia kilio chake wala haijataka figo, imemwezesha kutimiza ndoto za kijana huyu kwa kumpa ufadhili wa masomo. Ntandu anasema:

"Nilikuwa tayari kuweka maisha yangu hatarini kwa kutangaza kuuza figo yangu, lakini ufadhili huu mliotupatia umebadili maisha yetu. Idadi ya wanafunzi wanaokosa mikopo ni kubwa hivyo nawaomba muwe na moyo wa kuendelea kuwasaidia ili na wao wafikie azma ya kusoma".

Ni kweli wapo vijana wengi nchini ambao walikuwa wamekata tamaa ya kufika elimu ya juu lakini kupitia Mo Dewji, ndoto zao zimekuwa halisi kwa kulipiwa ada na fedha nyingine za kujikimu.

Mo Dewji anasema alianzisha mpango wa kutoa ufadhili kwa wanafunzi wa elimu ya juu ili kuunga mkono juhudi za Rais John Magufuli za kuwezesha vijana kupata elimu na kutoa mchango katika gurudumu la maendeleo ya nchi.

Serikali bado haijawa na uwezo wa kutoa mikopo kwa wanafunzi wote wa elimu ya juu. Hivyo baadhi ya wanafunzi hujikuta wakikosa mikopo, hali inayofifisha ndoto zao za kupata elimu.

Kinachofanywa na Taasisi ya Mo Dewji katika kutoa ufadhili si tu kuunga mkono jitihada za serikali bali pia ni kuwasaidia vijana kutoka familia maskini lakini wenye uwezo mkubwa wa kitaaluma kufikia malengo yao.

Katika uzinduzi wa mpango huu mnamo Septemba 7, 2016, Mkuu wa Taasisi ya Mo Dewji, Barbara Gonzalez, anasema "Tumeanza na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, hapo baadae tutatanua mikono yetu kwenda vyuo mbalimbali". Kwa neno hilo ni wazi kuwa Taasisi ya Mo Dewj imeanza, wengine wafuate nyayo au waunge mkono kuwasaidia vijana wa Tanzania kusoma.

***Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko Wilaya ya Kongwa, Jijini Dodoma.***

***Maoni: 0764-666349.***

# 'Kimbilio Letu' inavyotekeleza mapendekezo SADC kwa vitendo



Baadhi ya wajasiriamali wa mtandao wa Kimbilio Letu, wakielekezana namna ya kutengeneza sehemu ya bidhaa wanazozizalisha, walipokutana jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki iliyopita. **PICHA: MASHAKA MGETA**

**Na Mashaka Mgeta**

MIONGONI mwa hoja kubwa zilizojitokeza wakati wa mkutano wa marais na wakuu wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) uliofanyika hivi karibuni jijini Dar es Salaam ni kuchagiza soko la bidhaa ndani ya ukanda huo.

Marais na wakuu wa nchi za SADC wanaamini kuwa ukubwa wa idadi ya watu wanaokadiriwa kuwa milioni 650, kama ukitumika katika ununuzi na uuzaji wa bidhaa, ni wazi kwamba itachangia kuboresha biashara, kukuza kipato na kustawisha maisha ya watu.

Ingawa hoja hiyo imekuwa ikijirudia kwenye mikutano mingi ya SADC, kama ilivyo kwa mikutano ya jumuiya nyingine za kikanda, lakini umuhimu wake bado upo na unapata nguvu zaidi hasa wakati huu ambapo Tanzania inashikilia' uenyekiti.

Mwanaharakati wa masuala ya uchumi na biashara, Veneranda Nguvumali, anasema kushirikishana katika soko la ukanda wa SADC kutakuwa na maana ikiwa nchi wanachama zitachagiza hali hiyo ndani ya jamii zao.

"Kuboresha mazingira ya biashara ili kukuza soko la bidhaa ni hulka inayopaswa kujengwa kuanzia ngazi ya nchi moja moja ndipo itaenea vizuri katika ushirikiano wa kikanda," anasema.

> **Mpango huu umeshaanza kutekelezwa na wajasiriamali wameshaanza kunufaika kwa ongezeko la mauzo tofauti na jinsi walivyokuwa awali.**

Ni kutokana na hali hiyo, baadhi ya Watanzania wameshaanza kujipanga ili kuweka rekodi ya kuwa sehemu ya utekelezaji wa azma ya kuimarisha masoko ya SADC, ikiwa ni pamoja na kuanzia ndani ya nchi.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, wajasiriamali wadogo waliokadiriwa kuwa 300 walikutana jijini Dar es Salaam kubadilishana mawazo na kujenga mtandao thabiti utakaotoa fursa ya soko la bidhaa wanazozitengeneza.

Wajasiriamali hao wanatoka katika nyanja tofauti za uzalishaji bidhaa na huduma zinazotakiwa kwa matumizi ya binadamu.

Wakikutanishwa na taasisi ya Kimbilio Letu In Pair International, wajasiriamali wakaelezea namna wanavyokusudia kuongeza idadi yao kufikia angalau 400,00 nchi nzima, ili kuwa na soko kubwa kati yao na kutoka nje ya mtandao huo.

Meneja wa sera na mipango wa taasisi hiyo, Charles Wilbad, anasema kupitia kauli mbiu ya 'Mimi na Tanzania kuelekea uchumi wa kati', wajasiriamali hao wamekubaliana kuwa umoja huo utumike kama kituo cha habari na soko la kuuziana bidhaa wanazozizalisha.

"Mpango huu umeshaanza kutekelezwa na wajasiriamali wameshaanza kunufaika kwa ongezeko la mauzo tofauti na jinsi walivyokuwa awali," anasema.

Kwa mujibu wa Wilbad, wajasiriamali hao wanajishughulisha na usindikaji wa vyakula na vinywaji, mazao ya kilimo, uvuvi na bidhaa nyingine zinazohitajika kwa matumizi ya binadamu.

Bila shaka hatua hiyo inapaswa kuungwa mkono hasa kwa vile inaonyesha kwa vitendo namna bora ya kubuni na kutekeleza kuliko kuzungumza pasipokuwa na vitendo.

Utekelezaji wa vitendo unaolenga kuboresha mazingira ya wajasiriamali kupitia mtandao huo, unachangia sababu zilizomvutia mkulima wa uyoga kutoka Kibamba jijini Dar es Salaam, Henry Mwizanduru kujiunga, akitegemea kukuza soko la zao hilo na hivyo kuongeza kipato kinachoweza kumuingiza katika umiliki wa kiwanda kidogo.

Mwizanduru anawakilisha taasisi ya Green Preservers Tanzania, anasema uzalishaji uyoga una manufaa zaidi ya kiuchumi ikiwa utapata soko la uhakika, hivyo idadi ya watu wanaokadiriwa kuanzia 400,000 watakapofikia, atakuwa na uhakika kwa taasisi yake kuongeza uzalishaji na kupata kipato zaidi.

Anasema kwa kadri ya maelezo ya wataalamu, uyoga wa kisasa unaozalishwa kwenye eneo la ukubwa wa mita tano kwa sita, ni sawa na matumizi ya mashamba 2000 yanayoweza kuzalisha kiasi cha tani 4 za zao hilo kwa uvunaji unaofanyika kila baada ya miezi mitatu.

Kuanzishwa kwa mtandao huo hakutoi manufaa ya soko pekee, bali pia fursa ya kueneza ujuzi, teknolojia na kuunganisha nguvu ya uzalishaji bidhaa ili kufikia uwezo wa kuuza nje ya nchi.

Salome Ukasoni ni mmoja wa wanachama wa mtandao huo, anayezalisha bidhaa zinazotengenezwa kwa kutumia shanga.

Kwa mujibu wa Salome, nia nzuri ya kujihusisha katika ujasiriamali mdogo inaathiriwa kwa kiasi kikubwa na ukosefu wa masoko na mitaji.

Anatoa mfano kuwa wakati akianza kujihusisha na biashara hiyo, uwezo wake ulikuwa kutengeneza vikapu visivyozidi 10 , lakini tangu ajiunge kwenye mtandao huo takribani miezi mitano iliyopita, anaziona dalili za kuwapo fursa kubwa ya kuongeza uzalishaji.

Salome, anasema pamoja na manufaa ya kupata soko zaidi ya lile alilokuwa nalo awali ambapo aliuza bidhaa zake wilayani Masasi katika Mkoa wa Mtwara pekee, lakini pia hivi sasa anawafundisha wengine namna ya utengenezaji bidhaa hizo na hivyo kupata kipato zaidi.

"Ninapowafundisha wananilipa hela, lakini idadi yetu inapoongezeka ni wazi kwamba tutakuwa na uwezo mkubwa wa kuweka na kusafirisha pamoja bidhaa kwenda kuuza nje ya nchi," anasema.

Kutokana na hali hiyo, Salome anautazama mtandao huo kama sehemu muhimu inayopaswa kukuzwa na kuendelezwa, ili wajasiriamali waweza kupata soko la uhakika nap engine kuunganisha mitaji yao hasa katika kulifikia masoko ya kikanda na kimataifa.

Hatua hizo ambazo ni sehemu ya maelezo marefu ya mtandao huo na mipango mikakati yao, lakini angalau wameonyesha kwa vitendo ni namna gani watu wanaunganishwa kwa malengo yanayofanana, wanavyoweza kubuni namna bora ya kuwa sehemu ya soko la bidhaa wanazozizalisha.

Kuanza utekelezaji wa dhana hii katika ngazi ya chini kwenye jamii, kunaweza kuwa mfano wa kwa watu wengine kutoka ndani na nje ya nchi kujifunza, ili hatimaye muundo wake uchangie kuchagiza ushiriki wa wananchi katika masoko ya kikanda.

*Mawasiliano: 0754691540*

MAKALA



Wananchi wa Shehia ya Makangale , wilayani Micheweni, wakimsikiliza Mkuu wa Idara ya Wanawake na Watoto Pemba (hayupo picha-ni), Mwanaisha Ali Massoud, wakati akitoa elimu ya udhalilishaji ndani ya shehia hiyo. **PICHA: MWANDISHI WETU**

# Zanzibar inavyopambana na utelekezaji wa familia

**Na Theodatus Muchunguzi**

MATUKIO ya wanaume kuzitelekeza familia zao yameshika kasi visiwani Zanzibar, hali iliyozishitua mamlaka mbalimbali kuanzisha mapambano kukabiliana na tatizo hilo kubwa ambalo linatajwa kuwa chanzo cha ukatili wa kijinsia.

Unyanyasaji huo unawaathiri zaidi watoto wadogo hususan chini ya miaka 18 kutokana na kubakia chini ya mzazi mmoja, ambaye ni mama.

Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Wete, Pemba inalizungumzia tatizo hili kubwa katika jamii kupitia kwa Ofisa Maendeleo ya Jamii wilayani huyo, Haroub Suleman Hemed, kwa kusema:

"Hili ni tatizo la muda mrefu hapa. Kesi nyingi za matukio ya ukatili wa kijinsia ni zinazohusiana na utelekezaji na familia kusambaratika."

Hemed, ambaye amekuwa akifanya kazi katika ofisi hiyo ambayo ndiyo yenye dhamana ya kushughulikia masuala mbali mbali ya kijamii kwa miaka takribani zaidi ya 20, alibainisha hayo hivi karibuni alipozunguma na wanahabari kutoka Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA-Zanzibar) na kueleza:

"Aina nyingine za ukatili wa kijinsia zinapungua kutokana na hatua kadhaa zinazoendelea kuchukuliwa, lakini utelekezaji wa watoto na familia unaendelea, na huu unachangiwa na mambo mbalimbali, ikiwamo ndoa za utotoni na utamaduni wa zaidi ya ndoa moja."

Kwa mujibu wa Afisa huyo, umaskini ni miongoni mwa sababu kubwa zinazochangia utelekezaji wa watoto na familia , ambapo huzikimbia familia zao kwenda kutafuta kazi na fursa za biashara nje ya kisiwa cha Pemba-ambacho ni mashuhuri kwa kuwa na mazIngira mazuri kwa uvuvi.

'Hata hivyo, kuna watu ambao wanasita kuzitunza familia zao," anasema Hemed na kuongeza kuwa:

"Kama serikali, tunahangaika kuchukua hatua kukabiliana na changamoto hii kupitia mikutano na semina za mara kwa mara na viongozi wa ngazi za chini ili matukio ya utelekezaji yawe na athari chanya.'

Mratibu wa Tamwa Zanzibar, ofisi za Pemba, Fathiya Mussa Said, kwa upande wake anauelezea utelekezaji kuwa ni moja ya matukio ya ukatili wa kijinsia yanayoongoza katika kisiwa hicho, na kufafanua zaidi kuwa kuna matukio kadhaa ya wanaume kutelekeza familia na wake zao, hali ambayo mwishowe huchochea ongezeko la matukio ya ukatili wa kijinsia.

Akitolea mfano, Fathiya anasema katika eneo la Ole Mjini , kilomita chache kutoka Chakechake ambayo ni makao makuu ya Mkoa Kusini Pemba, mwanaume mmoja alitelekeza mke na watoto wawili moja kwa moja.

Licha ya kuripoti tukio hilo Mahakama ya Kadhi na kumwamuru baba kutoa matunzo kwa familia lakini utekelezaji wa hukumu hiyo ulishindikana," anasema Fatiya na kuongeza:

" Hali ni mbaya na wanamke na watoto wanaendelea kuathiriwa na umaskini, kutokana na mtu waliyemtegemea kuikimbia familia zaidi ya miaka miwili."

Mwanamke huyo Fatma Issa (26), anasema kuwa alitekelezwa na mumewe na kuondoka nyumbani hapo zaidi ya takribani miaka miwili na kumuacha na watoto wadogo wawili wa kiume kabla ya kuolewa na mwanaume mwingine.

Hata hivyo, jitihada za Tamwa kuibua na kufuatilia matukio ya ukatili wa kijinsia kumemwezesha mtoto wake mkubwa kuandikishwa na kuanza masomo ya darasa la kwanza katika Shule ya Msingo Ole mwishoni mwa Julai 390, mwaka huu, baada ya kuwezeshwa na Tamwa Zanzibar ofisi za Pemba kwa kumpatia mahitaji mbalimbali muhimu ya shule.

Fathiya anasema pia kwamba katika eneo la Selem wilauani Wete, (wazazi (baba na mama) waliiacha familia ya watoto watano ambapo baba alioa mke mwingine na mama kuolewa na mwanaume mwingine, hivyo kuwaacha watoto watano katika machungu.

Mratibu huyo anakielezea kitendo hicho kuwa ni kuwaweka watoto hao wakiwamo wasichana katika wakati ngumu kwa kuwa hawana pa kupata mahitaji yao muhimu.

"Jukumu letu ni kuhakikisha kuwa sauti ya wasiosikika inafika katika maeneo kadhaa, waathirika wanasaidiwa na wasamaria wema. Kwa mfano, kwa kuripotiwa kwa tukio la watoto watano walitekelezwa, baadhi ya wasamaria wema waliwasaidia kwa kuifanyia ukarabati nyumba wanayoishi," anasema mratibu huyo.

Kwa upande wake, Asha Mussa Omar, Ofisa Mpango wa Tamwa-Pemba, anaeleza kuwa licha ya vyombo vya habari kuripoti matukio ya ukatili wa kijinsia, utekelezaji umeendelea kuwa mwiba kwa wapambanaji dhidi ya matukio ya ukatili kisiwani Pemba.

Utafiti iliofanywa ma Tamwa-Zanzibar hivi karibuni ambao uliitwa "Ripoti ya ushirikishaji wa marafiki wachanga wa vyombo vya habari (YMF), ulitaja utelekezaji wa watoto au familia kuwa ni tatizo sugu Zanzibar linalochangia ukatili wa kijinsia hususan watoto chini ya miaka 18 ambao hulazimika kubakia chini ya mzazi mmoja au kuhamishiwa kupata malezi kwa jamaa wa karibu, hali ambayo katika matukio mengi hupuuzwa katika malezi.

Utafiti huo wa tathmini kuhusu hali ya ukatili wa kijinsia Zanzibar ulifanyika katika wilaya mbili za Kaskazini Unguja na Mkoani Pemba.

Lengo la utafiti huo lilikuwa ni kuwafanyia ushawishi vyombo vya habari kudhihirisha mchango wake muhimu wa kutokomeza udhalilishaji wa kijinsia kupitia mkakati wa utetezi na kuingilia kati kwa ajili ya kuboresha yaliyomo pamoja na kujielekeza katika mambo kadhaa kuhusiana na ukatili wa kijinsia pamoja na kuwahimiza wadau wengine serikalini na asasi binafsi kushiriki kwa dhati katika utokomezaji wa ukatili wa kijinsia kupitia vyombo vya habari.

Utafiti huo ni sehemu ya Mpango wa Taifa wa Zanzibar kutokomeza ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto (NPA-VAWC) wa 2017-2022, wenye dhamira ya kutokomeza aina zote za ukatili dhidi ya makundi hayo.

Wadau kadhaa wanaona kuwa kuna mambo kadhaa ya kufanya katika kupunguza tatizo hilo kama si kulitokomeza kabisa.

Kwa mfano Hemed anasema kuwa Mahakama ya Kadhi inahitaji kupewa mamlaka zaidi ili kuwapa kibano wahusika kwa sababu kwa sasa kinashughulikia masuala hayo kwa kutumia busara bila kuwa na nguvu za kisheria.

Anasema kutokuwa na nguvu za kisheria kunasababisha wahusika wengi wanapoitwa kwenye mashauri hususan ya kutelekeza familia wanaweza kwenda au wasiende na kwamba hata unapotolewa uamuzi wa kuwabana kutoa matunzo, wanaweza kutekeleza ama la.

Kimsingi, utelekezaji wa familia kisiwani Pemba unaofanywa na wanaume wengi kwa ni kilio kwa familia nyingi. Kisingizio ni hali ngumu ya maisha na kwamba wanakwenda kutafuta maisha.

Mwishowe wanawake wanajikuta wakizidiwa na mzigo wa kutunza familia na kuamua kuondoka na kuolewa pengine au kwenda makwao, hivyo watoto kukosa malezi na matunzo zikiwamo huduma za msingi kama elimu.

Kwa hali hii, watoto wanaishia kuzurura au kutunzwa na ndugu na jamaa bila kuwapa malezi mema ya kujitegemea.

Kinachotakiwa ni ushirikiano wa wadau, serikali, washirika wa maendeleo na vyombo vya habari kuendelea kuchukua hatua mbalimbali kuhakikisha jamii inabadilika na kuacha vitendo hivyo.

# Wanavijiji 80,000 Mugango kunywa maji ya Ziwa Victoria



Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Profesa Kitila Mkumbo (kulia waliokaa), akisaini mkataba na mmoja wa wawakilishi wa kampuni inayojenga mradi wa bomba kubwa la maji kutoka Mugango, Musoma Vijijini, kupitia Kiabakari hadi Butiama, huku akishuhudiwa na viongozi mbalimbali akiwamo Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adam Malima. **PICHA: MTANDAO**

**Na Sabato Kasika**

SERIKALI imepanga kumfikishia kila Mtanzania maji safi na salama bila kujali eneo analoishi. Mpango huo unawafikia walioko vijijini kwa kuwapa huduma hiyo kwa asilimia 85.

Ikimaanisha kuwa kwa kila watu 100 wanaoishi vijijini takribani wananchi 85 watakuwa wanapata maji ya bomba kwa namna yeyote ile na kwa gharama nafuu.

Kwa wakazi wa mijini asilimia 95 itakuwa inapata huduma hiyo, kwa tafsiri hiyo ni kama kila mtu anayeishi mjini atapata huduma ya maji safi na salama.

Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Profesa Makama Mbarawa, anasema serikali inataka kuwafikishia maji kwa asilimia 95 walioko mijini na asilimia 85 wakazi wa vijijini.

Kutokana na uamuzi huo wa serikali, miradi mbalimbali ya maji inaendelea kutekelezwa na mingine kusainiwa kwa ajili ya utekelezaji ili wananchi waweze kunufaika na huduma hiyo muhimu.

Mradi wa bomba la maji safi na salama kutoka ziwa Victoria eneo la Mugango, Musoma Vijijini kupitia Kiabakari hadi wilayani Butiama mkoani Mara ni miongoni mwa miradi hiyo inayotekelezwa kutimiza azma hiyo.

Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (BADEA) na Mfuko wa Maendeleo wa Saudia (SFD) zimeingia mkataba wa utekelezaji wa mradi huo.

Ujenzi wa huduma hiyo unaogharimu Sh. bilioni 70, unatarajia kuanza wakati wowote baada ya mkataba kutiwa saini tangu Agosti mwaka huu kazi iliyofanyika Nyamisisi wilayani Butiama.

Serikali iliwakilishwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Profesa Kitila Mkumbo, huku Mkoa uliongozwa na Mkuu wa Mkoa, Adam Malima, kwenye hafla hiyo ya utiaji saini.

Wengine wanaoshuhudia tukio hilo lililofanyika Agosti 15 mwaka huu ni wakuu wa wilaya za Musoma na Butiama, wakurugenzi wa halmashauri za wilaya hizo.

Mbali na hao walikuwapo pia wabunge Profesa Sospeter Muhongo (Musoma Vijijini), Agnes Marwa na Amina Makilagi (viti maalum), madiwani na viongozi wa chama na serikali.

Dokta Vincent Anney, ni Mkuu wa Wilaya ya Musoma, ambako bomba hilo linaanzia kwenye Kijiji cha Kwibara kilichoko kata ya Mugango, kuelekea maeneo mengine.

### WATAKAONUFAIKA

Anney anasema mbali na wakazi wa kata ya Mugango, ambako bomba hilo linaanzia, wananchi wengine 80,000 waliopo kwenye vijiji 13 eneo ambalo bomba hilo litapita, wanatarajia kunufaika na mradi huo.

Mkuu huyo wa wilaya anasema mradi huo mkongwe ni wa siku nyingi tangu mwaka 1974 na kwamba serikali imetenga Sh. bilioni 8.5 ili wakazi Musoma Vijijini na wa Butiama wanufaike na huduma hiyo muhimu.

Dokta Anney anasema, mradi huo unatarajia kukamilika ndani ya miezi 24 na kwamba mbali na huo, kuna mingine inayoendelea wilayani mwake na hasa kwenye wilaya ya Musoma Vijijini.

"Kuna mradi wa maziwa makuu, ambao vijiji vyote 33 vya Musoma Vijijini vilivyoko karibu na Ziwa Victoria vimo kwenye mradi huo na usanifu umeshafanyika," anasema Mkuu wa Wilaya.

Anasema serikali inajipanga kwa utekelezaji na pia maji yanayozalishwa na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Musoma (Muwasa), kwa ajili ya Mji wa Musoma ni mengi ikiwa ni takriban asilimia 50 ya maji yanayozalishwa, hivyo yatasambazwa vijijini.

Anasema mradi huo ni wa kipekee kwa kuwa maji yanayozalishwa yana uwezo wa kuchotwa na kunywewa kutoka bombani bila ya kuchemshwa kutokana na kuchujwa na kuwekwa dawa ya kutosha ya kutibu maji.

"Serikali imeamua vijijini vya Musoma Vijijini na Butiama visambaziwe maji hayo ya ziada, ambapo vijiji vya Musoma Vijijini ni vya kata za Etaro, Nyegina, Nyakatende na Ifulifu," anasema.

Anasema utekelezaji wa mradi huo umeanza na pia anataja mingine inayotekelezwa kuwa ni ya vijiji vya Bujaga, Bulinga, Bukima, Kwikerege, Chitare, Makojo, Suguti, Kusenyi, Chirorwe hadi Wanyere.

"Tangi lenye uwezo wa kuchukua lita 225,000, limejengwa kijiji cha Bujaga, vituo 18 vya kuchotea maji, vioski viwili vya kuuzia maji, birika la kunyweshea mifugo na utandazaji wa mabomba ya kusambazia maji," anasema Anney.

Mkuu huyo wa wilaya anasema serikali imedhamiria kumaliza tatizo la ukosefu wa maji safi na salama, na kuwataka wananchi waendelee kuiunga mkono kwa kazi ambazo inafanya kwa ajili yao.

Anafafanua kuwa kuna miradi mingine ambayo usanifu wake umekamilika ambayo ni ya vijiji vya kata za Bugoji, Nyambono, Bugwema, Musanja na Nyamrandirira, na kwamba maombi ya fedha za utekelezaji wa usambazaji wa maji yamefikishwa kwenye serikali kuu.

### WANANCHI

Kwa niaba ya wananchi wa vijiji 68 vya Musoma Vijijini, mbunge wao Profesa Sospeter Muhongo, anatoa shukrani za dhati kwa Serikali yao kwa kuanza kutekeleza miradi ya usambazaji maji safi na salama vijijini mwao.

"Shukrani maalum ni kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, kwa kuanza kutimiza ahadi yake ya kutekeleza mradi wa ujenzi wa bomba la maji la Mugango-Kiabakari-Butiama," Prof. Muhongo anasema.

Anasema wananchi wa Musoma Vijijini sasa wanakaribia kuondokana na changamoto ya ukosefu wa maji safi na salama, ambayo wamekuwa wakikabiliana nayo kwa muda mrefu.

"Wananchi hutembea umbali mrefu kufuata huduma ya maji pembezoni mwa ziwa Victoria na wengine walio mbali na ziwa hulazimika kuyatafuta kwenye visima vya kienyeji, lakini sasa wataondokana na hali hiyo," anasema.

Mbunge huyo anasema kilio cha wananchi kimewafikia viongozi wa serikali moja kwa moja, na sasa miradi ya maji inatekelezwa ili kuwaondolea changamoto hiyo ya ukosefu wa maji.


"Kwa mfano vijiji vyote 33 vya Musoma Vijijini vilivyoko karibu na ziwa Victoria kuwekwa kwenye mradi wa maziwa makuu ni hatua nzuri sana ndio maana wananchi wanatoa shukrani kwa serikali yao," anasema.

Prof. Muhongo anasema jimbo lake lina jumla ya vijiji 68, na kwamba 33 kati hivyo viko kwenye mradi huo wa maziwa makuu na vilivyosalia vinaendelea kufanyiwa mchakato wa kupata huduma ya maji safi na salama.

HABARI KIMATAIFA

# BURIANI MUGABE

## Afia Singapore, kilichomuua chabaki siri



**HARARE, ZIMBABWE**

RAIS wa zamani wa Zimbabwe, Robert Mugabe, amefariki dunia akiwa anatibiwa nchini Singapore.

Mugabe muasisi na Baba wa Taifa la Zimbabwe, alifariki dunia jana akiwa na katika hospitali ya Singapore alikokuwa amelazwa kwa miezi mitano.

Robert Mugabe (95), aliitawala Zimbabwe tangu uhuru wa nchi hiyo mwaka 1980, alilazimika kujiuzulu Novemba 2017 kwa shinikizo la jeshi na chama chake, ZANU-PF na nafasi yake kuchukuliwa na Makamu wa Rais, Emmerson Mnangagwa, aliyechaguliwa tena kama rais wa Zimbabwe Julai 2018.

"Ni kwa huzuni mkubwa ninatangaza kifo cha Baba wa Taifa na Mwasisi wa uhuru wa Zimbabwe na rais wa zamani, Kamanda Robert Mugabe," Rais wa sasa wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa, aliandika ujumbe kwenye ukurasa wake wa twitter.

Aidha, mmoja wa wanafamilia aliithibitishia BBC kuwa, Robert Mugabe, alifariki dunia. "Kamanda Mugabe alikuwa ni mwanga wa mapinduzi, mwana umajumui (pan Africanism) wa Afrika ambaye aliyatoa maisha yake katika ukombozi na kuwawezesha watu wake. Mchango wake kwa taifa letu na bara la Afrika hautasahaulika..." aliandika Mnangagwa.

Ujumbe mwingine: "Nimepokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kifo cha Rais Mstaafu na Baba wa Taifa la Zimbabwe Mzee Robert Mugabe. Afrika imepoteza mmoja wa viongozi jasiri, shupavu, mwanamajumui wa Afrika na aliyekataa ukoloni kwa vitendo. Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, Amina," aliandika Rais John Magufuli kupitia ukurasa wake wa twitter.

Naye Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta, alituma salamu za rambirambi akisema hana maneno ya kutosha kuelezea uzito wa kuachwa na kiongozi shupavu, shujaa na mzalendo wa Afrika ambaye alitekeleza jukumu muhimu katika kutetea maslahi ya bara la Afrika.

Kwa wakati huu wa majonzi, mawazo na maombi yangu ni kwa jamaa, ndugu na watu wa Zimbabwe ambao kwa miaka mingi aliwatumikia kwa kujitolea na kwa bidii... Bila shaka, tutamkumbuka Rais huyo wa zamani Robert Mugabe kama mtu jasiri ambaye kamwe hakuogopa kuelezea msimamo wake kwa jambo lolote hata kama wengi hawakumuunga mkono.

Kwa familia yake, serikali na raia wa Zimbabwe, Mola awafariji na ailaze roho ya Rais wa zamani Robert Mugabe mahala pema peponi," alieeleza Mugabe.

**UGONJWA WABAKI SIRI**

"Mugabe alikuwa alama ya ukombozi. Mpigania uhuru wa Afrika aliyejitolea maisha yake kwa ajili ya kuwainua watu. Mchango wake kwa Taifa hili na Bara hili hautasahaulika. Roho yake ipumzike kwa amani," aliongeza Mnangagwa.

Mugabe alikuwa anasumbuliwa na maradhi ambayo hayakuwahi kuwekwa wazi. Alikuwa akipatiwa matibabu nchini Singapore mara kadhaa, lakini alipatiwa matibabu mfululizo nchini humo tangu Aprili mwaka huu.

Hata hivyo Rais Emmerson Mnangagwa bila kusema zaidi, alibainisha kwamba Mugabe alikuwa anasumbuliwa na maradhi lakini pia ni pamoja na uzee.

HISTORIA YAKE

Mugabe alizaliwa Februari 21, 1924 na wakati huo nchi yake iliitwa Rhodesia. Alitupwa jela kwa miaka 10 bila ya kufunguliwa mashtaka kwa kuukosoa uongozi wa Rhodesia mwaka 1964.

Mwaka 1973, akiwa gerezani alichaguliwa kuwa Rais wa Chama cha Zimbabwe African Union (Zanu), ambacho alikuwa ni mwanachama mwanzilishi.

Baada ya kuachiwa kutoka gerezani, alikimbilia Msumbiji na kuongoza mapambano ya kijeshi ya kudai uhuru. Licha ya kuwa mpiganaji wa vita vya kushtukiza (guerrilla), alisifika kwa kuwa makini na mahiri kwenye majadiliano.

Mwaka 1980 alifanikisha kupatikana uhuru wa Zimbabwe na kuingia madarakani baada ya uchaguzi uliomaliza utawala wa walowezi wachache wa Kizungu.

**WANAOMKOSOA**

Hata baada ya kifo chake, maoni yaliyotolewa kumhusu Robert Mugabe alipokuwa hai, hayajabadilika. Wazimbabwe wanamkumbuka kuhusu ni nini alichowaachia kiongozi huyo aliyeiongoza Zimbabwe kwa miaka 37.

Wakitumia 'kaulimbiu RIP Mugabe' ama #LALA salama' baadhi wanamsifu kama shujaa, mtetezi wa hali ya watu weusi, huku wengine wakisema alikuwa mkombozi aliyegeuka kuwa mkandamizaji . Mwanaharakati na mkosoaji wa serikali ya chama cha Zanu-PF , Fadzayi Mahere, anatafakari maoni tofauti kuhusu namna Mugabe atakavyokumbukwa kwenye ujumbe wa twitter uliolenga namna Mugabe atakavyokumbukwa kwa uchumi wake ambao uliathiri kila sekta ya maisha, hususan huduma za matibabu

Japo Mugabe anayeitwa mpigania haki za Waafrika aliyekuwa mstari wa mbele kutetea mara kwa mara amekuwa akipata matibabu nchini Singapore na amefariki katika nchi ya kigeni ni kitu ambacho hakitasahaulika miongoni mwa wengi.

Baadhi ya Wazimbabwe pia wanatafakari juu ya ahadi nyingi nzuri za mwaka 1980 alipokuwa Waziri Mkuu wa kwanza.

**BBC**

# Mwenye miaka 73 ajifungua mapacha

**ANDHRA PRADESH, INDIA**

MAMA mwenye umri wa miaka 73 katika jimbo la kusini mwa India la Andhra Pradesh, amejifungua watoto wawili mapacha wa kike.

Wazazi waliomsaidia kujifungua mapacha hao walisema amejifungua kwa njia ya kuanguliwa mayai ya uzazi nje ya mfuko wa uzazi na baadaye kuchanganywa na mbegu za kiume na kisha kupandikizwa kwenye kizazi kwa njia ya IVF kitaalamu. "Mama na watoto kwa pamoja wanaendelea vizuri,"Dk. Uma Sankar aliimbia BBC.

Mangayamma Yaramati, alisema yeye na mumewe ambaye ana umri wa miaka 82, wamekuwa wakati wote wakitaka kuwa na watoto lakini hawakuwahi kujaliwa.

"Tumefurahi sana ,"alisema mume wake, Sitarama Rajarao, akiongeza kuwa mkewe alipata ujauzito katika kipindi cha miezi miwili tu baada ya kufanyiwa matibabu ya IVF.

"Tulijaribu mara nyingi kupata watoto na tukawatembelea madaktari wengi ," Alisema Yaramati , "kwa hiyo hiki ni kipindi cha furaha zaidi maishani mwangu

Aliongeza kuwa alihisi kutengwa na jamii na wanakijiji wenzake na mara kwa mara amekuwa akitengwa katika mikusanyiko kwasababu hakuwa mama.

Alisema :"Walikuwa wananiita mwanamke asiye na mtoto ,"

Lakini siku ambayo watoto wake mapacha walipozaliwa, Rajarao alipata kiharusi. Kwa sasa anapokea matibabu hospitalini.

Mapacha hao wasichana walizaliwa kwa njia ya upasuaji , jambo ambalo ni la kawaida kwa uzazi huo wa nadra.

**BBC**

# HADITHI

## Jumba Jekundi-17

WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawahitajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.
Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina.
Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.




**Na Adam Fungamwango**

**(0716 350534)**

USO wake angavu ulionyesha kabisa kuwa ni mwanamke mwenye madaraka au pesa. Wala haihitaji elimu ya chuo kikuu kujua kuwa ndiye mmiliki wa jumba na vitu vyote mle, au mke wa mwenye mali.

Kama ilivyotegemewa, alikaa kwenye kiti cha enzi na kuinamisha kichwa kidogo kama kushukuru, akainua.

Akaangalia pembeni kushoto na kulia kama kuihabarisha hadhira kuwa tayari ameshachukua nafasi yake.

Akaangalia mbele na uso wake ukamuelekezea moja kwa moja Kadili. Kwa aibu Kadili akaangalia chini.

Hadi wakati huo alikuwa hajabadilisha nguo. Ilishaloa na kukauka mara mbili. Kwa mbali alisikia harufu ya jasho lake na nguo zake mwenyewe kutokana na kukaa masaa zaidi ya 24 bila kubadilisha wala kuoga.

Akakunja sura na kutikisa kichwa kwa namna ya dharau. "Ndiyo haka kajitu kenyewe kanakotusumbua?"

"Ndiyo mkuu." Alijibu mmoja wa watu wake waliokuwa wanamsikiliza.

"Wewe kinyago, eti ndiyo unataka kumuoa Edina?" Swali hilo la dharau si tu lilimkwaza Kadili kutokana na kuangaliwa kwa dharau na kila mtu humo ndani, lakini pia lilimshangaza kwa sababu ni jipya kichwani kwake.

Hakuwaza, wala kumwambia hata siku moja Edina kuwa anataka kumuoa. Hajawahi kuwa na hata uhusiano wa kimapenzi na msichana huyo zaidi ya kucheza naye muziki tu.

Kadili sasa alionekana kujutia kitendo chake cha kukubali kucheza muziki na msichana huyo, kwani yote yanayomkuta kwa sasa ni sababu hiyo tu.

"Hapana, si kweli." Alijibu kama vile yuko mahakamani akikanusha tuhuma anazikabiliwa nazo.

"We Edina, njoo huku, mchumba 'ako kaja kutoa barua ya uchumba, njoo ushuhudie tafrija bibi harusi mtarajiwa."

Ilikuwa ni sauti ya mwanamke hiyo iliyojaa mzaha, kejeli, nyodo na dharau.

Mlango ulifunguliwa. Aliyetoka humo hakuna mgeni machoni mwa Kadili. Ni Edina. Hakuna amejipamba kama alivyokuwa akikutana naye Bluu Star.

Alivaa gauni mmoja fupi kiasi cha kuonyesha mapaja yake laini wazi. Alikuwa ameshikwa mkono na mmoja wa mabaunsa ambaye aliyeonekana kumtoa huko alikokuwa.

**"Binti yangu bado mdogo, halafu kifaa cha nguvu. Si unamuona? Huyu si msichana wa kuolewa na mtu kapuku kama wewe. Kula yako na vaa yako shida huyu unamuweza wewe? Hapa unaponiona, kichwa kinaniuma, maana wanaume kibao wenye wadhifa na pesa zao wametuma washenga kutaka kumuoa binti yangu, yaani sijui nimkubali nani nimuache nani. Halafu kanatoke kajitu kama wewe nako, eti nako kanajitia kutaka kupimana ubavu na watu hao," Alisema na kuonekana kama kuutua mzigo mzito uliokuwa kwenye kifua chake.**

Sura yake haikuwa na tabasamu. Naye kama ilivyo Kadili hakuwa akimuangalia mtu yoyote ndani. Ni mtu pekee ambaye hakutaka kukaa kwenye kitu, bali aliamua kukaa chini, huku akionekana amenuna kupita kiasi.

Kadili alionekana kama kuanza kumchukia Edina, kwani yote haya yanayompata ni kwa ajili yake.

Kikubwa zaidi si kucheza naye, bali hizi habari zilizoenea ndani ya jumba jekundu kuwa Edina ni mpenzi wake ni nani aliyezipeleka?

Moja kwa moja akili yake ikamtuma kuwa Edina ndiye aliyezipeleka, ingawa hajui kama alizipeleka kwa hiari yake au alilazimishwa kwa kupewa kibano.

"Haya mchumba 'ako huyo hapo, nataka nikuoze mkaishi naye huko Kwandale."

Kukatokea vicheko vya hapa na pale kutoka kwa wahudhuriaji kutokana na maneno yake ya mwanamke huyo.

"Mama siyo Kwandale ni Tandale." Baunsa mmoja alimsahihisha tajiri yake.

"Ndiyo huko huko tena, mimi siwezi kupata tabu ya kutaka kujua sehemu kama hizo za kishamba uswahilini huko." Alijibu baada ya kusahihishwa.

Kukatokea kimya cha nusu dakika ndani ya jumba lile. Mama aliyekaa kwenye kiti cha enzi alionekana kutafakari. Aliangaza huku na huko, huku wafuasi wake wakiwa kimya kabisa.

"Sikiliza we mtoto wa mbwa." Sauti yake sasa ilibadilika. Si ile ya kejeli na dharau tena. Ilijaa msisitizo, mamlaka, hasira na isiyo na mzaha hata chembe.

"Mimi naitwa Madame Pauline, huyu Edina ni binti yangu na si msichana na mchezo mchezo."Kwa maneno hayo, yalimjulisha Kadili kuwa yule aliyekaa kwenye kiti cha enzi ni mama mzazi wa Edina. Binti ambaye amesababisha kutekwa na kuletwa pale kwa sababu tu ya kucheza naye muziki kwenye hoteli ya Blue Star kule Sinza jijini Dar es Salaam, mara tatu kwa siku tofauti.

"Binti yangu bado mdogo, halafu kifaa cha nguvu. Si unamuona? Huyu si msichana wa kuolewa na mtu kapuku kama wewe. Kula yako na vaa yako shida huyu unamuweza wewe? Hapa unaponiona, kichwa kinaniuma, maana wanaume kibao wenye wadhifa na pesa zao wametuma washenga kutaka kumuoa binti yangu, yaani sijui nimkubali nani nimuache nani. Halafu kanatoke kajitu kama wewe nako, eti nako kanajitia kutaka kupimana ubavu na watu hao," Alisema na kuonekana kama kuutua mzigo mzito uliokuwa kwenye kifua chake.

Kuna mawaziri, mapofesa, madaktari na wafanyabiashara wakubwa nchini mpaka watoto wa vigogo wanataka kumuoa Edina, hadi marubani wa ndege. Lakini kwa sababu ni lazima aolewe na mtu mmoja, nimetuliza kichwa ili nione kati ya hao nani anaweza kuwa mtu sahihi kwa binti yangu ili asiende kupata tabu kwa sababu mimi mwenyewe mama yake nimemzaa na kumlea kwa mapenzi makubwa. Amelelewa kitajiri na hajawahi kupata shida yoyote."

Kwa mara ya kwanza ndipo Kadili alipojua kuwa kumbe Edina hajaolewa kama walivyokuwa wakidhani na rafiki yake Meze na kwamba hata kule kulindwa na mabaunsa si kwa sababu ya wivu wa mwenye mali, bali ni mama yake ndiye aliyekuwa akimlinda binti yake na watu watakaoonekana kutaka kumrubuni binti yake.

"Hawa mabaunsa ndiyo waliokuja kumwambia huyu mama mambo yote yale, ndiyo maana nimeletwa huku." Kadili alijisemea mwenyewe moyoni.

"Sasa sikiliza we mbwa mtoto. Nisikilize kwa makini. Leo nakusamehe kwa sababu binti yangu Edina amelia sana kwa sababu yako ili usiuawe. Saa hizi tayari ungekuwa umeshawasili kuzimu. Yoyote anayeingia kwenye jumba hili kwa sababu kama zako, au zingine za utovu wa nidhamu huwa hatoki salama. Nadhani ulitembezwa kwenye yale makaburi ya wajinga wenzako. Kuanzia leo sitaki umfuatilie tena mwanangu. Umuogope kama ukoma. Sitaki kusikia habari zako tena hapa. Nikisikia chochote kile juu yako na binti yangu, au kutoa siri ya hiki kilichomo kwenye nyumba hii, basi tusilaumiane. Kwa sababu ni lazima uuawe. Haya toeni hii taka taka mkaitupe huko." Aliamrisha.

**Itaendelea Jumamosi**

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO



**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0767 223311


### KUPOTEA KWA CHETI



**DISMAS ALPHONCE GIBAYI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.4049-0024 kilichotolewa na GREE VIEW SEKONDARI mwaka 2017. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MWA/NY/RB/251064/2019.**

115408702

### KUPOTEA KWA CHETI



**RUPINDER KAUR** anatangaza kupotelewa na cheti (CSEE) chenye index namba **S.442/29** kilichotolewa na BUHANGIJA SEKONDARI mwaka 1994. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/MBU/RB/276665/2019.**

115408902

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA SINGIDA**

**LILILOPO SINGIDA**

**SHAURI LA MAOMBI YA ARDHI NA.38 YA 2019**

**NATIONAL MICROFINANCE BANK PLC: ................. MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**AUGUST JOHN MUSHI ..................................MJIBU MAOMBI**

**KWA: AUGUST JOHN MUSHI**
**POPOTE ULIPO TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI:**

Kwa kuwa mwombaji tajwa hapo juu ameleta maombi yake hapa Barazani ambayo maelezo yake yameelezwa katika nalala ya maombi, ambayo yanaweza kupatikana katika Baraza hili. Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria hapa Barazani tarehe 01/10/2019 saa 2:00 asubuhi siku ya kusikilizwa shauri hilo.
Unatakiwa uhudhurie wewe binafsi au mwakilishi wako anaetambuliwa kisheria siku na saa tajwa hapo juu.
**ANGALIA:** kushindwa au kupuuza kufika tarehe na saa iliyotajwa hapo juu, kesi itapangwa na kusikilizwa upande mmoja na uamuzi kutolewa bila ya wewe au mwakilishi wako kuwepo.
HATI hii imetolewa kwa AMRI yangu na CHAPA ya BARAZA hii leo tarehe 03 Mwezi wa september,mwaka 2019.

115408802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**Katika mahakama ya Mwanzo DODOMA MJINI,Wilaya ya DODOMA**

**MADAI NAMBARI 219/2019**

**MDAI: KHADIJA ABDALLAH MAKBEL**

**MDAIWA; OMARY ABDALLAH MAKBEL**

**Kwa : OMARY ABDALLAH MAKBEL**
**KARIAKOO - GEREZANI -DSM**

**KWA kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba**
**MADAI YA MIRATHI**

Kwahiyo Unahitajika kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya tarehe 19/9/ mwaka 2019 saa 2:30 asubuhi kwa kujibu madai na kwa kuwa siku hiyo ya kuitwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zilizohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Na kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama itathibitisha kama umepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe5/9/2019.

115408102

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**BALJIT SINGH PANDHER** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya SCANIA yenye namba za usajili **T 369 ALS, Chassis No. 1009736,** Engine No. **5206616.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/271335/2019.**

115408201

### VYETI VIMEPOTEA



**REHEMA JOHNSON MBWAMBO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0945/0062** kilichotolewa na KWIZU SEKONDARI mwaka 2015. Cheti cha Chuo chenye namba **TRCS/DSMR/FA/2017/029/LB/4** kilichotolewa na ST. RAPHAELY YOUTH TRAINGING CENTRE mwaka 2017. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi (IV) **DAR/GOG/RB/273190/2019.** Taarifa ya polisi Chuo: **DAR/GOG/RB/273089/2019.**

115407902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**(S.M.M. 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo: TEMEKE**

**Usimamizi wa Mirathi No. 357/2019**

**Ombi la JUMA MUSSA MPINGILWA kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya Marehemu SALAMA RASHID MASKATI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 16/09/2019. kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe........................

115407502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

**Anuani ya Simu:"WARAKA"** **Ofisi ya Baraza la Ardhi na Nyumba(W)**
**Simu 212009** **S.L.P 5058,**
**Telefax 2124576** **TANGA**
**(Makao makuu)**
**Simu 027-2642622- (Tanga)** **28/8/2019**

**YAH: SHAURI NAMBA 50 LA 2019**

**SHABANI HAMISI KATOGOLO.............................MDAI**

**DHIDI YA**

**BRAC TANZANIA FINANCE & ANOTHER ..................MDAIWA**

**KWA:**
**MAIMUNA MOHAMED – POPOTE ULIPO**

SHABANI HAMISI KATOGOLO, amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Tanga dhidi yako. Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 17/09/2019 saa tano kamili asubuhi (11:00). Hivyo basi, unatakiwa kufika katika Baraza hili bila kukosa. Vielelezo vyote vya kesi vinapatikana katika Masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Tanga. Endapo hutatekeleza haya, shauri litasikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.
AMRI: hii imetolewa na kutiwa Saini Muhuri/Lakiri wa Baraza hili leo tarehe 02/09/2019.

**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)**
**TANGA**

115407602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**Mahakama ya Mwanzo: ARUSHA MJINI**

**Wilaya ya ARUSHA**

**MADAI NAMBARI 94/2019**

**Mdai: GODLIZEN AINEA ISANGYA**

**amdai**

**Mdaiwa REBECA MARTIN KIVIMBA**

**Kwa REBECA MARTIN KIVIMBA.**

**Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba hapa habari za Madai.**

**FIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA KUJIBU MADAI YA TALAKA**

Kwa hiyo unahitajiwa /mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya JUMATATU tarehe 16/09/2019 saa 08:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo na shauri hilo kwa ajii ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 06/09/2019.

115407502

### KUPOTEA KWA KADI YA TRAILER

**BALJIT SINGH PANDHER** anatangaza kupotelewa na kadi ya **TRAILER** aina ya Trailer yenye namba za usajili **T 127 ANA,.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/271354/2019.**

115408201


Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# INTER

## YAJITOSA KUMSAJILI GOTZE

**MILAN, Italia**

KLABU ya Inter Milan inajiandaa kutoa ofa ya kumsajili fowadi wa Borussia Dortmund, Mario Gotze, wakati wa dirisha dogo la usajili Januari, kwa mujibu wa Sky Sports Italia.

Kocha Antonio Conte ameripotiwa kwamba anamtaka mshindi huyo wa kombe la Dunia mwaka 2014, na kwamba atapambana kuhakikisha anamsajili Januari mwakani.

Gazeti la Gazetta Dello Sport limedai kwamba Inter watatuma ofa kwa Dortmund, kwa ajili ya kumsajili mchezaji huyo ili kuimarisha safu yake ya ushambuliaji.

Gotze amebakiza miezi tisa katika mkataba wake wa sasa na Dortmund, na atakuwa huru wakati wa kipindi cha majira ya joto kijacho.

Hivyo Inter watakuwa na wakati mzuri zaidi wa kumsajili nyota huyo mwenye umri wa miaka 27 Januari kwani miamba hao wa Bundesliga hawatakuwa tayari kumuachia aondoke huru.

Gotze alikuwa kizazi cha dhahabu akikulia kwenye akademi ya Dortmund kabla ya kutimkia kule Bayern Munich.

Gotze alicheza mechi 73 kwa miamba hao wa Bavaria na kufunga mabao 22.

## MKHITARYAN HAJUI HATIMA YAKE ARSENAL

**ROME, Italia**


MCHEZAJI Henrikh Mkhitaryan amesema kwamba hajui hatima ya majaliwa yake pale Arsenal baada ya kutolewa kwa mkopo katika klabu ya AS Roma.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 alitua Inter kwa mkopo wa muda muda mrefu baada ya miezi 18 tangu ajiunge na washikabunduki wa London.

Alipoulizwa kuhusu kucheza hapo kwa mkopo wa muda mrefu baada ya timu yake ya taifa ya Armenia kufungwa mabao 3-1 na Italia kwenye mchezo wa kufuzu Euro 2020, Mkhitaryan alisisitiza kwamba amejipanga kuitumikia Roma. "Kwanza tuangalie kile nitakachokifanya Roma na mwisho wa msimu nafikiri nitaangalia uwezekano wa kubaki au kwenda sehemu nyingine, kwa sasa sijui," alisema kiungo huyo akiiambia VBET.

"Sasa, siwezi kusema chochote kuhusu majaliwa yangu, kwa sasa tuangalie kwanza mechi zinazokuja."

Roma kwa sasa ipo nafasi ya 15 kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya England, Serie A.




## MEUNIER KUONDOKA PSG JANUARI

**PARIS, Ufaransa**

BEKI wa Paris Saint-Germain, Thomas Meunier amebainisha wazi kwamba anaweza kuondoka klabuni hapo wakati wa dirisha dogo la usajili Januari mwakani.

Mchezaji huyo amekuwa kihusishwa na mpango wa kutakiwa na klabu za Manchester United na Arsenal.

Huku mkataba wake ukiwa unakaribia kukamilika kipindi cha majira ya joto kijacho, mchezaji huyo raia wa Ubelgiji amekuwa akihusishwa na mpango wa kutaka kuondoka hapo Parc Des Princes.

Na sasa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 ameweka wazi kuwa kuna uwezekano mkubwa ataondoka Januari.

"Ulikuwa ni wakati wenye mambo mengi, huku klabu nyingi zikinitaka," amesema Meunier akiiambia RTBF wiki hii.

"Ningeweza kuondoka, lakini haikuwezekana kwa sababu ya klabu au mimi mwenyewe. Mambo hayakuwa sawa kwa asilimia 100.

"Mara zote nilisema kwamba nataka kubakia Paris. Bado nina mwaka mmoja kwenye mkataba wangu na bado natumaini naweza kuongezewa.

"Lakini hali ilivyo mambo yanaweza kwenda tofauti, kwani kwa sasa sio chaguo la kwanza kwenye kikosi, lakini mimi bado nataka kuendelea kucheza.

"Kucheza soka ndio kitu kinachokipenda, lakini unapokuwa huna namba maana yake kwamba nafasi yako ya kucheza inakuwa finyu na kila mchezaji anataka kucheza.

"Hivyo ni wazi kwamba, siwezi kuondoa uwezekano wa kuondoka Januari, maana nataka kwenda sehemu ambayo nitakuwa na nafasi ya kucheza mara kwa mara.

# EPL YATOA WACHEZAJI WENGI KIKOSI CHA FIFA

**LONDON, England**

LIGI Kuu ya England imetoa idadi kubwa ya wachezaji waliochaguliwa katika kikosi bora cha Shirikisho la soka la kimataifa, Fifa, cha wachezaji 11 katika kipindi cha miaka 10.

Wachezaji 21 kati ya 55 walioteuliwa wanacheza soka yao ya kulipwa nchini England huku ligi hiyo ikimaliza utawala wa ligi ya Hispania, LaLiga.

Wachezaji saba wa klabu ya Liverpool walioshinda ubingwa wa Ligi ya mabingwa Ulaya wameorodheshwa miongoni mwa wale watakaowania nafasi hizo 11 za kikosi cha Fifa ingawa Real Madrid na Barcelona wana wachezaji wengi zaidi.

Kikosi hicho cha wachezaji 11 kitafichuliwa katika tuzo bora za Fifa mjini Milan Septemba 23.

Zaidi ya wachezaji 23,000 wa kulipwa duniani walitakiwa kuchagua kikosi bora na Fifpro, muungano wa wachezaji kutokana na kiwango cha mchezo wao kati ya Julai, 2018 na Julai, 2019.

Kikosi cha wachezaji 11 kitakachochaguliwa kitashirikisha mlinda lango, mabeki wanne, viungo wa kati watatu na washambuliaji watatu.

Wachezaji wanne wa Liverpool ni miongoni mwa wachezaji 17 watakaoshiriki kwa mara ya kwanza akiwamo Trent Alexander-Arnold na Andrew Robertson, huku wachezaji maarufu kama vile Romelu Lukaku na David Silva wakikosa kura za kutosha kushiriki kwa mwaka wa pili mfululizo.

Huku Ligi ya England iliyo na wachezaji 21 ikimaliza utawala wa ligi ya La Liga yenye wachezaji 20 katika kipindi cha miaka 9 kama ligi yenye wachezaji bora.

Mabingwa wa Hispania, Barceona ndio klabu ilioshirikishwa na wachezaji wengi zaidi.



# MATIC atupa dongo kwa Solskjaer

**MANCHESTER, England**

KIUNGO wa Manchester United, Nemanja Matic, amesema Ole Gunnar Solskjaer atatakiwa kulaumiwa kama klabu hiyo haitakuwa kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu ya England msimu huu.

Matic mwenye umri wa miaka 31, alikuwa mchezaji muhimu wa United katika safu ya kiungo tangu alipotoka Chelsea mwaka 2017, lakini amecheza dakika 22 tu msimu huu akiwa anatokea benchi.

United, ambayo kwa mara ya mwisho ilishinda taji hilo mwaka 2013, kwa sasa inashika nafasi ya nane kwenye msimamo baada ya kucheza mechi nne za Ligi Kuu na inaburuzwa na vinara Liverpool kwa pointi saba.

"Kocha anatakiwa kuchagua timu ambayo itapigania ubingwa na kama hatashinda yeye ndiye atabeba mzigo wa lawama," alisema Matic akiwaambia waandishi wa habari wakati Serbia ikijiandaa na mchezo wa kufuzu michuano ya Euro dhidi ya Uren oleo Jumamosi.

"Nimekuwa kwenye soka kwa muda mrefu, nimecheza mechi zote kwa klabu kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita."

Solskjaer amekuwa akimchezesha Scott McTominay mwenye umri wa miaka 22 kama patina wa Paul Pogba kwenye kiungo ya kati katika mechi zote nne ambao wameshinda moja, kufungwa moja na sare mbili.

## Bale: Nilifanywa kuwa mbuzi wa kafara

**MADRID, Hispania**

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid, Gareth Bale, amesema kwamba alifanywa kuwa mbuzi wa kafara na kukaribia kuondoka kipindi cha majira ya joto na anaamini hawakumtendea haki.

Bale mwenye umri wa miaka 30, hakuwa kwenye mahusiano mazuri na kocha Zinedine Zidane wakati wa maandalizi ya msimu mpya, huku kocha huyo alibainisha kwamba Bale ataondoka, ingawa uhamisho wake wa kwenda klabu ya nchini China ya Jiangsu Suning ulikwama.

"Naelewa nilifanywa kuwa mbuzi wa kafara na sikuwa na furaha," amesema Bale akiiambia Sky Sports wakati Wales ikijiandaa na mchezo wa kufuzu michuano ya Ulaya dhidi ya Azerbaijan.

"Sikuwa na furaha namna nilivyokuwa natendewa, haikuwa haki kwangu, maana nilionekana kama vile sifai na lazima niseme kwamba, sikupendezwa na hali ile na sikuwa na furaha."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# NEYMAR KUMFUATA CRISTIANO JUVENTUS

●●●Mabingwa hao wa Italia wajipanga kutoa dau nono pamoja na Dybala ili...

**TURIN, Italia**

KLABU ya Juventus imetajwa kuwa kwenye mpango wa kumsajili Neymar ili aweze kuungana na mshambuliaji wao Cristiano Ronaldo, huku pia mabingwa hao wa Italia wakiwa tayari kumtoa, Paulo Dybala pamoja na pauni milioni 90 ili kuhakikisha Mbrazil huyo anatua klabuni hapo katika kipindi cha majira ya joto.

Neymar hakuficha uamuzi wake wa kutaka kuondoka Paris Saint-Germain katika kipindi hiki cha majira ya joto na kuweka wazi kwamba anataka kurejea Barcelona lakini mchakato huo ulishindwa kukamilika mpaka dirisha la usajili likafungwa.

Lakini baada ya dirisha la usajili kufungwa na Neymar kubakia PSG, gazeti la Tuttosport imebaini kuwa Juventus imeanza kufanya mchakato wa kuhakikisha inamsajili mshambuliaji huyo na kutengeneza safu bora ya ushambuliaji pamoja na Ronaldo katika klabu hiyo ya jijini Turin.

Neymar, ambaye yuko tayari kuitumikia PSG katika msimu huu huku klabu hiyo ikiendelea na utaratibu wa kujua hatima yake, ameamua kuachana na uamuzi aliokuwa ameuweka huku bado akiwa anajipanga kuona anarejea tena Hispania.

Dybala anatajwa kuwa kiunganisho cha kufanikisha uhamisho baada ya mchakato wake wa kujiunga na Manchester United na Tottenham kushindwa kukamilisha mapema mwezi uliopita.

Lakini Dybala anapotakiwa kujaribu kusimama na kuonyesha uwezo wake ili aendelee kubakia na Ronaldo katika klabu hiyo ya Turin, anashuhudia mchakato wa kumsajili Neymar unakuwa mwisho wake na kuwa sehemu ya majadiliano ambayo yanashusha thamani yake.

Tuttosport limeendelea kuandika kuwa kama Dybala alikuwa sehemu ya ofa ya Juventus kwenda kwa PSG ambayo ikakataliwa , watahitajika kuongeza kiasi cha fedha kwa ajili ya kumnasa Neymar, ambao walikuwa tayari kutumia pauni milioni 198 ili kumpata mshambuliaji huyo wa Barcelona miaka miwili iliyopita.

Ronaldo tayari ameshauelewa vema mfumo wa Juventus tangu alipotua klabuni hapo akitokea Real Madrid msimu uliopita na amekuwa mchezaji muhimu ambaye ameisaidia timu hiyo kushinda taji la nane mfululizo la Serie A.

Akiwa tayari ameanza kupachika mabao katika msimu huu, mreno huyo anatajwa kupewa mikoba ya kuhakikisha wanafanya vema na kurejea kwenye ufalme waliokuwa nao katika mwaka 1996, ambapo wamekaa bila ya kushinda taji la Ligi ya Mabinga Ulaya.

Kwa Neymar, sasa anatarajia kuungana na Thomas Tuchel katika kikosi hicho cha PSG baada ya kumalizika kwa kalenda ya mechi za kimataifa.

## KWA UFUPI

**DYBALA AISUMBUA SPURS**

TOTTENHAM itarejea tena kutuma ofa ya kutaka kumsajili mshambuliaji wa Juventus na Timu ya Taifa ya Argentina, Paulo Dybala (25), ambaye thamani yake imetajwa kuwa ni pauni milioni 65 wakati dirisha la usajili la Januari litakapofunguliwa baada ya kushindwa kukamilisha mchakato huo katika kipindi cha majira ya joto. ***(Star)***

**POGBA, UTD KUTETA**

MABOSI ya Manchester United wameanza mawasiliano na wakala wa Paul Pogba, ili kujadili uwezekano wa kumpa mkataba mpya kiungo Mfaransa baada ya mkataba wake wa awali kutarajiwa kumalizika mwaka 2021. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 26 anahusishwa na mipango ya kujiunga na Real Madrid katika kipindi cha majira ya joto. ***(L'Equipe, via Mail)***

**CITY KUIMARISHA ULINZI**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, anatarajia kusajili beki wa kati mpya katika kipindi cha usajili cha dirisha dogo hapo Januari hata kama beki wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Aymeric Laporte (25), anatarajia kurejea uwanjani hivi karibuni. ***(Mail)***

**WALKER NJIA PANDA**

BEKI wa kulia wa City, Kyle Walker (29), anahofia hatima yake katika Timu ya Taifa ya England baada ya Kocha Mkuu wa timu hiyo, Gareth Southgate, kumwacha katika kikosi chake alichokiita kwa ajili ya mechi za kufuzu kushiriki Kombe la Ulaya (Euro 2020) dhidi ya Bulgaria na Kosovo. ***(Star)***

**MEUNIER AJIWEKA SOKONI**

BEKI wa Paris St-Germain, Thomas Meunier (27), amekacha kutoa uamuzi kuhusiana na uhamisho wa dirisha dogo la Januari. Mlinzi huyo wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji anatarajia kumaliza mkataba wake na mabingwa hao wa Ufaransa katika kipindi cha majira ya joto mwakani na sasa anahusishwa na tetesi za kujiunga na Arsenal na Manchester United. ***(RTBF - in French)***

**ZIDANE, BALE MAMBO SAFI**

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane ameanza kukubaliana na tabia mpya ya mshambuliaji, Gareth Bale na anaamini kuwa nyota huyo mwenye umri wa miaka 30 pamoja na winga Mbelgiji Eden Hazard, watakuwa sehemu ya wachezaji muhimu kwenye kikosi hicho cha Bernabeu. ***(ESPN)***

**GIROUD KUTUA MAREKANI**

STRAIKA wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Olivier Giroud, ambaye ana umri wa miaka 32 amefungua milango kwa timu yotote inayomhitaji ambayo inashiriki Ligi Kuu Marekani hasa kwenye jiji la United States. ***(Mail)***

**LISBON: SPURS WALIJIKWAMISHA**

TOTTENHAM imeshindwa kukamilisha mchakato wa kumsajili kiungo wa Sporting Lisbon, Bruno Fernandes kutokana na ugumu na vipengele walivyoweka wakati wa kuwasilisha ofa, amesema rais wa klabu hiyo ya Ureno. Spurs ilikuwa tayari kulipa kiasi cha pauni milioni 40 na baadaye kumalizia pauni milioni 18 kama wangefanikiwa kutwaa taji la Ligi Kuu England na Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Evening Standard)***

**MKHITARYAN AFUNGUKA**

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Armenia, Henrikh Mkhitaryan (30), amesema kuwa ameamua kuondoka Arsenal na kujiunga na Roma kwa mkopo kwa sababu ya kukosa nafasi ya kucheza katika kikosi cha Gunners. ***(Mirror)***

**DIAS ANUKIA UNITED**

MANCHESTER United ilituma mawakala kwa ajili ya kumfuatilia beki, Ruben Dias (22), wakati Benfica ilipopata ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Braga wikendi iliyopita. Nyota huyo wa Timu ya Taifa ya Ureno anatajwa pia kuwindwa na Wolves. ***(Birmingham Mail)***

**CHONG KIMEELEWEKA**

WINGA wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Tahith Chong (19), amesema kuwa yuko katika mazungumzo ya kusaini mkataba mpya wa kuendelea kuitumikia Manchester United ambayo inatumia Uwanja wa Old Trafford. ***(Star)***

HABARI MICHEZO

# KIUNGO SIMBA AJIPANGA KUFANYA MAKUBWA DRC

**Na Somoe Ng'itu**

KIUNGO wa zamani wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba ya jijini Dar es Salaam, Uhuru Selemani, amesema kuwa anatarajia kwenda kucheza soka la kiwango cha juu katika klabu yake mpya ya FC Lupopo ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), imefahamika.

Uhuru amejiunga na FC Lupopo kwa mkataba wa miaka miwili akitokea Royal Eagles inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza nchini Afrika Kusini.

Akizungumza na gazeti hili jana, Uhuru, alisema kuwa bado anaweza kucheza soka la ushindani na anamatumaini klabu yake mpya itaridhishwa na huduma ambayo ataitoa kwenye kikosi hicho.

Uhuru alisema pia amefurahi kujiunga na FC Lupopo, kwa sababu itamfanya awe karibu na familia yake.

"Nimeondoka Royal Eagles, nawashukuru kwa ushirikiano wao kwa muda wote niliokuwa hapo, kwa sasa mimi ni mchezaji rasmi wa FC Lupopo ya DRC, nimesaini mkataba wa miaka miwili, pia ninafuraha kuona kwamba nitakuwa karibu na familia yangu," alisema Uhuru.

Aliongeza kuwa anafurahi kuona wachezaji wa Tanzania wanaendelea kupata timu nje, jambo ambalo linawasaidia wao binafsi na taifa pia.

"Kwa wanaopata nafasi ya kuitwa katika timu ya Taifa, wanaisaidia nchi kutokana na uzoefu wanaorudi nao, na wengine tunaendelea kupambana kwa ajili ya familia, si kwamba hatuna uwezo, ila ni nafasi ambayo hupatikana kwa wachache," Uhuru alisema.

Nyota huyo wa zamani wa Taifa Stars, ambaye sasa ni shabiki wa Wekundu wa Msimbazi, amedumu kwa muda wa miaka minne na kikosi cha Royal Eagles.



Golikipa wa Simba, Aishi Manula (kushoto), akifanya mazoezi chini ya kocha wa makipa wa timu hiyo, Mohammed Mwarami, kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Mtibwa Sugar itakayochezwa Septemba 17 mwaka huu jijini Dar es Salaam.
**PICHA: SSC**

## Jama Festival mambo yamenoga

**Na Renatha Msungu, Dodoma**

WATANZANIA wametakiwa kujitokeza kushiriki katika Tamasha la Utamaduni na Sanaa maarufu Jama Festival la Afrika Mashariki ambalo linatarajiwa kufanyika kati ya Septemba 21 hadi 29 mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Tamasha hilo litakwenda sambamba na tamasha la Urithi Festival ambalo lengo lake ni kutangaza utalii wa Tanzania.

Akizungumza jana jijini hapa, Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Juliana Shonza, alisema kuwa mpaka sasa zaidi ya wadau 2,000 wamethibitisha kushiriki katika tamasha hilo.

Shonza alisema kuwa maandalizi ya tamasha hilo ambalo lina sura ya kitaifa yanaendelea vizuri kutokana na ushirikiano unaoonyeshwa na wadau mbalimbali kwa kushirikiana na serikali.

Hata hivyo Shonza alisema wataalika wadau mbalimbali wakiwamo wabunifu na wachoraji ili kuonyesha bidhaa zao katika tamasha hilo.

"Nafurahi kuona mwitikio wa ushiriki wa wadau ni mkubwa mpaka sasa wadau zaidi ya 2,000 wamejitokeza, kwa upande wa wenyeji Watanzania ni 700," alisema Shonza.

Kutokana na hilo alisema jamii iendelee kujitokeza katika tamasha hilo ambalo litasaidia kutangaza utalii tulionao kupitia hifadhi mbalimbali pamoja na tamaduni zetu.

Naye Naibu Waziri wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Costantine Kanyasu, alisema anaipongeza kamati iliyoundwa kwa ajili ya maandalizi ya tamasha hilo ambalo linataka kuona vivutio vya utalii vilivyoko hapa nchini vinajulikana zaidi ndani na nje ya nchi.

Kanyasu alisema kuwa mwaka wizara yake iliandaa tamasha la Urithi kwa lengo la "kuichokoza" mikoa ili iweze kujiandaa kushiriki tamasha la Jama festival kwa ajili ya kuendelea kutangaza utalii wa ndani.

# Shiboub aufikiria ubingwa Ligi Kuu

**Na Mwandishi Wetu**

KIUNGO wa kimataifa wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara kutoka Sudan, Sharaf Eldin Shiboub, amesema kuwa akili na mawazo yake yote ni kupambana ili kuhakikisha wanashinda taji la ligi hiyo kwa mara ya tatu mfululizo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Sharaf Eldin Shiboub, alisema kuwa baada ya kutolewa kwenye mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, sasa nguvu ya kila mchezaji wa timu hiyo imehamia kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara. Shiboub alisema kuwa wamejipanga vema kupata ushindi katika kila mechi kwa sababu wanataka kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kutetea taji hilo na hatimaye kupata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa hapo mwakani.

"Malengo yetu ni kushinda mechi zetu zote, tumeongeza nguvu kwenye ligi, tunahitaji kufanya vizuri zaidi, tumejipanga na ninaamini tutafanikiwa," alisema Shiboub, kiungo huyo wa Timu ya Taifa ya Sudan.

Aliongeza kwamba hasira ya kutolewa mapema katika mashindano ya kimataifa, ndiyo inawafanya wajiweke tayari kushinda mechi za Ligi Kuu na kuwapa furaha mashabiki wa timu yao.

Simba ambayo ilianza kwa ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya JKT Tanzania, itaikaribisha Mtibwa Sugar katika mchezo wa raundi ya pili ya Ligi Kuu Bara utakaochezwa Septemba 17 mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

## Azam kuwakabili Pan African leo

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kujiimarisha kuelekea mchezo wao wa kimataifa wa Kombe la Shirikisho Afrika, kikosi cha Azam FC, kinatarajia kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya timu ya Pan African itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam.

Azam FC, inatarajia kuwakaribisha Triangle FC kutoka Zimbabwe katika mchezo wa kwanza wa raundi ya kwanza ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika utakaochezwa kati ya Septemba 13 na 15 mwaka huu hapa jijini.

Ofisa Habari wa Azam FC, Jaffer Iddi, alisema jana kuwa benchi la ufundi limependekeza kucheza mechi za kirafiki kwa lengo la kuendelea kuwaimarisha wachezaji wao ili waweze kupata matokeo mazuri katika mchezo huo wa kimataifa pamoja na Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Tunatarajia kucheza mechi nyingine ya kirafiki dhidi ya timu kongwe ya Pan African, kwetu tunaamini ni kipimo kizuri baada ya kumaliza mchezo dhidi ya timu ngumu ya Friends Rangers inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza," alisema kiongozi huyo.

Katika mechi ya kirafiki dhidi ya Friends Rangers iliyochezwa juzi, wawakilishi hao wa Tanzania katika michuano hiyo ya kimataifa walipata ushindi wa mabao 3-1.

Michezo

Jumamosi Septemba 7, 2019

Nipashe



Neymar kumfuata Cristiano Juventus HABARI UK 30

# SAMATTA: TUKO TAYARI KWA VITA

●●●Wajipanga kufanya makubwa kesho, lakini...



**Na Somoe Ng'itu**

NAHODHA na mshambuliaji tegemeo wa Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Mbwana Samatta, amesema kuwa wamejipanga kupambana na kucheza soka la kiwango cha juu katika mchezo dhidi ya wenzao kutoka Burundi utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, ili wapate ushindi na hatimaye kusonga mbele.

Taifa Stars inatarajia kuikaribisha Burundi katika mechi ya marudiano ya kuwania tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia za mwaka 2022 zitakazochezwa nchini Qatar, baada ya kutoka sare ya bao 1-1 huko mjini Bujumbura, Jumatano iliyopita.

Akizungumza na Nipashe jana, Samatta, alisema kuwa kila mchezaji anafahamu umuhimu na deni walilonalo la kuhakikisha wanapata matokeo mazuri katika mchezo na kutinga hatua ya makundi.

Samatta alisema kila mchezaji anajua mechi hiyo inatarajiwa kuwa na ushindani na ngumu kwa timu zote, na wao kama wenyeji wanahitaji kuongeza utulivu ili waweze kufikia malengo.

"Tutaingia uwanjani kwa lengo moja la kupambana, tunashukuru kwa ushirikiano mkubwa tunaoupata kutoka kwa wadau mbalimbali, hii inatufanya tuone kuwa tuna deni kwenu, ninaamini tutawapa furaha, ingawa Burundi si timu ya kuidharau," alisema Samatta, mshambuliaji wa zamani wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba na African Lyon, zote za jijini. -Naye Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Juma Mgunda, aliliambia gazeti hili kuwa kikosi chake kitacheza "kufa au kupona" kuhakikisha wanapata ushindi.

Mgunda alisema kwamba wanafahamu mchezo wa kesho utakuwa mgumu na bado kikosi hicho kina jukumu la kupambana ili kumalizia kazi waliyoianza ugenini Bujumbura.

"Kipindi kimoja cha mechi tulichocheza Burundi kimekwisha, yaani dakika 45 nyingine ni Jumapili, pamoja na vijana kujitahidi, kuna mapungufu ambayo tumeyaona, na kuna mazuri ambayo yamejitokeza, mapungufu tunayasahihisha na mazuri yaliyoonekana, tutayaongezea nguvu, kwa sababu tunajua kabisa, mchezo wa mwisho ni "Do or Die", lazima tuhakikishe tunapata matokeo yaliyokuwa mazuri," Mgunda, alisema.

Wakati huo huo, Katibu Mkuu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wilfred Kidao, alisema jana kuwa wachezaji walifanya kazi kubwa katika mchezo wa kwanza na wanatarajia watamalizia kazi waliyoianza ili kuwapa furaha Watanzania.

"Nawaomba Watanzania wajitokeze kwa wingi kuisapoti timu yetu ili tuweze kusonga mbele na kufanikiwa kuingia hatua ya makundi,"alisema Kidao. Alisema pia shirikisho limeamua kupanga kiingilio kidogo cha Sh. 2,000 kwa eneo la mzunguko na VIP B na C kwa Sh. 5,000 ili kutoa fursa kwa kila Mtanzania kwenda uwanjani kushuhudia mchezo huo ambao unatarajiwa kuwa na ushindani.

Naye Katibu Mkuu wa zamani wa shirikisho hilo, Angetile Osiah, aliwataka Watanzania kuwa kitu kimoja kuishangilia timu hiyo na kuachana na upenzi wa klabu kwa sasa.

"Watanzania tuwe kitu kimoja kuisapoti timu yetu ili tupate matokeo mazuri nyumbani, tuna wachezaji wazuri ambao watatuletea sifa katika Taifa letu,"alisema Angetile.

## Yanga waishtaki TFF serikalini

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Yanga umepeleka barua ya malalamiko katika Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ya kupinga adhabu iliyotolewa na Bodi ya Ligi Kuu ya kusimamishwa mechi tatu pamoja na kulipa faini ya Sh. 500,000 ambayo amepewa Kocha Mkuu wa timu yao, Mwinyi Zahera.

Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, alisema kuwa uongozi wa klabu hiyo umesikitishwa na adhabu hiyo iliyotolewa na bodi hiyo ambayo iko chini ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).

Mwakalebela alisema kuwa wanashangaa kuona Zahera anafungiwa kabla ya kupewa muda wa kusikilizwa, jambo ambalo linaonyesha udhaifu katika kusimamia ligi.

"Bodi ilitakiwa imuite kwanza Zahera na kumueleza makosa yake, hawezi kuisema bodi kama hakuna jambo, busara inasema kama mtu anazungumzia jambo mwiteni mumsikilize, bodi siyo Mungu ni watu tu," alisema kiongozi huyo.

Alisema kuwa klabu iko pamoja na kocha wao na wanaamini barua waliyoipeleka katika wizara husika, itapatiwa ufumbuzi na kumaliza hali ya klabu yao kuonewa.

Aliongeza kuwa pia Yanga inaweza wazi kwamba haitakuwa tayari kuvaa jezi yenye nembo nyekundu ya wadhamini wa Ligi Kuu Bara, Vodacom kwa sababu si utamaduni wa klabu yao.

" Ni kweli tuko katika hali mbaya ya kiuchumi, lakini isiwe sababu ya kuwafanya wageuke kanuni, taratibu na katiba ya klabu, kwani ni jambo ambalo haliwezekani," alisisitiza Mwakalebela.

Alimtaka Rais wa TFF, Wallace Karia, kufanya mazungumzo na Vodacom ili kubadili rangi ya nembo hiyo ili waweze kuivaa.

Wakati huo huo, Mwakalebela, alisema kuwa tayari wamepokea leseni ya golikipa, Farouk Shikalo, na kusema anaweza kusimama langoni katika mchezo wao wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Zesco kutoka Zambia unaotarajiwa kuchezwa Septemba 14 mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >